# Nipashe

Jumatatu Oktoba 28, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580060

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII



The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## 13 wa 'tuma kwa namba hii' wahukumiwa kulipa mil. 154/-

UKURASA 3




UKURASA 13

# Kipenga cha uchaguzi mitaa kupulizwa kesho

UKURASA 2



## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**GEREZA LAANZA KULISHA WAFUNGWA MIKOA MITATU**

GEREZA la Kilimo na Mifugo la Kitai, limeanza utaratibu kwa kulisha wafungwa...

UKURASA WA 5

**WASIOREJESHA FEDHA ZA USHIRIKA KUSHUGHULIKIWA**

MWENYEKITI wa Tume ya Ushirika, Dk. Titus Kamani, amewataka wanachama...


## Aomba Ikulu kupata mafao

UKURASA 2





Mvua kubwa inayoendelea kunyesha Mkoa wa Tanga ikiwa imekata daraja katika Kijiji cha Mandera wilayani Korogwe jana na kusababisha barabara kuu ya Arusha-Dar kufungwa. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mafuriko yaua 13, yaacha mamia bila makazi

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** **UPEPO WA KISULISULI WAGEUKIA YANGA** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Askari aomba Ikulu kumsaidia apate mafao

**Na Mwandishi Wetu**

ASKARI mstaafu, Thomas Sebastian, amemwomba Rais John Magufuli, kumsaidia kupata mafao ya Sh. milioni 47.2 anazodai kutoka mfuko wa hifadhi ya jamii kwa watumishi wa umma (PSSSF).

Sebastian aliyesajiliwa PSSSF kwa namba 4894928, alisema amesotea mafao ya Sh. 47,162,022.22 kwa muda mrefu bila mafanikio.

Akinukuu maelezo ya uliokuwa mfuko wa hifadhi ya jamii kwa watumishi wa umma (PSPF) kabla ya kuunganishwa mwaka jana, ilisema angelipwa malipo ya mkupuo ya Sh. 23,581,011.11 na pensheni ya kila mwezi Sh. 253,559.26.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam, mstaafu Sebastian alisema aliajiriwa mwaka 1978 na ilipofika mwaka 2002 alishtakiwa kwa mauaji kesi iliyoendelea kwa miaka mitano.

Alisema kwa mujibu wa taratibu za kijeshi askari wa daraja lake anapokosea hufukuzwa kazi na kwamba alifutwa kazi hadi Juni 14, mwaka 2007, Mahakama Kuu ilipomwona hana hatia na kumwachia huru.

"Kwa mujibu wa sheria za kijeshi tangu siku tulivyopelekwa mahakamani mshahara na stahiki zangu zote zilifutwa. Lakini mkuu wa kazi aliamuru nirejeshwe kazini na kulipwa haki zangu zote ikiwamo kurudishwa tena PSPF," alisema.

**MKANGANYIKO**

Kwa miaka mitano aliyokuwa gerezani alikuwa akilipwa mshahara na alikatwa michango iliyoingizwa kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Watumishi wa Serikali (GEPF), japo hakuridhia kujiunga na mfuko huo, alisema.

Sebastian alifanyakazi miaka 37 na bila kujua alikuwa akichangia mifuko miwili ya PSPF na GEPF na kote hajalipwa mafao mbali na kupigwa danadana.

"Baada ya kurudi kazini na kuanza kufuatilia taarifa kwenye mfuko wa PSPF niligundua kwamba kuna pesa zimepelekwa GEPF na nilipofuatilia niliambiwa niende PSPF ambako kuna michango yangu," alisema.

Alisema alipofuatilia PSPF walibaini kuwa alistahili kulipwa Sh. 47,162,022.22.

"Januari 27, 2016 GEPF walinikabidhi hundi ya Sh. 7,574,513 na kuniambia ndicho kiinua mgongo changu ambacho nimelipwa baada ya kuitumikia nchi kwa miaka 37.6 jambo ambalo sikuliafiki," alisema na kuomba Ikulu imsaidie.

"Naomba kusaidiwa nipate haki yangu ambayo imepotea kwa muda wa miaka ya utumishi wangu,"

INAENDELEA UK. 8

# Kipenga cha uchaguzi S/Mitaa kupulizwa kesho

**Na Enock Charles**

KIPENGA cha uchaguzi wa serikali za mitaa kinatarajiwa kupulizwa kesho, wakati fomu za kuwania nafasi mbalimbali katika uchaguzi huo zikianza kutolewa.

Nafasi zinazogombewa ni Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji Midogo, Mwenyekiti wa Mtaa na wajumbe wa Kamati ya Mtaa (Kundi mchanganyiko la wanawake na wanaume) na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa (kundi la wanawake) katika Mamlaka za Miji.

Nyingine ni Mwenyekiti wa Kijiji, wajumbe wa Halmshauri ya Kijiji (Kundi mchanganyiko la wanawake na wanaume), Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji (kundi la wanawake) na Wenyeviti wa Vitongoji katika Mamlaka za Wilaya.

Uchaguzi wa kuwapata viongozi hao unatarajiwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu, huku mchakato wa fomu za kuwania nafasi hizo zikitarajiwa kutolewa kesho na kukamilika Novemba 4 ikiwa ni takribani siku 26 kabla ya uchaguzi kufanyika.

Kwa mujibu wa ratiba, uteuzi wa wagombea ambao hufanywa na msimamizi wa uchaguzi katika kata husika, unatarajiwa kufanyika Novemba 5, mwaka huu, kwa nafasi za Mwenyekiti wa Kijiji/Mtaa, ujumbe wa halmashauri ya kijiji/mtaa kuanzia saa 2:00 asubuhi na kukamilika saa 10:00 jioni, huku kampeni zikitarajiwa kuanza Novemba 17 hadi 23 mwaka huu.

Kwa mujibu wa mwongozo uliotolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ulieleza kuwa msimamizi wa uchaguzi atafanya uteuzi wa wagombea wa nafasi za uongozi katika ngazi zote kuanzia Novemba 5, 2019.

Pia ilieleza kuwa mgombea au mtu aliyeomba kuteuliwa anaweza kuweka pingamizi kuhusu uteuzi wa wagombea na litawasilishwa kwa msimamizi wa uchaguzi kuanzia Novemba 5 hadi 6 na msimamizi atasikiliza na kutoa uamuzi kuanzia Novemba 5 hadi 7.

Kadhalika, endapo mtu hakuridhika na uamuzi utakaotolewa na msimamizi wa uchaguzi atatakiwa kupeleka shauri lake katika kamati ya rufani itakayosikiliza na kutoa uamuzi katika kipindi cha siku nne tangu kupokelewa kwa rufani hiyo, iwapo hakuridhika kanuni zinaelekeza shauri litapelekwa katika Mahakama ya Wilaya na kutolewa uamuzi ndani ya siku 30 baada ya matokeo ya uchaguzi kutangazwa.

Mwongozo pia ulitaja sifa za mgombea ni pamoja na: "Raia wa Tanzania, awe na umri wa miaka 21 au zaidi, anaweza kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza, ana shughuli halali ya kumwezesha kuishi, ni mwanachama wa chama cha siasa na amedhaminiwa na chama hicho, hajawahi kupatikana na hatia kwa kosa la utovu wa uaminifu katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi, hana ugonjwa wa akili.

Uchaguzi huo unatarajiwa kuhusisha watu milioni 19.7 sawa na asilimia 86 ambao walijitokeza kujiandikisha katika daftari la orodha ya wapigakura, wanaume ni 9,529,992 na wanawake ni 10,151,267 ikiwa ni ongezeko la watu milioni nane waliojindikisha mwaka 2014 ambapo idadi ilikuwa watu 11,882,086.



Mhandisi wa Maji wa Shirika la Water Mission Tanzania, Opita Tarcicous (kushoto), akitoa maelezo kwa ujumbe wa wakurugenzi waandamizi kutoka Water Mission International na The Grundfos Foundation (Poul Due Jensen Foundation) wakati wa uzinduzi wa mradi wa maji katika kambi ya wakimbizi ya Nyarugusu mkoani Kigoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mafuriko yaua 13, yaacha mamia bila makazi

**Na Waandishi Wetu**

MVUA zinazoendelea kunyesha nchini zimeendelea kusababisha vifo na uharibifu wa miundombinu, huku mamia ya wananchi wakikosa makazi.

Mvua hizo ambazo zilianza mwanzoni mwa mwezi huu kwa kunyesha katika mikoa mbalimbali zimesababisha vifo vya watu 13 ambako 11 vimetokea mkoani Tanga, hadi sasa, huku mkoani Mwanza watoto wawili wakifariki.

Kadhalika, mkoani Mwanza kaya zipatazo 158 zimeathiriwa na mvua hizo zilizoambatana na upepo mkali.

**MWANZA**

Katibu wa Kamati ya Maafa wa Wilaya ya Nyamagana, Masatu Magafu, alisema kaya 158 katika kata nne za Wilaya ya Nyamagana zimeathirika kutokana na mvua kubwa iliyoambatana na upepo mkali iliyonyesha Oktoba 24 kuanzia majira ya saa 11 jioni na kusababisha vifo vya watoto wawili.

Alisema kata zilizoathirika kutokana na mvua hizo ni Kishiri ambako kaya 66 zimekosa sehemu za kulala, Igoma kaya tatu, Igogo kaya mbili na kaya 87 za mitaa ya Kata ya Lwanima.

Alisema mvua hizo pia zimesababisha vifo vya watato wawili ambao ni Yohana Maiko, mwanafunzi wa darasa la pili katika Shule ya Msingi Mahina aliyeangukiwa na ukuta wa nyumba yao na Vaileth Godfrey (3), mkazi wa Igogo ambaye alisombwa na maji ya mvua na mwili wake kupatikana katika Ziwa Victoria baada ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Nyamagana wakishirikiana na uongozi wa kata na wananchi.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Handemi, DK.

INAENDELEA UK. 26

## HABARI KITAIFA




Waziri wa Biashara na Viwanda, Innocent Bashungwa, akipata maelezo ya bidhaa za mvinyo zinazozalishwa na Tanzania Distilleries Ltd, chini ya kampuni ya TBL Group kutoka kwa Meneja Mauzo Kanda Kusini, Mwesiga Muchuruza (kushoto) wakati alipotembelea banda la maonyesho la kampuni hiyo, katika maonyesho ya Urithi Festival jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 13 wahukumiwa kulipa mil. 154/- kudai fedha mtandaoni

**Na Hellen Mwango**

WATU 13 wamehukumiwa kulipa fidia ya zaidi ya Sh. milioni 154 na kutumikia kifungo cha nje cha mwaka mmoja baada ya kutiwa hatiani kwa kukiri kosa la kutuma ujumbe wa kielektroniki bila ridhaa ya wapokeaji na kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Hukumu hiyo ilisomwa mwishoni mwa wiki na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es salaam, Kelvin Mhina, baada ya washtakiwa kukiri makosa yao.

Washtakiwa hao ni Boniface Maombwe (23), David Luvanda(31), Moshi Sungura (32), Amos Bosco (21), Lule Kadenge (40), Jofrey Kapangamwaka (27), William Nturo (26), Regius Mauka (34), Collins Mwang'omolan (27), Francis Kapalata (26), Kasonde Kapela (40), Enock Mwandaji (35) na Pascal Kiatu (42).

Hakimu Mhina alisema washtakiwa hao walipe faini ya Sh. milioni 10 kama ingizo la awali na kiasi kilichobakia cha Sh. 144,032,830 kila mshtakiwa anatakiwa kulipa Sh. 11, 079,448 ndani ya miezi 12 (mwaka mmoja tangu hukumu iliposomwa).

Mbali na adhabu hizo mahakama iliwahukumu washtakiwa hao kila mmoja kutumikia kifungo cha nje ya miezi 12 na kutaifisha vifaa vya kielektroniki vikiwamo simu 34, laini za simu, flashi pamoja na kompyuta tatu kuwa mali ya serikali.

Hakimu Mhina alitoa hukumu hiyo baada ya washtakiwa hao kuingia makubaliano na Mkurugenzi wa Mashaka (DPP), kuihakikishia mahakama kwa njia ya kiapo kuwa makubaliano hayo kwa hiari yao bila ya kuwapo kwa vitisho vyovyote. Kabla ya kutoa hukumu hiyo, Hakimu Mhina aliwataka washtakiwa hao walijieleze ni kwanini mahakama isiwape adhabu.

Washtakiwa hao kwa nyakati tofauti waliomba kupunguziwa adhabu kwa sababu ni wakosaji wa mara ya kwanza, na kwamba kukaa kwao gerezani wamejifunza mengi. Kwa nyakati tofauti washtakiwa hao walidai walijiingiza kwenye vitendo hivyo kutokana na makundi kwa kuwa hawakuwa na hofu ya Mungu ndani yao, hivyo sasa wamejifunza kuwa na hofu ya Mungu na wamegundua makosa yao wanayajutia. Pia walidai wengine walijiingiza katika makosa hayo kutokana na ugumu wa maisha, walikuwa wakihangaika huku na kule wakajikuta wamejiingiza katika hali hiyo. Hata hivyo, wengine waliomba wasamehewe, wengine wafungwe kifungo cha nje cha miezi sita ili wakaitumikie jamii.

Kabla ya kutolewa kwa adhabu hizo, Wakili wa Serikali, Jacqline Nyantori, aliieleza mahakama kuwa hawana kumbukumbu za makosa ya nyuma za washtakiwa hao na akaiomba mahakama iwape adhabu kali ili iwe fundisho kwao na kwa jamii inayosambaza makosa kama hayo.

Pia aliiomba mahakama izingatie makubaliano ambayo washtakiwa hao waliingia na DPP, na kwamba iwapo watakiuka makubaliano hayo DPP atawarejeshea makosa aliyoyaacha awali.

Washtakiwa walikuwa wanadai kuwa kati ya Machi na Juni , 2018 katika mkoa wa Dar es Salaam na mkoa wa Rukwa na maeneo mengine ndani ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa nia ya udanganyifu, walisambaza ujumbe wa kielektroniki bila ridhaa ya wapokeaji.

Wakisomewa maelezo ya awali (PH) na Wakili wa Serikali, Janeth Magoho, ilidaiwa washtakiwa Maombwe, Luvanda, Sungura, Kapangamwaka, Mwang'omolan na Kapalata ni mawakala wa kampuni za simu za Vodacom, Airtel, Tigo na Halotel walisambaza ujumbe tofauti ukiwamo tuma pesa kwenye namba hii.

# Kamati Bunge yaagiza Sido kutengeneza bidhaa za ngozi

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, imelitaka Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido) kujenga vituo vya kutengeneza bidhaa za ngozi katika mikoa yote nchini ili kuwasaidia wajasiriamali wa ngozi.

Maelekezo hayo yalitangazwa jana na kiiongozi wa msafara wa wabunge wa kamati hiyo ambaye ni Mbunge wa Igalula (CCM), Mussa Ntimizi, kamati hiyo ilipotembelea kujionea kazi za uchakataji na uzalishaji mali wa mazao ya ngozi kwa vikundi vinavyohudumiwa na shirika hilo Dodoma.

Ntimizi alisema kamati inaona kuna umuhimu wa kujengwa vituo hivyo kulingana na rasilimali hizo ili kuwafanya wajasiriamali kujifunza mambo mbalimbali.

"Kamati imeitaka Sido kuhakikisha vituo hivyo vinakuwepo katika kila mkoa wenye rasilimali ili kuwainua vijana pamoja na wajasiriamali wa maeneo yanayozunguka mkoa husika.

"Kamati ilitoa agizo kuwa vituo hivyo vianzishwe katika mikoa yote ya Tanzania kulingana na rasilimali zilizopo katika mkoa husika, ili kuwasaidia vijana na wajasiriamali waliopo kwenye mkoa husika kujifunza, isibaki kuwa ni Dodoma yenye kituo cha kuzalishia bidhaa za ngozi," alisema.

Hata hivyo, alisema Sido imetakiwa kuendelea kutoa huduma hadi vijijini ili kuwafikia wananchi wengi zaidi kwa lengo la kuinua kipato chao kupitia elimu mbalimbali watakayokuwa wanapatiwa.

"Tumefurahi na kuhamasika na bidhaa zenye ubora zinazotengezwa na vijana katika kituo cha ngozi Sido kilichopo Kizota tukiwekeza vituo vingi vijana watapata ujuzi wa kutengeneza bidhaa zinazotokana na ngozi," alisema.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya, aliwataka wafanyabiashara wakubwa na kampuni kutumia bidhaa za ngozi kutoka kwa wajasiriamali wadogo ili kuwainua kiuchumi.

Akizungumzia utekelezaji wa maagizo hayo, Kaimu Mkurugenzi wa Masoko na Uwekezaji wa Shirika hilo, Shoma Kibende, alisema katika mpango mkakati wa sita Sido itaanzisha vituo mbalimbali kwa awamu kama vile mkoa wa Arusha , Manyara, Shinyanga kulingana na hali ya fedha ambayo shirika litakuwa limekusanya.


## TANGAZO KWA UMMA
## MATUMIZI MABAYA YA JINA LA
### BENKI YA MAENDELEO YA AFRIKA KWA UDANGANYIFU

Tumepata taarifa za mawakala mbalimbali wanaojivika nafasi za uongo za kusaidia katika kufanya biashara na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa nia ya kujipatia fedha. Udanganyifu huu mara nyingi hufanywa kwa kupitia barua-pepe, au njia nyingine za mawasiliano.

Benki ya Maendeleo ya Afrika inasikitishwa sana na udanganyifu huu, ambao ni ukiukwaji wa maadili ya taasisi, na itashirikiana na mamlaka zinazohusika kupambana na mtandao huo wa ulaghai.

**Sisi, Benki ya Maendeleo ya Afrika, tunathibitisha kwamba:**

- Hatudai wala kupokea malipo kutoka kwa watoa huduma, wagavi, wataalamu-washauri, wanaotafuta ajira, n.k., ili kuwapa mikataba ya kutoa huduma, ugavi wa bidhaa au malipo ili kutoa ajira.
- Tunatangaza waziwazi maombi yote ya manunuzi ya taasisi kwenye tovuti ya Benki, ambayo ni: **www.afdb.org/en/about-us/corporate-procurement**. Ikiwa ombi lolote la manunuzi halijatangazwa kwenye tovuti hiyo, ombi hilo halipo, ni ulaghai.
- Tunatangaza nafasi zote za ajira kwenye tovuti yetu: **www.afdb.org/jobseekers**. Kama nafasi ya ajira haijatangazwa kwenye tovuti hiyo, nafasi hiyo haipo, ni ulaghai.

Kwa hiyo, tunawashauri watu wote, pamoja na wafanya biashara wanaopenda kufanya biashara na Benki ya Maendeleo ya Afrika kuzingatia yafuatayo:

- Zingatia matangazo yanayohusu manunuzi, ambayo yanapatikana kwenye tovuti ya Benki tu, na si kwingineko.
- Kamwe usilipe au kutuma fedha kwa mtu yeyote ili kupata kazi, mkataba wa huduma au kufanya biashara yoyote na Benki.
- Toa taarifa za majaribio yote ya udanganyifu kwa mamlaka zinazohusika za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na pia ifahamishe Benki kupitia anwani hii ya **barua-pepe: security@afdb.org.**

215468802


# Gereza Kitai laanza kulisha wafungwa mikoa 3

**Na Mwandishi Wetu,**
SONGEA

GEREZA la Kilimo na Mifugo la Kitai, limeanza utaratibu kwa kulisha wafungwa katika mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli la kutaka Jeshi la Magereza kujitosheleza kwa chakula cha wafungwa. Mkuu wa Gereza hilo, Kamishna Msaidizi wa Magereza, Dk. Sylivesta Shija, alisema hayo wakati akisoma taarifa ya kilimo wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni.

Alisema lengo ni kuyapitia magereza yote ya kimkakati nchini yaliyoteuliwa kutekeleza agizo hilo.

"Mwaka 2018/2019, gereza hili liliingizwa kwenye mkakati wa wafungwa kujitosheleza kwa chakula na tumevuna magunia 5,528 yenye ujazo wa kilogramu 90 na kufanya tujitosheleze kwa chakula kwa asilimia 87.5 kwa mikoa mitatu ya Ruvuma, Lindi na Mtwara," alisema Dk. Shija.

Akizungumza baada ya kutembelea gereza hilo, Naibu Waziri Masauni, amemwagiza Kamishna Jenerali wa Magereza kupeleka timu ya wataalamu ili kutatua tatizo la ukame linalorudisha chini uzalishaji wa mazao gerezani hapo.

"Gereza hili lilipangiwa kulima ekari 1,000, lakini walilima ekari 950 pekee kutokana na changamoto mbalimbali ikiwamo ukame, sasa namwagiza CGP alete timu ya wataalamu ili waweze kutengeneza mpango kazi wa jinsi ya kutumia bwawa kubwa lililopo karibu na gereza ambalo linaweza kutumika kwa kilimo cha umwagiliaji na tukaondokana na hilo tatizo la ukame," alisema.

Mkakati wa gereza hilo kwa msimu wa mwaka 2019/2020 ni kuandaa shamba jipya lenye ekari 900 litakaloweza kulimwa mahindi ekari 750, maharage ekari 100, mihogo ekari 15, viazi ekari tano na ekari 30 maparachichi.

# Samia ahimiza wanawake Madola kugombea uongozi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA



MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ametoa rai kwa wanawake walioko kwenye nchi za Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika (CPA) zinazofanya uchaguzi mwaka huu na mwakani kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

Akizungumza jana jijini Arusha wakati akifungua mkutano wa Wabunge Wanawake wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika (CPA), Samia alisema ni wakati mwafaka kwao kutumia fursa ya chaguzi hizo zinazofanyika mwaka huu na mwakani katika nchi zao hususan Tanzania kugombea nafasi za uongozi.

"Jitokezeni kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika nchi zenu zenye uchaguzi mwaka huu na mwakani ikiwamo Tanzania," alisema.

Samia alisema wanawake wananafasi na haki sawa katika kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika vyama vyenu vya siasa hivyo vema wakasimama na kushindania nafasi hizo.

Alisema kwa miongo kadhaa nchi zao wameona jinsi utengwaji wa wanawake katika michakato ya uchaguzi umewaacha nyuma katika ajenda muhimu ya maendeleo hasa katika ufikiaji wa malengo ya ulimwengu, malengo endelevu ya maendeleo ambayo yanahitaji kufikia usawa wa kijinsia na kuwezesha wanawake na wasichana wote.

Pia alisema kukuza jamii zenye amani na umoja kwa maendeleo endelevu hutoa ufikiaji wa haki kwa wote na kujenga taasisi zenye uwajibikaji na zinazoweza kuhimili katika kila ngazi na ni moja ya kutimiza ajenda ya Umoja wa Afrika (AU) na mkataba wa Jumuiya ya Madola.

"Hivyo ni vema wanawake, wasichana mkatambua mnahaki sawa na wengine hasa katika kupigania usawa wa kijinsia, maendeleo endelevu na masuala mbalimbali mnahitajika sana katika kuendeleza nchi zenu," alisema.

Alisema nchi zote zimepata athari chanya kwa kupata nafasi za uongozi kwenye nchi zao.

Samia alimpongeza Rais John Magufuli kuonyesha kwa vitendo kwa kuwapa fursa wanawake kwenye nafasi mbalimbali za uongozi ambapo kwa sasa katika Bunge kuna wabunge wanawake 145 sawa na asilimia 36.9 ya wabunge wote.

"Kwa upande wa majaji wa Mahakama ya Rufani Tanzania kuna majaji wanawake 21 kati ya majaji 68 waliopo hapa nchini na majaji wa Mahakama Kuu wapo saba kati ya 20 sawa na asilimia 31.8 ya majaji waliopo nchini," alisema.

Naye Spika wa Bunge la Tanzania, Job Ndugai, alisema lengo la Tanzania kuhakikisha uwakilishi wa wabunge wanawake katika bunge hilo unafikia asilimia 50, ambapo kwa sasa ongezeko la wanawake lipo sawa na asilimia 30.

# Wasiorejesha fedha za ushirika kushughulikiwa

**Na Hellen Mwango**

MWENYEKITI wa Tume ya Ushirika, Dk. Titus Kamani, amewataka wanachama na viongozi wa vyama vya ushirika ikiwamo Saccos kurejesha mali na kulipa fedha wanazodaiwa na kwamba bila kufanya hivyo ni sawa na uhujumu uchumi.

Kadhalika, amesema mwanachama au kiongozi aliyepewa mali/fedha iwe kwa kuaminiwa na kukopa walipe kwa kuwa haraka kwa kuwa hakuna atakayeachwa ahujumu wanachama wa chama husika.

Rai hiyo aliitoa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam wakati akifungua Mkutano Mkuu wa mwaka wa chama cha kuweka na kukopa cha Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco Saccos).

"Viongozi na wanachama wa Saccos popote nchini walipokula na kupora mali za wanachama hatutawaacha tutawapeleka mahali salama, hao ni sawa na wahujumu uchumi kwa sababu wenzao wanajinyima wanaweka na manufaa ya kujiinua kiuchumi wao wanajinufaisha binafsi," alisema na kuongeza.

"Nawatangazia kabisa wale waliopewa kwa kuaminiwa na hawataki kulipa madeni yao au kurejesha mali za wanachama, mjiandae tutawafikia tu, hakuna jiwe ambalo halitapinduliwa mdokozi yeyote huyo ni sawa na mhujumu uchumi," alisema.

Aidha, alisema Tanesco Saccos ni, chama cha mfano wa kuigwa wamekuwa mstari wa mbele kujiendesha wenyewe bila kutegemea taasisi ya fedha kutoka nje ya chama chao.

Alisema Saccos 86 kati ya 230 zinakabiliwa na tuhuma mbalimbali ikiwamo ubadhirifu na waajiri kutumia michango ya wanachama nje ya matakwa ya kisheria.

"Baadhi ya waajiri ni wasumbufu wanakusanya michango ya wanachama lakini wanaitumia kwa matumizi yao binafsi badala ya kutimiza matakwa ya sheria za ushirika, wengine wamefanya ubadhirifu wa mali za umma, tumeshawasilisha orodha kwa Waziri Mkuu kwa hatua na maelekezo zaidi," alisema Dk. Kamani.

Alisema kwa upande wa Tanesco Saccos wamepiga hatua kwa kutumia mtandao wao katika kuwahudumia wanachama.

Alisema wana wawatumie wataalamu zaidi kupata maelekezo kujua jinsi gani watakavyoingia kwenye uwekezaji na kwamba wawekeze kwa akili kwani hakuna ziada mbovu wanapowekeza.

Mwenyekiti wa Tanesco Saccos, Somoe Nguhwe, alisema chama chake kimeboresha huduma za kifedha kwa wanachama wake pasipokuvunja sheria ya kazi.

Alisema miongoni mwa sababu zilizoinua chama chake ni viongozi kuhakikisha kutokukopa mkopo kutoka taasisi yoyote ya fedha.

"Huduma zote za fedha zinapatikana ndani ya Tanesco Saccos kwa hiyo viongozi wetu hawaruhusiwi kuwa na mikopo katika taasisi yoyote ya fedha," alisema Nguhwe.

Alisema mtaji wa Tanesco Saccos kutoka mwaka 2017 mpaka 2018, umefikia Sh. bilioni 34.


## UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED
## MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES

| S/N | ITEM/TRANSACTION | | |
|---|---|---|---|
| SECTION A | SAVINGS ACCOUNTS | RETAIL | CORPORATE |
| 1 | FREEDOM SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 5,000 | |
| | Minimum operating balance | TZS 2,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | NIL | |
| 2 | GENERAL SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 20,000 | |
| | Minimum operating balance | TZS 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | TZS 1,000 | |
| 3 | EMPLOYEE SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS15,000 USD 15 | |
| | Minimum operating balance | TZS 2,000 USD 10 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Adhoc statement request | TZS 1,000/ PAGE | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 4 | SAVINGS ACCOUNT INDIVIDUALS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | 15,000 | |
| | Minimum operating balance | 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 5 | SAVINGS ACCOUNT SALARY | | N/A |
| | Required minimum opening balance | 15,000 | |
| | Minimum operating balance | 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 6 | SAVINGS ACCOUNT DOMICILARY | | |
| | Required minimum opening balance | USD10 | |
| | Minimum operating balance | USD 5 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | 1% per Transaction | |
| | Closing account | USD 5 | |
| 7 | U-CARE CHILDREN SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 20,000 USD 15 | |
| | Minimum operating balance | TZS 20,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | TZS 1,000 | |
| SECTION B | CURRENT ACCOUNTS | | |
| 1 | INDIVIDUAL CURRENT ACCOUNT | | BUSINESS CURRENT ACCOUNT |
| | Required minimum opening balance | TZS 30,000 | TZS 100,000 |
| | Minimum operating balance | TZS 10,000 | TZS 100,000 |
| | Monthly maintenance fee | TZS 10,000 | TZS 12,000 |
| | Cash withdrawal at counter | 1 PER MILLE | TZS A/C 1 PER MILLE |
| | Closing account | TZS 10,000 | TZS 10,000 |
| | Penalty for overdrawn account | PLR + 10% | TZS A/C PLR + 10% |
| 2 | DIPLOMAT ACCOUNTS | | |
| | Required minimum opening balance | USD 200 | N/A |
| | Minimum operating balance | USD 100 | N/A |
| | Monthly maintenance fee | NIL | N/A |
| | Cash withdrawal at counter | NIL | N/A |
| | Closing account | NIL | N/A |
| | Penalty for overdrawn account | NIL | N/A |
| | Outward fund transfers(TTs) | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 200 | N/A |
| | Inward fund transfers(TTs Incoming) | NIL | N/A |
| | FOREX exchange | Favourable rates will be applied | N/A |
| 3 | DOMICILIARY CURRENT ACCOUNT | | |
| | Required minimum opening balance | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 |
| | Minimum operating balance | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 |
| | Monthly maintenance fee | USD 12 or its equivalent | USD 15 or its equivalent |
| | Minimum search fees | USD 25/ EUR 25/ GBP 25 | USD 25/ EUR 25/ GBP 25 |
| | Cash withdrawal | 1% per Transaction | 1% per Transaction |
| | Cheque book - 25 LEAF | USD 10 or its equivalent | N/A |
| | Closing account | USD 10 | USD 10 |
| | Penalty for overdrawn account | PLR + 2% | PLR + 2% |
| | Transfer From TZS to DOMICILIARY/ DOMICILIARYto TZS | NIL | NIL |
| SECTION C | DEPOSIT ACCOUNTS | | |
| 1 | Call Accounts | | Call Accounts |
| | Minimum opening balance | TZS 1,000,000 | TZS 10,000,000 |
| | Minimum operating balance | TZS 1,000,000 | TZS 10,000,000 |
| | Monthly Average balance requirement | Negotiable | Negotiable |
| | Interest Rates | Negotiable | Negotiable |
| 2 | Term Deposits | | Term Deposits |
| | Minimum deposit - local currency | TZS 500,000 | TZS 10,000,000 |
| | Minimum deposit - USD | USD 1,000 | USD 10,000 or equivalent |
| | Interest Rates | Negotiable | Negotiable |
| SECTION D | ELECTRONIC BANKING | | |
| 1 | E-Banking | | E-Banking |
| | Internet banking monthly subscription | TZS 2,000 Per Month. | TZS 10,000 per Month |
| | Internet banking ( Re issue pin) | TZS 5000 | TZS 5000 |
| | U - Direct (Reversal of transaction) | TZS 4000 | TZS 4000 |
| | E-statement (self downloaded) | FREE | FREE |
| | POS purchase (Local) | FREE | N/A |
| | POS purchase (International) | TZS 6000 (up to 1000$) TZS 10,000 ($1001 - $2000) TZS 20,000 (Above $ 2000) | N/A |
| | ATM reversal | TZS 1,000 per transaction | N/A |
| | Fund transfer/ company load | TZS 1,000 per transaction | TZS 1,000 per transaction |
| | Card Load | TZS 1,000 per transaction | TZS 1,000 per transaction |
| | Manual pin change | TZS 1,500 per transaction | TZS 1,500 per transaction |
| | U-MOBILE(mobile banking-Bank to wallet) | TZS 1,000 (0 - 200,000/=) and TZS 2,000 (200,001 - 400,000/=) | N/A |
| | Card to card transfer | TZS 1,500 per transaction | TZS 1,500 per tr |
| | Africash | TZS 6000 + 1.5% of the amount sent/USD 4.45 + 1.5% | N/A |
| 2 | Visa Debit Card | | N/A |
| | Issuance fees | TZS 10,000 | |
| | Re-issuance fee | TZS 10,000 | |
| 3 | Visa Perapid Cards | | N/A |
| | Issuance fees for instant card | TZS 12,000 | |
| | Issuance fees for personalized card | TZS 16,000 | |
| | Re-issuance fees | TZS 12,000 | |
| | Online Passcode reset fee | TZS 1,500 | |
| | ATM Pin reset fee | TZS 1,500 | |
| | Loading fee | TZS 1,000 | |
| | Online shopping fee - Local transactions | FREE | N/A |
| | Online shopping fee/Web - Int. transactions | TZS 6000 (up to 1000$) TZS 10,000 ($1001 - $2000) TZS 20,000 (Above $ 2000) | N/A |
| 4 | ATM Withdrawals | | N/A |
| | At UBA ATMs (On us) | TZS 500 | |
| | ATM Balance inquiry(Local) | TZS 200 | |
| | ATM Balance inquiry(international) | TZS 1000 | |
| | To other banks ATM (On others/OFF US)Local | TZS 2,500 | |
| | international ATM withdraw | TZS 6000 | |
| SECTION E | ASSET BANKING | | |
| 1 | LOANS | | |
| | Processing fee | negotiable | 2% |
| | Insurance for personal loans | N/A | 1.50% |
| | Legal fees | 0.5% minimum of TZS 300,000 | 0.5% minimum of TZS 300,000 |
| 2 | TEMPORARY OVERDAFT (TODs) | | |
| | Processing fee | 2% | 2% |
| SECTION F | TRADE FINANCE | | |
| 1 | Guarantees | | Guarantees |
| | Facility Commission | 2% p.a (0.5% per qtr). Min USD 250 per qrt. | 2% p.a (0.5% per qtr). Min USD 250 per qtr. |
| | Arrangement fees | 2% | 2% |
| | Cash Covered | 0.5% per qtr Min 250 per qtr | 0.5% per qtr Min 250 per qtr |
| | Amendment | USD 100.00 flat | USD 100.00 flat |
| | Extension to next quarter | 0.5% per qtr ( Or % of the agreed rate) | 0.5% per qtr ( Or % of the agreed rate) |
| | Amount increase | 0.5% /qtr on the diff ( Or % of the agreed rate) | 0.5% /qtr on the diff ( Or % of the agreed rate) |
| 2 | Letters of Credit - Imports | | Letters of Credit - Imports |
| | Issuance commision | 0.5% per quarter. Min USD 150. | 0.5% per quarter. Min USD 150. |
| | Handling Fees | USD 100 flat | USD 100 flat |
| | Swift charge | USD 50 flat | USD 50 flat |
| | Amendment | USD 100.00 flat | USD 100.00 flat |
| 3 | Letters of Credit - Exports | | Letters of Credit - Exports |
| | LC Advising Commission | USD 200 flat | USD 200 flat |
| | Amendment advising commision | USD 100 Flat | USD 100 Flat |
| | Correspondences Swift charge | USD 50 flat | USD 50 flat |
| | Documents handling and examination fee | 1.5% of invoice amount ,min usd 200 | 1.5% of invoice amount ,min usd 200 |
| | Courier charge | USD 100 flat | USD 100 flat |
| | LC confirmation charges | 1.5% per quarter (only for confirmed usance lcs) | 1.5% per quarter (only for confirmed usance lcs) |
| 4 | Letters of Credit Refinancing | | Letters of Credit Refinancing |
| | Interest on refinance | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 |
| | Commission on refinance | USD 50 flat | USD 50 flat |
| 5 | Discounting on LC/Invoice/Cheque | | |
| | Interest on discounting | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 |
| | Commission on discounting | USD 50 flat | USD 50 flat |
| 6 | Bills Discounting (Bills of exchange including cheques) | | |
| | Interest on discounting | PLR +3%-local; International Lobor+8% | PLR +3%-local; International Lobor+8% |
| 7 | Documentary Collection - Export | | |
| | Handling charge | 0.25% of the invoice min USD 100 flat | 0.25% of the invoice min USD 100 flat |
| | Courier charge | USD 100 | USD 100 |
| | Corespondence commission | USD 50 Per tracer | USD 50 Per tracer |
| 8 | Documentary Collection - Import | | |
| | Handling Commission | 0.25%. Min USD 100 | 0.25%. Min USD 100 |
| | correspondence Swift charge | USD 50 | USD 50 |
| 9 | Outward Bills for Collection (clean collections & TCs) | | |
| | Handling Commision | 0.25% of value, min USD 75 or its equivalent | 0.25% of value, min USD 75 or its equivalent |
| | Dhl charges | usd 75 flat | usd 75 flat |
| | Returned foreign cheques | claimed charges + locally un re-covered charges | claimed charges + locally un re-covered charges |
| 10 | Inward Bills for Collection | | |
| | Handling Commission | USD 50 flat per collection | USD 50 flat per collection |
| | Swift charged | USD 40 flat per collection | USD 40 flat per collection |
| 11 | Local Currency Transactions | | Local Currency Transactions |
| | Outward remittances (TISS) | TZS10,000 PER TRANSACTION | TZS10,000 PER TRANSACTION |
| | Amendment fee for Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers by customer or by bank | TZS 10,000.00 OR ITS EQUIVALENT | TZS 10,000.00 OR ITS EQUIVALENT |
| | Inward Swift Transfers (TISS) | NIL | NIL |
| 12 | Foreign Currency Transactions | | Foreign Currency Transactions |
| | Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 500 | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 500 |
| | Telegraphic Overseas Charges/ OURS | USD/EUR/GBP 35 FLAT (OURS) | USD/EUR/GBP 35 FLAT (OURS) |
| | Amendment fee for Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers by customer or by bank | USD 10 FLAT | USD 10 FLAT |
| | Inward Swift Transfers | USD 10 FLAT | USD 10 FLAT |
| | International Money Order (IMO) | USD 30 per IMO | USD 30 per IMO |
| | Foreign cheques for collection | 0.25% of value. USD 75 min; USD 250 max; | 0.25% of value. USD 75 min; USD 250 max; |
| SECTION G | OTHERS | | |
| 1 | Statements | | Statements |
| | Monthly | FREE | FREE |
| | Adhoc requests | TZS 1,000/ PAGE | TZS 1,000/ PAGE |
| 2 | Cheque Books Issuing | | Cheque Books Issuing |
| | - 25 Leaf | TZS 15,000; USD 10 | N/A |
| | - 50 Leaf | TZS 30,000; USD 20 | N/A |
| | - 100 Leaf | TZS 45,000; USD 30 | TZS 45,000; USD 30 |
| | Counter cheque request | TZS 20,000; USD 10 | TZS 20,000; USD 10 |
| | Cheque Stop payment instructions | leaf lost: TZS 20,000; Book lost: TZS 40,000; | Leaf lost: TZS 20,000; Book lost: TZS 40,000; |
| | Issuance of Manager's cheque | TZS 25,000; USD 20 per item | TZS 25,000; USD 20 per item |
| | Managers cheque cancellation charges | FREE | FREE |
| 3 | Standing order | | Standing order |
| | Standing order set-up | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent |
| | Standing order maintanance | NIL | NIL |
| | Standing order/Foreign Bank (TT charge) | MIN USD 50; 0.25% MAX USD 500 | MIN USD 50; 0.25% MAX USD 500 |
| | Amend / Stop standing Order | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent |
| | Unpaid standing order | TZS 40,000; USD 40 or its equivalent | TZS 40,000; USD 40 or its equivalent |
| 4 | Insufficient funds/effects not cleared | | Insufficient funds/effects not cleared |
| | Effects not cleared | **ITEM REMOVED** | **ITEM REMOVED** |
| | Insufficient Funds (Refer to drawer) | TZS 50,000; USD 50 | TZS 50,000; USD 50 |
| 5 | Other services/charges | | |
| | Retriving old documents (2-6 months) | TZS 10,000; USD 10 | TZS 10,000; USD 10 |
| | Retriving documents (6 months and above) | TZS 15,000; USD 15 | TZS 5,000; USD 15 |
| | Confirmation/Audit/ Certificate of balance | TZS 50,0,000; USD 25 or its equivalent | TZS 50,0,000; USD 25 or its equivalent |
| | Status enquiry / Reference Letters | TZS 25,000; USD 25 or its equivalent per customer request | TZS 25,000; USD 25 or its equivalent |
| | Manual processing of salaries | TZS 1,000; USD1 or its equivalent | TZS 1,000; USD1 or its equivalent |
| | Closure of Account | TZS10,000 | TZS10,000 |
| | Dormant Account Reactivation | FREE | FREE |
| | Cash handling fee-COINS ONLY | 9% of the Deposit | 9% of the Deposit |
| 6 | Soiled notes | 3% of principal amount | 3% of principal amount |
| 7 | Coins | 3% of principal amount | 3% of principal amount |
| | | | |
| | **approved by:** | | |
| | **Signature:** | | **Signature:** |
| | | | |
| | Flavia Kiyanga | | Chomete Hussein |
| | **Chief Operating Officer** | | **Country Chief Finance Officer** |
| | **United Bank for Africa (Tanzania) Ltd** | | **United Bank for Africa (Tanzania) Ltd** |
| | **Disclaimer: All fees are VAT exclusive.** | | |

UBA
Africa's global bank

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ndayiragije aachwe huru Stars akipewa ushirikiano

**HATIMAYE** Shirikisho la Soka nchini (TFF), limehitimisha mchakato wa kumsaka Kocha Mkuu wa timu ya Taifa, Taifa Stars kwa kumrasimisha Mrundi Etienne Ndayiragije aliyekuwa akikaimu nafasi hiyo.

Ndayiragije sasa amechukua rasmi mikoba ya Mnigeria Emmanuel Amunike aliyefungashiwa virago vyake baada ya matokeo mabaya ya Stars kwenye fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) nchini Misri mwaka huu.

Aidha, Ndayiragije ambaye wakati akikaimu nafasi hiyo alikuwa akisaidiwa na Kocha wa Polisi Tanzania, Selemani Matola pamoja na Kocha wa Coastal Union, Juma Mgunda, amekabidhiwa mikoba hiyo tayari akiwa ameipa Stars mafanikio.

Kocha huyo wa zamani wa KMC na Azam FC, ameiwezesha Taifa Stars kucheza hatua ya makundi kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia nchini Qatar 2022. Si mafanikio hayo tu, bali pia ameiongoza Taifa Stars kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zitakazofanyika nchini Cameroon Aprili mwakani.

Hakika Ndayiragije anaanza majukumu hayo rasmi akiwa na mafanikio makubwa, hivyo anahitaji kupewa ushirikiano mkubwa ili kuweza kuendelea kuwapa raha Watanzania kwa kuifikisha Stars mbali zaidi.

Tunauhakika Ndayiragije anaweza kufanya makubwa zaidi kama ataachwa afanye kazi yake akiwa huru pasi kuingiliwa katika majukumu yake wala kuwapo kwa shinikizo lolote kwake wakati wa kuchagua wachezaji wa Stars ama kupanga kikosi chake.

Tunatambua kuwapo kwa utamaduni kama huo ama kutoka kwa viongozi wa TFF au wa klabu kongwe, lakini kutokana na kelele za wadau wa soka kama si mashabiki husika wa klabu hizo.

Lakini pia, Nipashe hatuna budi kumsisitiza Ndayiragije katika kutekeleza majukumu yake hayo azingatie zaidi ubora na viwango vya wachezaji na asitekwe na nguvu kubwa za U-simba na U-yanga.

Kwa miaka kadhaa sasa tumekuwa tukishuhudia makocha wa Taifa Stars wakitekwa na U-simba na U-yanga hivyo kulazimika kutafuta uwiano wa wachezaji kutoka klabu hizo wakati wa kutangaza kikosi cha timu ya taifa.

Tunaamini kama ambavyo Ndayiragije katika mechi ya marudiano ugenini dhidi ya Sudan kuwania kufuzu CHAN, alivyofanya kwa kutompanga mchezaji hata mmoja wa Yanga na Stars ikashinda 2-1 ataendelea kuzingatia viwango na si ukubwa wa klabu mchezaji anapotoka.

Si kwa Yanga tu, lakini pia tumeshuhudia kipa namba moja wa Simba, Aishi Manula akipoteza nafasi Stars dhidi ya Juma Kaseja wa KMC ambaye anasaidiwa na Metacha Mnacha wa Yanga. Nipashe tunataka kuona mchezaji wa Simba ama Yanga na klabu nyinginezo anapata nafasi Taifa Stars kutokana na ubora na kiwango chake tu na si kuongozwa na ukubwa ama ukongwe wa klabu anayoichezea au kutafuta uwiano kutoka timu hizo.

Na hayo yote yatawezekana tu kama ambavyo TFF ya Rais Wallace Karia ilivyomwacha Ndayiragije kuamua mwenyewe wachezaji anaowataka na kutomwingilia katika upangaji wa kikosi chake.

Tunaamini huo ni mwanzo mzuri kwa Ndayiragije na sasa atakuwa na wigo mpana zaidi wa kuzunguka kila kona nchini kushuhudia mechi za Ligi Kuu na Ligi Daraja la Kwanza kusaka wachezaji wenye sifa ya kuunda kikosi chake.

Nipashe tunamtakia kila la kheri Ndayiragije katika kutekeleza majukumu yake hayo, huku pia tukiwaonya wale wote wenye tabia ya kuingilia majukumu ya makocha wa Taifa Stars sasa kuacha mara moja tabia hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Mkude, wenzake wafanyie kazi upungufu walionao

Na Adam Fungamwango

**HIVI** karibuni iliripotiwa kiungo mkabaji wa Simba, Jonas Mkude na wenzake kuchelewa ndege kwenda mkoani Kagera kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Kagera Sugar.

Mkude, pamoja na wachezaji wenzake Erasto Nyoni, Gadiel Michael, na Cleotus Chama walidaiwa kuchelewa kujiunga na wenzao na kubaki Dar es Salaam, hivyo kukosa mechi mbili dhidi ya Kagera Sugar na Biashara United.

Uongozi wa Simba ulitoa taarifa kuwa ungetolea ufafanuzi au adhabu kwa wachezaji hao, lakini ukakiri kuwa wachezaji hao ni watovu wa nidhamu.

Hata hivyo, baada ya kurejea wachezaji hao wameonekana kuungana tena na timu yao, huku taarifa zikieleza kuwa tayari wachezaji hao wameshamalizana ndani kwa ndani na uongozi.

Huenda wamesamehewa au uongozi umeamua kuwakata mishahara, adhabu ambayo inamwathiri zaidi mchezaji kuliko klabu. Unapomsimamisha mchezaji ni klabu ndiyo inaumia kwani haipati tena huduma ya mchezaji.

Wakati ilipotoka ripoti ya kwanza ya utovu wa nidhamu ya wachezaji hao, wengi walionekana kushangazwa tu na wachezaji watatu, Gadiel, Nyoni na Chama, lakini si Mkude.

Mashabiki wengi nchini ukiwasoma kwenye mitandao ya kijamii, hata wakihojiwa kwenye vipindi vya michezo, wanamtaja Mkude kama ni mchezaji ambaye huwa hashangai anapotajwa kwenye suala la utovu wa nidhamu, kuchelewa mazoezi na mengine yanayofanana na hayo.

Kabla hata hayajapoa, taarifa zinasema kuwa Mkude akazua tena tatizo siku ya Ijumaa, siku moja tu kabla ya timu hiyo kusafiri kwenda mkoani Arusha kucheza dhidi ya Singida United.

Inadaiwa kuwa Mkude aliwasili mazoezini nusu saa tangu wachezaji wenzake waanze mazoezi.

Baada ya kuteremka kwenye gari alikutana na Meneja wa timu, Patrick Rweyemamu ambaye alionyeshwa kuchukizwa na kumwonya kabla ya kwenda kukutana na Kocha Mkuu, Mbelgiji Patrick Aussems.

Mkude ambaye ni majeruhi alikutana na daktari Yassin Gembe baada ya mazungumzo hayo, lakini akawekwa kitimoto kuhusiana na kuchelewa kwake.

Inawezekana alichelewa kwa kudhani kuwa hahitajiki kufanya mazoezi kwa sababu ni majeruhi, lakini kitendo cha wakubwa zake kuchukizwa na kumuweka chini, kinaonyesha kuwa hata kama mchezaji ameumia, lakini anatakiwa awahi kama wenzake na wakishaanza mazoezi yeye anapewa mazoezi ya peke yake au matibabu.

Kama ni kweli Mkude alichelewa, sijaona mantiki yoyote ya kufanya hivyo kwani aliwasili na gari lake binafsi. Na kama atasema kuwa kulikuwa na foleni, iweje yeye tu ndiye achelewe hasa ikizingatiwa anadai kuwa na rekodi mbaya ya tabia hizi?

Inawezekana ikawa ni kweli alikuwa amechelewa kwa bahati mbaya, lakini mara nyingi mtu mwenye rekodi yoyote ambayo si nzuri, hata ikitokea kwake bahati mbaya, inaonekana ni makusudi tu na hakuna yeyote wa kumtetea.

Muhimu kwake ni kubadilika, kwani taarifa zake za utovu wa mara kwa mara ambazo tayari hata mashabiki wa Simba wameshaanza kuchoshwa nazo zinaweza kumletea matatizo mbele ya safari.

Siku viongozi wakichoshwa na yakiwafika shingoni wanaweza kufanya uamuzi mgumu ambao hautokuwa na tija kwake, matokeo yake kila mtu ataonekana mbaya kwake. Soka ni kazi kama kazi zingine, hivyo nalo linahitaji nidhamu ndani na je ya uwanja.

Ikumbukwe kwa sasa Simba ina Ofisa Mtendaji Mkuu mpya, Senzo Masingizi kutoka Afrika Kusini ambaye ameonekana kuwa mkali hasa kwa wale wote walio na tabia ya utovu wa nidhamu.

Huyu siyo Mtanzania ambaye anaweza kuwa na huruma na mchezaji kwa sababu ya kujuana, badala yake anaweza kufanya maamuzi magumu kutokana na sheria za kazi zinavyotaka, na watu wote wakashangaa. Kinachotakiwa kwake ni kubadilika, hata kama yanayosemwa kwake si kweli, lakini kuna asilimia fulani za ukweli, kwani haiwezekani inapotokea taarifa za utovu wa nidhamu basi na yeye anakuwa mmoja wa wanaokuwamo kwenye mkumbo.

# Askari aomba Ikulu kumsaidia apate mafao

**INATOKA UK. 2**

alisema.

**KUFUTIWA MASHTAKA**

Katika barua yenye kumbukumbu PHQ/C.8350/13 ya Feb 22, 2008 iliyotumwa Sebastian ikiandikwa na W.R. Gumbu, kwa niaba ya Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) yenye kichwa " kurejeshwa kazini," ilimweleza kuwa IGP, ameelekeza arudishwe kazini.

"...ujulishwe kwamba baada ya kupitia barua ya rufani pamoja na mwenendo mzima wa mashtaka ya kijeshi dhidi yako ameridhika kwamba hukustahili kutiwa hatiani na kufukuzwa kazini kwa fedheha.

"Hivyo basi kwa mamlaka niliyonayo chini ya KF.C.18 (3) IGP amefuta adhabu uliyopewa na kuamuru urejeshwe kazini kuanzia kuanzia Februari 22, 2008," ilisema barua hiyo. Aidha, ilimtaka kuripoti kwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, iliyempokea na kumpangia kazi.

Barua nyingine PHQ/205/4/VOL./XXXIV/90 ya Desemba 21, 2015, iliyotumwa Wizara ya Fedha, ilimwombea hati ya mshahara wa mwezi Juni 2010 ili aweze kukokotolewa mafao yake na mfuko wa PSPF.

Kwa mujibu wa taarifa ya uchangiaji iliyotolewa Februari 24, 2016, Sebastian ameanza kuchangia PSPF Agosti 25, 1999, akiwa analipwa mshahara wa Sh. 64,900 na akitoa Sh. 3,245 na mwajiri wake akimchangia 9,735.

Kuanzia Julai 31, mwaka 2008 akiwa na mshahara wa Sh. 205,670 alichangia Sh. 10,283 na mwajiri Sh. 30,850 ambayo ilikwenda hadi Juni 30, mwaka 2009 alivyoanza kulipwa Sh. 230,140 huku akichangia Sh. 11,507 na baada ya miezi michache mshahara uliongezeka kila wakati hadi 500,000 alipostaafu Januari 28, 2016 michango yake haikwenda kwenye mfuko.



Kwa mujibu wa hitoria hiyo, mshahara wa mwisho ni wa Junuari 30, 2015 aliolipwa Sh. 614,000 huku akipelekwa kwenye mfuko Sh. 39,700 na mwajiri akichangia Sh. 92,100. Aidha, historia hiyo ilionyesha kuwa idadi ya michango ni 103 kati ya iliyotarajiwa 199, na kwamba askari huyo amechangia Sh. 2,197,094 na mwajiri wake Sh. 6,591,284.

**MICHANGO GEPF**

Historia ya uchangiaji ilionyesha Sebastian mwenye namba 4894928 alianza kuchangia Machi 2001, ikiwa ni Sh. 6,490 kutoka kwenye mshahara wake na mwajiri Sh. 9,735, michango iliyoongezeka hadi kufikia Sh. 7,271 kwa Sh. 10,906.

Aidha, alichangia mara 57 na mwezi wa mwisho ulikuwa ni Januari 1, 2011, ikiwa ni Sh. 37,354 na mwajiri Sh. 56,031. Aidha, Juni 30, 2010, alichangia Sh. 829,699 na mwajiri Sh. 1,244,548.50, ikiwa ni mkusanyiko wa michango yake yote kwa kipindi alichokuwa jela.

GEPF ilionyesha kuwa michango yake ilikuwa ni Sh. 1,759,989, mwajiri alichangia Sh. 2,626,483 na kufanya jumla kuu kuwa Sh. 4,377,472.50.

Kwa mujibu wa hati ya mshahara ya askari huyo, alitakiwa kustaafu Julai 1, 2020, lakini alilazimishwa kustaafu kwa kuandika barua ya kuomba kustaafu kwa hiari na alifanya hivyo.

Hati ya mshahara ya Juni 30, mwaka 2010, ilionyesha kuwa alilipwa malimbikizo yake ya Sh. 8,066,250 na zilikatwa kwenda GEPF mfuko ukipokea Sh. 829,849 na PSPF Sh. 414,849.50. Aidha, baada ya makato hayo alibakiwa na Sh. 6,427,400 zilizolipwa kwenye akaunti yake.

**MAFAO PSSSF**

Barua ya PSSSF, kwenda kwa Sebastian kujibu barua yake, walisema kuwa barua zinaonyesha alistaafu akimilikiwa na masharti ya bakshishi hivyo kutakiwa kulipwa na mfuko wa GEPF na siyo PSPF.

"Hivyo basi kutayarishiwa mafao na mfuko wa GEPF ilikuwa ni halali yako kutokana na vielelezo kutokana kwa aliyekuwa mwajiri wake na taratibu zilizokuwapo," alisema Ramadhani Mkeyenge, aliyesaini barua kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF.

Askari huyo aliyestaafu kwa cheo cha sajini (namba S/SGT C. 8350), ilieleza kuwa amestaafu kwa umri wa hiari wa miaka 55, akiwa mkoani Arusha na alitunukiwa cheti cha utumishi uliotukuka na sifa ya askari aliyefuzu.

Canara Bank (Tanzania) Ltd.

(Together we can build a better life)

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2019 *(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 30 Septemba 2019 | Robo Mwaka uliopita 30 Juni 2019 |
|---|---|---|
| **A MALI** | | |
| 1 Fedha Taslimu | 451.67 | 662.76 |
| 2 Salio katika Benki kuu ya Tanzania | 8,437.49 | 8,129.05 |
| 3 Uwekezaji katika Amana za serikali | 29,524.24 | 30,837.70 |
| 4 Salio katika Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 258.50 | 2,181.48 |
| 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 84.85 | -5.68 |
| 6 Miamala Baina ya Matawi | 0.00 | 0.00 |
| 7 Bili zilizoafikiwa | 0.00 | 0.00 |
| 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0.00 | 0.00 |
| 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 26,170.00 | 21,280.00 |
| 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0.00 | 0.00 |
| 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 37,459.06 | 34,593.23 |
| 12 Mali Nyingine | 971.65 | 1,136.95 |
| 13 Uwekezaji wa Hisa | 0.00 | 0.00 |
| 14 Akaunti za udhamini | 0.00 | 0.00 |
| 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 785.76 | 829.16 |
| **16 JUMLA YA MALI** | 104,143.22 | 99,644.65 |
| **B DHIMA** | | |
| 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 26,750.00 | 28,050.00 |
| 18 Amana za Wateja | 40,912.39 | 33,657.05 |
| 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0.00 | 0.00 |
| 20 Amana Maalumu | 0.00 | 0.00 |
| 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0.00 | 0.00 |
| 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 0.00 | 0.00 |
| 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,133.45 | 793.16 |
| 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0.00 | 0.00 |
| 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0.00 | 0.00 |
| 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 0.00 | 0.00 |
| 27 Dhima Nyingine | 15.10 | 18.43 |
| 28 Madeni | 0.00 | 1,000.00 |
| **29 JUMLA YA DHIMA** | 68,810.94 | 63,518.64 |
| **30 MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29* | 35,332.28 | 36,126.01 |
| **C FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 32,830.00 | 32,830.00 |
| 32 Akiba ya Mtaji | 479.44 | 416.06 |
| 33 Mapato Yaliyobakizwa | 535.62 | 1,248.91 |
| 34 Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 849.41 | 631.04 |
| 35 Akaunti Nyingine za Mtaji | 637.81 | 0.00 |
| 36 Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0.00 | 0.00 |
| **37 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **35,332.28** | **35,126.01** |
| 38 Dhima Zisizo Dhahiri | 12,298.42 | 14,764.59 |
| 39 Mikopo Chechefu | 4,497.05 | 0.00 |
| 40 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 261.59 | 221.27 |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | 0.00 | 0.00 |
| **D BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 33.93% | 35.25% |
| (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo | 11.92% | 0.00% |
| (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 55.75% | 55.52% |
| (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 36.22% | 34.94% |
| (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 89.70% | 89.21% |
| (vi) Ongezeko la Amana | 9.65% | 0.21% |
| (vii) Ongezeko la Mali | 4.51% | 2.42% |

**Notisi**

*Mikopo Ghafi=Mikopo Halisi+Bili zilizoafikiwa+Tengo kwa ajili ya mikopo chefuchefu
*Jumla ya Amana = Amana za wateja + Amana za benki nyingine na Taasisi za fedha + Amana Maalum+ Madeni
*Mali zenye riba = Uwekezaji katika amana za serikali + Mikopo Halisi +bili zilizoafikiwa+mikopo iliyotolewa kwa benki nyingine + salio katika benki nyingine
* BENKI IMEANZA OPARESHENI 09 MEI 2016.

### KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA 2019 *(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo ya mwaka sasa 30 Septemba 2019 | Robo ya mwaka linganishi(mwaka uliopita) 30 Septemba 2018 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30 Septemba 2019 | Limbikizo la mwaka linganishi(Mwaka uliopita) 30 Septemba 2018 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 2,003.96 | 1,782.96 | 5,821.03 | 4,872.45 |
| 2 Gharama za Riba | 756.70 | 579.41 | 1,949.83 | 1,546.18 |
| 3 **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | 1,247.26 | 1,203.55 | 3,871.20 | 3,326.27 |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | 40.32 | 50.00 | 160.32 | 100.00 |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba** | 137.28 | 244.90 | 632.91 | 514.44 |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha | 19.30 | 17.04 | 105.98 | 56.74 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 117.98 | 227.86 | 526.93 | 457.70 |
| 6.3 Gawio | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| 6.4 Mapato Mengine | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | 947.18 | 1,073.97 | 3,054.38 | 2,956.50 |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 436.87 | 317.25 | 1,201.20 | 943.94 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 510.31 | 756.72 | 1,853.18 | 2,012.56 |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | 437.36 | 374.48 | 1,449.73 | 884.21 |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 160.00 | 115.00 | 440.00 | 205.00 |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | 237.04 | 209.48 | 849.41 | 579.21 |
| 11 Idadi ya Waajiriwa | 23 | 20 | 23 | 20 |
| 12 Mapato kwa Hisa | 7 | 6 | 26 | 18 |
| 13 Mapato kwa Hisa | 7 | 6 | 26 | 18 |
| 14 **Idadi ya Matawi** | 1 | 1 | 1 | 1 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (I) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.23% | 0.22% | 0.83% | 0.62% |
| (II) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 0.67% | 0.61% | 2.41% | 1.70% |
| (III) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 44.24% | 52.96% | 47.33% | 54.88% |
| (IV) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5.47% | 5.54% | 16.99% | 7.65% |

*Ada na kamisheni inahusisha ada ya wakaguzi,kodi na ada ya leseni na Bima
* uwiano wa faida kabla ya kodi na wastani wa mali=mapato halisi kabla ya kodi/wastani wa mali
*Mapato Ghafi =Mapato yasiyo na riba +Mapato ya riba
*Wastani= (opening +closing)/2

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA 30 Septemba 2019 *(Kiasi kwa shilingi milioni )*

| | Robo Mwaka ya sasa 30 Septemba 2019 | Robo Mwaka iliyopita 30 Juni 2019 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30 Septemba 2019 | Limbikizo la mwaka linganishi(Mwaka uliopita) 30 Septemba 2018 |
|---|---|---|---|---|
| **I Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 237.04 | 379.60 | 849.41 | 579.21 |
| Marekebisho kwa ajili ya: | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Hasara katika mali | 240.00 | 240.00 | 720.00 | 736.00 |
| -Badiliko halisi katika Mikopo | (2,906.15) | (2,807.01) | 0.00 | (7,601.51) |
| Faida/Hasara kwenye mauzo ya Mali | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Mabadiliko halisi katika Amana | 5,955.34 | 128.55 | 1,099.47 | 17,580.33 |
| Mabadiliko halisi katika Amana za muda Mfupi Zilizoafikiwa | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | -663.04 | 849.29 | -62.20 | 516.79 |
| Mabadiliko Halisi katika mali nyingine | 165.30 | 34.93 | 30.40 | -135.34 |
| Kodi iliyolipwa | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Mengineyo(bainisha) | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji | 3,028.49 | -1,174.64 | 2,637.08 | 11,675.48 |
| **II Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | | | |
| Gawio lililopokewa | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Ununuzi wa Mali za kudumu | -16.60 | -2.79 | -19.39 | -60.83 |
| Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Ununuzi wa Amana zilizoshughulikiwa na Mawakala | 1,313.46 | (4,525.47) | -6,776.56 | -1,675.52 |
| Mapato kutokana na mauzo ya Amana zilizoshugulikiwa na Mawakala | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Mengineyo(bainisha) | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji | 1,296.86 | -4,528.26 | -6,795.95 | -1,736.35 |
| **III Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | **0.00** | **0.00** | **0.00** | **0.00** |
| Mapato kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | **0.00** | **0.00** | **0.00** | **0.00** |
| Mapato kutokana na utoaji wa Mtaji wa Hisa | **0.00** | **0.00** | **0.00** | **0.00** |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | **0.00** | **0.00** | **0.00** | **0.00** |
| Mabadiliko halisi katika Madeni Mengine | **0.00** | **0.00** | **0.00** | **0.00** |
| Mengineyo(bainisha) | **0.00** | **0.00** | **0.00** | **0.00** |
| Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za kifedha | **0.00** | **0.00** | **0.00** | **0.00** |
| **IV Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha taslimu** | | | | |
| Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 4,325.35 | -5,702.90 | -4,158.87 | 9,939.13 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo mwaka/mwaka | 40,000.11 | 45,703.01 | 48,484.33 | 34,649.74 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni | 44,325.46 | 40,000.11 | 44,325.46 | 44,588.87 |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2019

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la Ziada ya jumla | Menginey (Bainisha) | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2019** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 32,830.00 | 0.00 | 506.62 | 0.00 | 416.06 | 0.00 | 33,752.68 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0.00 | 0.00 | 849.41 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 849.41 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Miamala na wanahisa | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Gawio lililolipwa | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Ziada ya Kisheria | 0.00 | 0.00 | 92.38 | 637.81 | 0.00 | 0.00 | 730.19 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0.00 | 0.00 | -63.38 | 0.00 | 63.38 | 0.00 | 0.00 |
| Mengineyo | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | 32,830.00 | 0.00 | 1,385.03 | 637.81 | 479.44 | 0.00 | 35,332.28 |
| **Mwaka Uliopita 2018** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 32,830.00 | 0.00 | 339.00 | 0.00 | 460.00 | 0.00 | 33,629.00 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0.00 | 0.00 | 579.21 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 579.21 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Miamala na wanahisa | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Gawio lililolipwa | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Ziada ya Kisheria | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 150.00 | -150.00 | 0.00 | 0.00 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Mengineyo | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | 32,830.00 | 0.00 | 918.21 | 150.00 | 310.00 | 0.00 | 34,208.21 |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2019

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha,sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita(kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka sasa,mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| T R BALAJI RAO (Ofisa Mtendaji mkuu) | (Imesainiwa) | 25th October 2019 |
| PETER JONATHAN MKANDE (Mkuu wa fedha) | (Imesainiwa) | 25th October 2019 |
| ZABLON GEORGE STAMBULI (Mkaguzi mkuu wa ndani) | (Imesainiwa) | 25th October 2019 |

**Sisi tuliotajwa hapo chini wajumbe wa bodi ya wakurugenzi tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na zinaonesha hali halisi.**

| *Jina* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| 1. PATRICK AMBWENE MUWOWO DIRECTOR | (Imesainiwa) | 25th October 2019 |
| 2. RAJAB SELEMENI KAKUSA DIRECTOR | (Imesainiwa) | 25th October 2019 |

**Canara Bank (T) Ltd**
**Head Office Dar Es Salaam Branch**
**Elia Complex P.O. Box 491, Dar Es Salaam, Tanzania**
**E:mail ctbl@canarabank.co.tz, T +255 222112530 (D) +255 222112532**
**www.canarabank.co.tz**

215482002

## HABARI KITAIFA

# Waliong'ara darasa la saba kujichagulia shule

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imeagiza wanafunzi waliofanya vizuri kitaifa kwenye mtihani wa darasa la saba na kuingia 10 bora mwaka huu wachague shule za umma za sekondari wanazotaka kusoma.

Agizo hilo lilitolewa jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Tamisemi), Selemani Jafo, wakati wa hafla ya utoaji wa Tuzo za Taifa za Elimu.

"Hawa wa darasa la saba waliofanya vizuri wachague shule wanazotaka tusiharibu ndoto zao, niliangalia kwenye mtandao yule aliyeongoza kitaifa akisema anatamani kwenda Ilboru sasa nitashangaa kama hatapata nafasi huko," alisema waziri.

"Nawahakikishia nyie mlioongoza darasa la saba Rais John Magufuli, anawapenda sana na mtachagua shule mnazotaka za umma na hii ni hatua muhimu ya kuwashika mkono wanafunzi wanaofanya vizuri," aliongeza Waziri Jafo.

Alitoa wito kwa wadau wa sekta binafsi kuendelea kuboresha elimu nchini akisema kuwa kadri wanavyofanya vyema kitaaluma na shule za serikali nazo zinaendelea kufanya vizuri.

Alisema wakati huu Tanzania inapoelekea kwenye uchumi wa viwanda kuna umuhimu mkubwa kwa wadau kuendelea kuiunga mkono serikali katika kuwekeza kwenye elimu.

"Suala la kuwekeza kwenye elimu halina mjadala, lazima tuweke mikakati ya kuendelea kuwekeza kwenye elimu, mimi na wasaidizi wangu tumejipanga kufanya mambo makubwa," alisema.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa Global Education Link, Abdulmalik Mollel, alisema wadau wa elimu wako wengi lakini hawana daraja linalowaunganisha na kwamba tuzo hizo ndiyo mwanzo wa ushirikiano.

Mollel alisema wanafunzi wanaofanya vizuri wamekuwa wakiomba kutambuliwa kutokana na kujiona kuwa wao ni wa kipekee hivyo utoaji wa tuzo hizo ni mwanzo mzuri wa kuwapa moyo kuendelea kufanya vyema kitaaluma.

Alisema kuna wanafunzi waliomaliza kidato cha sita na kufanya vizuri sana na wanachohitaji ni Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu isiwasahau kwenye mikopo.

# Wasaidia kutibu watoto saratani

**Na Frank Monyo**

KATIKA kuunga mkono jitihada za taifa za kutibu watoto wenye saratani, wadau wamekubaliana kuanzisha kituo cha matibabu mkoani Lindi ili kupeleka huduma karibu na wahitaji.

Miongoni mwa wadau hao ni kampuni ya uzalishaji gesi ya Pan African Energy (PAET), imesaini mkataba wa makubaliano (MoU) na Shirika la Kuhudumia Watoto wenye saratani la Tumaini la Maisha (TLM) kwa ajili ya kusaidia utoaji wa huduma za matibabu kwa watoto wenye saratani katika Hospitali ya Rufani ya Sokoine mkoani Lindi.

Makubaliano hayo yalisainiwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa PAET, Andy Hanna na Mwenyekiti wa Bodi ya TLM, Gerald Mongella, ambapo pande zote mbili zilieleza kuwa na imani na hatua hiyo ambayo ni mwanzo katika kufikisha huduma hiyo katika maeneo mengine nchini.

"Ushirikiano huu utasaidia katika utambuzi wa magonjwa ya saratani kwa watoto hususani kwenye maeneo yasiyofikika kwa urahisi hapa nchini baada ya kazi hii kufanyika katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Tunafarijika kuunga mkono jitihada hizi ambazo ni msaada mkubwa kwa watoto wote hapa Tanzania," alisema Hanna.

Aliongeza kuwa ushirikiano huo utaanza na uanzishwaji wa kituo cha matibabu mkoani Lindi ili kupeleka huduma karibu na wahitaji.


Canara Bank (Tanzania) Ltd.

**DISCLOSURE UNDER REGULATION 12 OF BANKING & FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS 2014**

**CUSTOMER COMPLAINT REDRESSAL MECHANISM: To The Esteemed Customers Canara Bank (Tanzania) Ltd Tanzania**

**1. INTRODUCTION (UTANGULIZI)**

The Complaints Resolution Desk (the Desk) has been established by the Bank of Tanzania (BOT) as a cost effective and efficient mechanism to resolve complaints between banking institutions and their customers. The Desk, which is fully funded by the Bank, is intended to resolve complaints (small claims) whose monetary value in respect of both the claim amount and remedy awarded does not exceed fifteen million Tanzania shillings (15,000,000) Mn.

**2. HOW TO LODGE A COMPLAINT WITH OUR BANK (JINSI YA KUWASILISHA MALALAMIKO KWA DAWATI)**

When you are dissatisfied with our services or you have any complaint pertaining to our staff or bank or otherwise, you may lodge complaint to us in writing by post or fax or through your registered email address on the following contact addresses.

**General Manager (Operations) Canara Bank (Tanzania) Ltd,**
**Dar es Salaam Branch,**
**Post Box 491 Dar es Salaam**
**Phone : +255 (22) 2112532**
**Fax: +255 (22)2112534**
**E Mail : cbtl@canarabank.co.tz**

**The Nodal Officer, Grievance Redressal Cell,**
**Canara Bank (Tanzania) Ltd**
**Post Box 491 Dar es Salaam,**
**Phone : +255 (22) 2112530;**
**Fax: +255 (22)2112534**
**E Mail compliance.cbtl@canarabank.co.tz**

**NOTE:**
- For lodging complaint with BOT please use Complaint Form No 1.
- For detailed information for lodging compliant with BOT please visit BOT website https://www.bot-tz.org.

**3. INTERNAL COMPLIANT RESLUTION MECHANISM (MCHAKATO WA KUTAFUTA UFUMBUZI WA MALALAMIKO)**

We through our internal complaint handling mechanism shall resolve your complaints within 21 working days from the date of lodging the compliant. The Internal Complaint handling mechanism in our Bank is as under:
- Receiving and timely processing consumers' complaints.
- Keeping complainants updated throughout the process.
- Keeping a record of all complaints and submit it to the Bank of Tanzania on quarterly basis.
- Resolving all consumer complaints within 21 working days from the date of lodging the complaint.
- In exceptional circumstances if we are unable to resolve the complaint within 21 working days, we will immediately inform the complainant of our inability and reason for the inability and what measures are being taken to resolve the matter urgently and in any case not more than 14 working days thereafter.

**4. HOW TO LODGE A COMPLAINT WITH THE DESK AT BANK OF TANZANIA (BOT) (NAMNA YA KUWASILISHA LALAMIKO KWA DAWATI LA BOT)**

If you are dissatisfied with the decision of our Bank in respect of your compliant or do not receive a response from our Bank within 21 working days from the date of lodging your complaint, you may within 14 working days lodge your complaint with the Desk at BOT. However, before lodging your complaint with the Desk at BOT, you are required to exhaust the Internal Complaints resolution mechanism of our Bank first.

The compliant with Complaints Resolution Desk at Bank of Tanzania shall be lodged in the prescribed form (Schedule A), duly signed by the complainant and shall be submitted in any of the following ways:

a) By hand or by post to:
Complaint Resolution Desk
Office of the Secretary to the Bank of Tanzania,
10 Mirambo Street,
11884, Dar es Salaam.

b) By electronic mail: complaints-desk@bot.go.tz
d) By facsimile to fax no: +255 22 2234067
e) By phone: +255 22 2233265/ +255 22 2233246

**Note:**
a) Complaints shall be lodged with the Desk from 9.00 AM to 12.30 Pm (Monday to Friday).
b) Your complaint must be lodged before expiry of two years after the cause of action arose.

**5. PECUNIARY JURISDICTION OF THE BOT DESK (MAMLAKA ZA KIFEDHA ZA DAWATI)**

The desk shall handle complaints whose total monetary value in respect of both the claim amount and remedy to be awarded does not exceed Fifteen Million Tanzania Shillings (TZS 15,000,000/-).

**6. ELIGIBLE COMPLAINTS (MALALAMIKO YA HAKI)**

Only the following categories of complaints are eligible for submission to the Desk;
a) A complaint against a banking institution which is either a member of the Tanzania Bankers Association or regulated by the Bank.
b) A complaint which is lodged within 14 days after a banking institution has delivered its decision or has failed to respond.
c) A complaint in respect of an incident which occurred less than two (2) years ago.

**7. INELIGIBLE COMPLAINTS (MALALAMIKO YASIYO NA HAKI)**

In terms of the Guidelines issued, the Desk considers the following complaints as ineligible:
a) A complaint which has been the subject of legal proceedings before a Court or Tribunal.
b) Where the complainant has not suffered any financial loss, material inconvenience or distress.
c) A complaint which would be more suitably dealt with by a Court or under other dispute resolution arrangement.
d) A complaint whose resolution would prejudice the rights of other parties who have not consented to the resolution by the Desk.
e) A complaint which is vexatious or frivolous or not in good faith.
f) A complaint which was not first reported to the banking institution concerned.
g) A complaint which is lodged more than 14 days after a banking institution has delivered its decision or failed to resolve the complaint.
h) A complaint which is beyond the pecuniary jurisdiction of the Desk.

**8. INFORMATION YOU MUST INCLUDE IN THE COMPLAINT (TAARIFA MUHIMU ZA KUJUMUISHA KWENYE LALAMIKO)**

a) Your name and address.
b) The name and address of the banking institution against which the complaint is made.
c) Details of what your complaint is about including exactly what the bank did that it shouldn't have done or what it didn't do that it should have done.
d) What you have lost in terms of personal injustice, financial loss, hardship or inconvenience.
e) What you would like the Desk to do to put things right and details of what you have done so far to try to resolve the complaint
f) Include documentary evidence, if any.

**9. WITHDRAWAL OF THE COMPLAINT (KUFUTA LALAMIKO)**

A complainant may, at any time before the Desk's determination, withdraw his complaint in writing from the Desk, and the matter shall be closed by the Desk.

**10. FREE SERVICE (HUDUMA ZA BURE)**

Resolution of banking consumers' complaints is free of charge as the Desk does not charge any fee whatsoever.

**11. MEDIUM OF COMMUNICATION (NJIA YA MAWASILIANO)**

The medium of communication is both English and Kiswahili.

**12. REMEDIES AWARDED (SULUHISHO LILILOPATIKANA)**

The function performed by the Desk is different from that performed by courts. The Desk is enjoined not to have regard to technicality and legal form but resolve complaints using criteria that would not usually be used by courts; for instance whether an explanation for the conduct was not given when it should have been given. A banking institution may be required to issue an apology, change its practices, effect payment or compensation as the case may be. The Desk is not bound by the legal principles of handling complaints such as rules of evidence but adheres to the general principles of natural justice.

When Aggrieved by Desk decision

Either party may request the Desk to reconsider any of its decision. Each party also has a right to seek redress before a competent court when it is not satisfied with the decision given by the Desk


**CANARA BANK (TANZANIA) LIMITED**
**VIWANGO VYA TOZO NA HUDUMA KUANZIA 01/07/ 2018**

| | TZS | USD |
|---|---|---|
| **A. AKAUNTI ZA AKIBA** | | |
| 1. Kufungua akaunti | 50,000 | 50 |
| 2. Ada ya huduma kila mwezi | Hakuna tozo | Hakuna tozo |
| 3. Akaunti kutokua na kima cha chini | Hakuna tozo | Hakuna tozo |
| 4. Tozo za taarifa ya akaunti | | |
| a) Mwezi | Hakuna tozo | Hakuna tozo |
| b) Kipindi fulani | 5,000.00 | $5 |
| 5. Tozo ya kutoa pesa kwenye akaunti | Hakuna tozo | Mpaka 5000 Hakuna tozo Above 5000 - 0.3% |
| 6. Tozo ya kuweka pesa kwenye akaunti | Hakuna tozo | Hakuna tozo |
| 7. Cheti cha kuhakiki salio | 15,000.00 | $7 |
| 8. Tozo ya kufunga akaunti | 15,000.00 | $15 |
| 9. Kufufua akaunti | 6,000.00 | $6 |
| **B. AKAUNTI ZA HUNDI** | | |
| 1. Kufungua akaunti | 100,000 | 100 |
| 2. Ada ya huduma kila mwezi | Hakuna tozo | Hakuna tozo |
| 3. Akaunti kutokua na kima cha chini | Hakuna tozo | Hakuna tozo |
| 4. Tozo za taarifa za akaunti a) Mwezi b) Mpito | 5000 5000+500 Kwa kila kurasa | $5 $ 5+1 kwa kila kurasa |
| 5. Tozo ya kutoa pesa kwenye akaunti | MPAKA 25 MIO-Hakuna tozo MPAKA 25 MIO--0.12% | Mpaka 5000 Hakuna tozo 5000 to 10,000 - 0.3% Zaidi 10,000 - 0.5% |
| 6. Tozo ya kuweka pesa kwenye akaunti | Zaidi 50 MIO- Hakuna tozo Zaidi 50 MIO--0.12% | Zaidi 10,000- Hakuna tozo > 10,000- 0.3% |
| 7. Cheti cha kuhakiki salio | 25,000.00 | $15 |
| 8. Agizo la kusimamisha malipo | 30,000.00 | $15 |
| 9. Hundi iliyokataliwa | | |
| a) Hundi ya ndani | 30,000.00 | $15 |
| b) Hundi ya nje | 30,000.00 | $20 |
| 10. Tozo kufunga Akaunti | 25,000.00 | $20 |
| **C. TOZO ZA MIAMALA YA SIMU** | | |
| 1. Kutoa pesa | | |
| Mpaka 100,000 | 2,000.00 | NA |
| 101,000 to 200,000 | 3,000.00 | NA |
| 201,000 to 400,000 | 5,000.00 | NA |
| 401,000 to 600,000 | 6,000.00 | NA |
| 601,000 to 999,000 | 8,000.00 | NA |
| 2. Kuhamisha fedha/Kuhamisha kwa njia ya mtandao wa simu | | |
| Mpaka 100,000 | 500.00 | NA |
| 101,000 to 250,000 | 1,000.00 | NA |
| 251,000 to 500,000 | 2,000.00 | NA |
| 501,000 to 1,000,000 | 5,000.00 | NA |
| 1,001,000 MPAKA 10,000,000 | 10,000.00 | NA |
| | | |
| **HUDUMA ZA KIBENKI** | | |
| A) Tozo za mwezi | 500.00 | NA |
| B) Kuomba namba ya siri | 2,500.00 | NA |
| **H. TOZO YA LOCKERS KWA MWAKA** | | |
| 1.NDOGO | 350,000.00 | |
| 2. SAIZI YA KATI | 600,000.00 | |
| 3. KUBWA | 750,000.00 | |

| **D. KUHAMISHA FEDHA BAINA YA BENKI** | TZS | USD |
|---|---|---|
| 1. TISS | 11,800.00 | $11.8 |
| 2. E Remittances | | |
| Mpaka USD 1,000 au Eq. TZS | 20,000.00 | $10 |
| 1001 mpaka 5000 | 24,000.00 | $12 |
| 5001 mpaka 10000 | 48,000.00 | $25 |
| 10,001 na zaidi | 100,000.00 | $50 |
| 3. SWIFT | | |
| a) Swift Outward | | |
| Mpaka 5,000 | NA | $45 |
| 5,001 mpaka 10,000 | NA | $60 |
| Zaidi 10,000 | NA | $90 |
| b) Swift Inward | | |
| Mpaka 5,000 | NA | $12 |
| 5,001 mpaka 10,000 | NA | $18 |
| Zaidi ya 10,000 | NA | $30 |
| **E. TOZO ZA MIKOPO** | | |
| 1. Ada ya kushughulikia mkopo | Mpaka 5 Mio - 25,000 5Mio mpaka 10 Mio - 200,000 10 Mio mpaka 25mio - 400,000 25 mio mpaka 500 mio - 1.5% >500mio--1.25%* *minimum 7.5mio | Mpaka 5,000 - $100 5000 to 10,000 - $200 Mpaka 20,000 - $300 20,000 to 500,000 - 1.5% >500,000--1.25%* *Kima cha chini 7,500 |
| 2. Nyaraka za mkopo | Mpaka 100 mio --NIL-- >100 Mio 0.3% -Min 300,000 | Mpaka 50,000 --NIL-- >50,000 - 0.3% Min 150 |
| 3. Mkopo wa muda-Malipo ya awali | Mpaka 5Mio - 25,000 5 Mio mpaka 10 Mio - 200,000 10Mio 25mio - 450,000 25 mn to 500 mio -1.8% >500mio--1.5%* *minimum 9mio | Mpaka 20,000 - $300 20,000 to 500,000 - 1.8% >500,000--1.5%* *kiwango cha chini 9000 |
| 4. Tozo ya ukaguzi | Mpaka 100 Mio -25,000 >100 mio - 50,000 | Mpaka 50,000 - 25 >50,000 ----50 |
| **F. LETTER OF CREDIT** | | |
| Import Letter of Credit (per qrtr of Part thereof) | | |
| Opening commission | NA | 1.2% ( Kiwango cha chini $ 200) |
| LC amendment Commission | NA | 0.4% ( Kiwango cha chini $50 Kiwango cha juu 350) |
| Swift charge for LC opening | NA | $40 |
| Swift charge for other message/amendments | NA | $40 |
| Extensions - Commissions | NA | 1.2% ( Kiwango cha chini $200) |
| LC cancellation charges | NA | 1.2% ( Kiwango cha chini $200) |
| Non payment of Bills on due date | NA | 16% Till Payment |
| **Export Letters of Credit (per quarter or part thereof)** | | |
| Advising commission | NA | $140 |
| Confirmation Commission | NA | 0.5% ( Kiwango cha chini $150) |
| Negotiating bills under LC | NA | 0.5%(Kiwango cha chini $75+cuourier+int) |
| Reimbursement claim paid | NA | 0.5% ( Kiwango cha chini $75) |
| Extensions - Commissions | NA | 1.2% ( Kiwango cha chini $200) |
| Collection of Export LC | NA | 0.5%(Kiwango cha chini $75+cuourier+int) |
| Amendments | NA | $75 |
| **G. Guarantees (Local & International)** | | |
| Bonds & Guarantees | 1.2% ( Kima cha chini TZS 75,000) | 1.20% |
| Bonds & Guarantees with 100 % Cash Margin | 0.5% kwa robo mwaka (Min TZS 75,000) | 40% gharama halisi |

**Banking Services offered BY Canara Bank (Tanzania) Ltd** **We offer following Services**

- Current and Saving Account
- Salary Account
- Student Account
- Fixed Deposit Account
- Re Investment Deposit Account
- Recurring Deposit Account
- Overdraft and Term Loans
- Vehicle Loan
- Mortgage Loan
- Personal Loan
- Insurance Premium Funding
- Safe Deposit Lockers
- All Export and Import Related transactions
- Letter of Credit and Guarantees
- E- Remit Facility to India
- Mobile Banking



Plot No 16/1, Elia Complex
Zanaki-Bibi Titi Street, P.O Box 491- Dar es Salaam, Tanzania
T: +255 222 112 2530 (D) +255 222 112 532
Email: cbtl@canarabank.co.tz

Access your A/c 24x7

215482002

## Bil. 1/- kwa wajasiriamali

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KATIKA kutatua changamoto ya ukosefu wa mitaji kwa vikundi vya wajasiriamali, Halmashauri ya Mji wa Kahama, imetoa kiasi cha Sh. bilioni 1.182 kwa vikundi vya wajasirimali vya wanawake, vijana na wenye ulemavu ili kuviwezesha vikundi hivyo kukua kiuchumi.

Mary Chima, mratibu wa mfuko wa wanawake, vijana na wenye ulemavu kutoka halmashauri hiyo, aliyasema hayo jana wakati akizungumza wa wanahabari, na kusema kuwa vikundi vya kinamama vimekuwa vikirejesha mikopo hiyo kwa wakati tofauti na vijana.

Alisema mwaka wa fedha 2018/19 halmashauri ilitenga na kutoa kiasi cha Sh. milioni 564.5 na kutoa mikopo kwa vikundi 158 vya wajasiriamali vijana, wanawake pamoja na walemavu.

Aidha, Chima alisema kuwa, vikundi 104 vya wanawake vilipata kiasi cha Sh. milioni 342.5, vikundi 47 vya vijana Sh. milioni 243 pamoja na vikundi saba vya wajasiriamali walemavu walipata kiasi cha Sh. milioni 15.

Pia alisema, mwaka wa fedha wa 2019/20 halmashauri imetenga kiasi cha Sh. milioni 618 na kutoa kiasi cha Sh. milioni 199 kwa vikundi vya wajasiriamali 68 kwa robo ya kwanza ya mwaka wa fedha huku vikundi vya kinamama 53 vilipata Sh. milioni 160 na vijana vikundi 15 vilipata Sh. milioni 39.

"Mikopo hii tunatoa kwa vijana, kinamama na walemavu wenye umri chini ya miaka 35, wapo wanaokosa mikopo hii kulingana na umri wao, lakini sisi tumekuwa tukiwaelekeza na kuwaunganisha katika kituo cha uwezeshaji wananchi kiuchumi ambao kituo hicho hakijali umri na kinatoa mikopo na ushauri kwa wajasiriamali wote," alisema Chima.

Hata hivyo Chima alisema, vikundi vya wanawake na walemavu vimekuwa vikirejesha mikopo hiyo kwa wakati na ukilinganisha na vikundi vya vijana na kwa vikundi vya vijana vilivyoshindwa kurejesha mikopo, vimekuwa vikichukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kuvifikisha mahakamani.

Alisema kuwa, wanashindwa kutoa mikopo hiyo kwa wachimbaji wadogo kutokana na shughuli zao za uchumbaji wa madini kuwa za kuhamahama na hii inaweza ikasababisha fedha za umma zikapotea na vikundi vingine vikashindwa kuendelea kupata mikopo hiyo.

Aidha Chima, aliwataka Maofisa Maendeleo ya Jamii walioko kila kata kutoa elimu ya namna ya matumizi sahihi ya fedha zinazotolewa na halmashauri kwenye vikundi kwa ngazi ya kata ili ziweze kutumika kwenye matumizi yaliyopangwa na sio kwenda kufanyia anasa.

# Watendaji wa serikali wapewa somo

**Na Mwandishi Wetu,**

WATENDAJI wa serikali Zanzibar wametakiwa kuacha tabia ya kupelekeshwa na viongozi wao kwa lengo la kuvunja maadili, badala yake wawashauri, ili wafanye kazi kwa kuzingatia sheria na kanuni za kazi.

Akizungumza na watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango wilayani Chakechake, Pemba Katibu wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Asma Hamid Jidawi, alisema ni vyema watendaji wa wizara kufanya kazi kwa kufuata maadili.

Alisema wana jukumu la kumshauri kiongozi wao iwapo ana lengo la kukiuka maadili, ili kuepusha matatizo yanayoweza kujitokeza. "Sio kila kitu unachoambiwa ufuate tu, iwapo umeshajua kitu hicho ni kinyume cha maadili ya kazi, basi mshauri kiongozi wako huenda amepitiwa, la sihivyo ipo siku utajikuta unaingia kwenye matatizo," alisema.

Aliwataka watendaji hao pia kuwa makini na inapotokezea kiongozi ameenda kinyume cha maadili azungumze nae kwa utaratibu, ili aweze kufahamu.

Alieleza ubadhirifu unarejesha nyuma maendeleo ya nchi, hivyo ni vyema wafanyakazi wote wakafuata maadili, ili kuwa na Taifa lililo imara zaidi.

Aidha, Jidawi aliiomba jamii kuwalea watoto wao katika maadili mema, ili wawe viongozi bora wa Taifa la baadaye.

Ofisa wa Sheria kutoka Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Unguja, Makame Mussa Mwadini, alisema, kutumia mali ya serikali kwa matumizi binafsi ni kuvunja maadili, hivyo ni vyema kufanyakazi kwa mujibu wa sheria na dini yako inayokuongoza.

"Kuna viongozi hutumia mali ya serikali kwa kujinufaisha yeye binafsi, hili ni kosa kwani amekiuka maadili, hivyo watumie vizuri vyeo vyao kwani ni dhamana kwao," alisema.

Aliwaomba wananchi kushirikiana na kuendelea kutoa taarifa kwa Tume ya Maadili pale inapotokezea kiongozi wa umma amevunja maadili.

"Dira yetu ni kupata jamii yenye maadili na hapo ndipo tutaisaidia serikali katika kuleta maendeleo endelevu katika nchi yetu," alieleza.

"Tunaomba pia viongozi waitwe na wapewe elimu hii ya maadili, kwani kuna baadhi yao hulazimisha kitu kinyume na maadili na hawataki hata kuandika, jambo ambalo linawasikitisha sana," alieleza.

Ofisa Mapato kutoka Wizara hiyo, Mohamed Bakar Mohamed, alisema watu wa chini ndio wanaoathirika zaidi na ukiukwaji wa maadili, jambo ambalo linawakaza katika utendaji wa kazi zao za kila siku.



Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Fedha wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Jerry Sabi, akizungumza namna mfumo wa kanzidata za mkopo kwa wakopaji na wakopeshaji unavyosaidia kukuza sekta ya fedha na uchumi nchini baada ya kuuzindua jijini Dar es Salaam kwa kushirikiana na Kampuni ya Dun & Bradstreet Credit Bureau Tanzania Ltd. **MPIGAPICHA WETU**

# Agizo la waziri umeme kwa shule latekelezwa

**Na Futuna Seleman,** KISARAWE

TAKRIBANI miezi mitatu iliyopita, baada ya Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, alipoitembelea Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Christon wilayani Kisarawe mkoani Pwani na kuagiza Shirika la Umeme (Tanesco) kuiunganisha na gridi ya Taifa, utekelezaji wa agizo hilo umeanza.

Jana wafanyakazi wa Tanesco walifikisha nguzo za umeme katika eneo lililopimwa kwa ajili hiyo.

Upelekaji wa nguzo hizo uliibua shangwe na furaha kutoka kwa wanafunzi, wafanyakazi na wakazi wa eneo linalozunguka shule hiyo. Ofisa wa Tanesco, ambaye hakutaja jina lake, alisema kutokana na mchango wa shule hiyo katika kuinua taaluma mkoani Pwani, shirika limeona ni wakati mzuri kutekeleza agizo la Naibu Waziri.

"Itakumbukwa kwamba wakati Naibu Waziri alipotembelea shule hii alitoa maagizo ya kuiunganisha na gridi ya taifa. Tumeleta nguzo hizi ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa maagizo hayo na muda sio mrefu... tutaanza zoezi la kuunganisha nyaya kwa wateja wetu," alisema ofisa huyo.

Shule hiyo imekuwa ikitumia gharama kubwa katika kununua mafuta ya kuendesha majenereta na kukosa umeme wa uhakika kwa sababu haikuunganishwa na gridi ya Taifa.

"Moja ya kero ambayo Naibu Waziri alielezwa na uongozi wa shule alipofanya ziara shuleni hapo ni kukosekana kwa umeme wa uhakika.

"Tanesco tumesikia na muda sio mrefu wataiunganisha na gridi ya taifa," aliahidi.

Hata hivyo, Mkuu wa shule hiyo, August Minja, hakuwapo kuzungumzia hatua hiyo.

Mkazi wa eneo hilo, Idd Shabani, alifurahishwa na tukio hilo na kueleza kuwa katika uongozi wa Rais John Magufuli, familia maskini na tajiri zina fursa sawa ya kupata umeme.

"Tunamshukuru Naibu Waziri kwa agizo la kuunganisha Shule ya Christon na gridi ya Taifa. Umeme hautasaidia shule tu bali hata sisi wakazi wa eneo la karibu na shule hii... Kupata umeme ilikuwa ni ndoto isiyotekelezeka kwa siku za nyuma," alisema Shabani.

Aliongeza kuwa pia kuwa kuwapo kwa umeme katika eneo hilo kutawavutia wawekezaji wa kujenga viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo, kuibua na kukuza shughuli za kibiashara.

# Wapewa mbinu kuepuka mafataki

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

WANAFUNZI wa kike wa Shule ya Sekondari Qash Halmashauri ya Babati mkoani Manyara, wamepewa mbinu za kukwepa mafataki wanaowarubuni na kuwafanya wakatishe ndoto zao.

Mbinu hizo zikitolewa juzi na Mjumbe wa Baraza Kuu la Jumuiya ya Wanawake wa CC (UWT) na mjumbe wa kamati ya elimu, afya, malezi na mafunzo, Magreth Maina, wakati akizungumza na wasichana wa shule hiyo alipowatembelea.

Maina aliwashauri kuepuka tamaa na vishawishi wanavyopatiwa na mafataki ili watimize ndoto zao za kuwa wabunge, madaktari, walimu na wakurugenzi.

"Ukikutana na kijana au mwanaume akakulubuni kwa fedha ukakubali mwishowe atakuingiza mkenge mtafanya ngono na utabeba mimba na shule ndio mwisho wake hivyo wakatalieni," alisema Maina na kuongeza:

"Ukitaka kuwa na nafasi nzuri ya cheo ni lazima uwe mvumilivu, hivyo vumilieni msibebe mimba za utotoni maana zitaharibu malengo yako," aliongeza.

Aidha, aliwataka kujiamini katika masomo yao na kutokubali pale wanapokutana na wanaowarubuni.

Maina aliambatana na wajumbe wa kamati ya utekelezaji ya Wilaya ya Babati ikiwa sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya UWT pamoja na kugawa pedi kwa wanafunzi hao.

Naye mwalimu mlezi, Hosana Kitumu, alisema tangu Januari hadi Oktoba mwaka huu, wanafunzi waliobeba mimba ni wanne.

"Wanafunzi hawa wengi wao wamepewa mimba na waendesha bodaboda na wafanyabiashara wa mazao wanaokuja vijijini," alisema.

Nasima Abdallah, mwanafunzi wa kidato cha pili, alisema kutokana na umbali mrefu wanafunzi wengi wanashawishiwa kwa kupewa lifti na bodaboda hatimaye wanapachikwa mimba za utotoni.

Mjumbe kutoka Mkoa wa Manyara, Mansueta Sanka, aliwataka wanawake kuzungumza na watoto wao wa kike na kuwa karibu nao ili kukwepa vishawishi.

# Mgogoro wa mipaka mbioni kupata suluhu

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SERIKALI imesema ipo katika hatua za mwisho kukamilisha ufumbuzi wa kudumu wa mgogoro wa kugombea mipaka kati ya wananchi wa kitongoji cha Momela Wilaya ya Arumeru na Hifadhi ya Taifa ya Arusha (Anapa) uliodumu kwa miaka 30 na kuathiri shughuli za kiuchumi.

Akizungumza na wananchi wa kitongoji hicho jana, katika mkutano wa hadhara, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, alisema ufumbuzi wa mgogoro huo utaenda sambamba na utatuzi wa migogoro mingine katika vijiji 1,000 nchini vyenye migogoro ya aina hiyo.

Hata hivyo, Kanyasu alisema amesikitishwa na taarifa ya wananchi waliodai kwamba mahusiano yao mabaya na hifadhi ya Anapa yamesababisha mifugo yao kuuawa ovyo kwa kupigwa risasi na askari wa hifadhi hiyo, huku baadhi ya wananchi wakibambikiwa kesi za jinai.

"Namwelekeza mhifadhi wa Anapa hana mamlaka ya kupiga wananchi na kama bado ataendelea kupiga inamaana anavunja sheria na likiendelea kufanyika maana yake mhifadhi hatoshi," alisema Kanyasu.

Kanyasu aliwataka wananchi hao kuwa wavumilivu kwani yeye kama mteule wa Rais hatakubali kuona wananchi wakinyanyaswa au kuuawa mifugo yao na mazao yao kuharibiwa bila fidia na kuutaka uongozi wa hifadhi hiyo kurejesha mfuko wa ujirani mwema ili kufidia wananchi wanaopoteza mifugo ama kuharibiwa kwa mazao yao.

Awali wakizungumza kwa niaba ya wenzao, Mwenyekiti wa Kitongoji hicho, Sanyaeli Nko, Anna Nasary na Elizabeth Nko licha ya kumpongeza Kanyasu kwa kufika katika kitongoji chao, walieleza jinsi mgogoro huo jinsi ulivyoathiri maisha yao na kudumaza maendeleo ya kitongoji chao.

Mbunge wa Arumeru Mashariki, John Palangyo, alisema amekuwa akifanya jitihada mbalimbali katika kupata utatuzi wa mgogoro huo, hivyo anashukuru kuona Kanyasu akifika katika kitongoji hicho ili kushughulikia suala hilo ambalo limekuwa kero.

Naye Naibu Mhifadhi wa Anapa, Albert Mziray, alikanusha kuwapo kwa mgogoro na kudai kuwa mahusiano yao na wananchi hao ni mazuri.

Awali Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, aliwahakikishia wananchi hao kutoonewa na mtu yeyote katika uongozi wake na kuwataka watumie mawasiliano yake kumjulisha changamoto zinazowakumba, huku akiwasisitiza kuwa wavumilivu na kufuata sheria wanapoishi karibu na hifadhi hiyo wakati serikali inashughulikia mgogoro huo.

# DC ataja sifa wagombea wa kuchaguliwa S/Mitaa

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, amewataka wananchi kuchagua viongozi wenye hofu ya Mungu ambao watakuwa tayari kushughulikia changamoto zao, badala ya kujali maslahi yao binafsi. Aliyasema hayo jana wakati akizungumza katika ibada ya maombi maalumu ya kuombea Taifa yaliyofanyika katika Kanisa la Pentekoste eneo la Ngulelo.

Muro alisema katika kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa ni jukumu la kila mwananchi kujitokeza kwenda kuchagua viongozi wanaowafaa ambao watakuwa tayari kuleta maendeleo katika maeneo yao sambamba na kuwatatulia kero zao.

"Nimefurahi sana kuona kanisa linatambua wajibu wake wa kuombea Taifa sambamba na kumshukuru Mungu kwa mambo mbalimbali ya maendeleo yanayofanyika kupitia Rais John Magufuli...huu ni mfano wa kuigwa kwani mnapoombea nchi pamoja na viongozi wake inasaidia sana kuzidi kudumisha amani na upendo," alisema Muro.

Mtumishi wa kanisa hilo, Mwalimu Onesmo Anaeli, alisema ni mara ya kwanza kufanya maombi ya kuombea Taifa, na kuwa utakuwa ni mwendelezo. Anaeli alisema kama kanisa litatambua wajibu wake na kusimama katika nafasi yake na kuiombea nchi, kunatoa nafasi kubwa ya Taifa kuendelea kufanikiwa.

"Kwa kweli sisi kama kanisa, tuna kila sababu ya kumshukuru Mungu kwa ajili ya kutupa Rais ambaye ni kimbilio la watu, huku akimfanya kila kiongozi kusimama katika nafasi yake akitenda haki bila kuwapo ubaguzi," alisema.

Mwalimu Onesmo aliongeza suala la kuombea Taifa sio la kisiasa wala la kichama bali kila mmoja katika nafasi yake kutokana na kuwa na wajibu wa kufanya hivyo.

Askofu wa Kanisa la Pentekoste Arusha, Dk. Askofu Steven Melisheki, alisema kanisa hilo limeamua kufanya maombi hayo ili Taifa kuendelea kuwa na amani.

Askofu Melisheki alisema wamekusanyika kuliombea Taifa ili liendelee kuwa na amani ambayo itawasaidia viongozi na wananchi kutekeleza majukumu yao ya kila siku na kuiletea nchi maendeleo tarajiwa kwani jukumu la kuliombea Taifa sio la mtu mmoja, chama cha siasa bali ni la kila mwananchi mwenye kulitakia mema.








# Wanawake 4,000 kuibua ukatili kijinsia

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

ZAIDI ya wanawake 4,000 wa Mkoa wa Kilimanjaro, wanaandaliwa kutumika kama askari kanzu wa kuchimba na kuibua matukio ya ukatili wa kijinsia yanayotishia ustawi wa jamii katika halmashauri saba za mkoa huo kwa sasa.

Katika Manispaa ya Moshi peke yake, hali ni mbaya zaidi kwa kuwa ripoti inaonyesha kuanzia Januari hadi Septemba mwaka huu, watoto 157 wameripotiwa kufanyiwa ukatili wa aina mbalimbali na 52 kati ya hao, wamefanyiwa ukatili wa kingono, sawa na asilimia 33.

Akizungumza na Nipashe jana katika mahojiano maalum kuhusu utekelezaji wa mpango huo, Mratibu wa Mradi Ujenzi wa nguvu ya pamoja ya kutetea wanawake na watoto wa mkoa wa Kilimanjaro, Veronica Ollomi, alisema lengo hasa ni kuwaelimisha kwanza kutambua ukatili wa kijinsia upo lakini pia ni mikakati gani na mbinu gani wanayoweza kutumia ili kupambana na matukio hayo.

"Hivi sasa tunatoa elimu ya jinsi ya kuendelea kuwakagua watoto wetu, watoe taarifa kama kuna matukio ya ukatili, lakini wachukue hatua ya kuielimisha jamii jinsi ya kukabiliana na matatizo haya. Hawa watakuwa ni wawakilishi wa wanawake wengine, kwa sababu hao wanatoka kwenye makundi mbalimbali ya ujasiriamali, majukwaa ya wanawake katika kila wilaya, vyama vya watu wenye ulemavu na wanawake mashuhuri ambao watatumika kuwaelimisha wanawake wengine kwenye ngazi ya chini zaidi," alisema Ollomi.

Shirika hilo la Kwieco limeshawanoa wawakilishi wa wanawake ngazi ya mkoa, na sasa limeshuka hadi ngazi ya wilaya na kuwafikia wanawake mashuhuri 15 kutoka kata tano za Shirimatunda, Pasua, Njoro, Kiborloni na Bomambuzi.

Mradi huo wa majaribio wa mwaka mmoja, unatekelezwa na Shirika lisilo la kiserikali la Kwieco, kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania (WFT).

Zaidi Ollomi alieleza: "Hizo timu tulizokutana nazo, wao ndio watatusaidia kufika kwenye jamii zaidi kuibua vitendo hivi, kwa sababu mara nyingi vinafanyika kwa siri, kwa hiyo ni lazima kuwe na watu ambao wataviibua ili viweze kujulikana kwamba vipo vinafanyika na hatua gani ziwe kuchukuliwa."

Kiongozi wa wanawake mashuhuri waliojitoa kupambana na ukatili wa kijinsia katika Manispaa ya Moshi, Rubelina Meena, alisema kupaa kwa takwimu za ukatili wa kijinsia kunatokana na baadhi ya familia kumalizana kimyakimya kwa kuombana msamaha kwa kutumia majani ya masale, badala ya kuripotiwa kwenye vyombo vya kisheria.

Mama mashuri Maryline Lugano alipouliza ili kudhibiti kasi ya matukio hayo kufanyike nini alisema: "Kutokana na hali ya matukio ya ukatili wa kijinsia katika mkoa wa Kilimanjaro ilivyo kwa sasa, kupitia mradi huu, kwanza tunataka kuwa na ile sauti ya pamoja katika mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia, kwa kweli yamezidi kuongezeka yamekuwa mengi, lakini hatujaweza kuwa na ule msukumo au nguvu ya pamoja kuweza kupambana nao."

Pia Halima Said akizungumzia mkakati huo, alisema wanajua Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (Mtakuwwa) upo lakini kwa kuwa serikali haiwezi peke yake, ndiyo maana Kwieco wamewaita kinamama kutoka ngazi ya mkoa na wilaya kupata elimu na kisha kwenda kuibua na kutoa taarifa za ukatili kwenye jamii wanamoishi.



Mratibu kutoka Taasisi ya Sanku, Jane Maloo, akimwonyesha Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu (katikati) mashine maalumu inayotumia mfumo wa laini ya simu katika utendaji wake wa kuchanganya unga na virutubisho kwenye maadhimisho ya Siku ya Mtoto Mwenye Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi yaliyofanyika kitaifa kwenye viwanja vya Tangamano jijini Tanga mwishoni mwa wiki. **PICHA BONFACE GIDEON**

## Moshi yakwepa mtego wa Jafo

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Moshi, imejiandaa kuukwepa mtego wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, baada ya Mkurugenzi Mtendaji wa wilaya hiyo, Kastori Msigalla, kutangaza rasmi watahama Novemba 5, mwaka huu.

Oktoba 7 mwaka huu, Jafo alitangaza kuwa halmashauri 31 ikiwamo Moshi ambazo zina ofisi nje ya maeneo yao ya utawala kama hazitahama maeneo hayo katika kipindi cha siku 30, zitafutwa.

Kutokana na agizo hilo, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi imetangaza kuwa itahamia katika majengo ya iliyokuwa Shule ya Sekondari Kolila Jumanne ya wiki ijayo.

Taarifa iliyowekwa katika tovuti ya halmashauri hiyo, inaeleza kuwa Msigalla aliweka wazi mpango huo wakati wa Kikao cha Menejimenti ya Halmashauri hiyo (CMT) kilichoketi siku tano zilizopita.

Mkurugenzi huyo amenukuliwa akisema: "Wakuu wote wa idara muwaandae watu wenu kwa hili, tutahama tarehe 5 mwezi wa 11 kuelekea Kolila katika Kijiji cha Kikarara. Tunatarajia kwamba ofisi yetu kuu ya wilaya itahamia Kata ya Old Moshi Mashariki, kwenye majengo ya iliyowahi kuwa Shule ya Sekondari Kolila, hakuna mjadala ni kuhama tu."

Wakati Msigalla anatangaza msimamo huo, kulikuwa na mpango wa chini kwa chini wa wanasiasa wachache waliokuwa wakitengeneza visingizio na chokochoko za kutaka wananchi wapinge ofisi za halmashauri hiyo zisihamie katika majengo ya iliyokuwa Shule ya Sekondari Kolila.

Wanasisasa hao walikuwa wakitengeneza vikwazo kwamba eneo hilo ni mbali kwenda kutafuta huduma.

Shule ya Sekondari Kolila ambayo awali, ilikuwa ikimilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini, ilifungwa zaidi ya miaka 10 iliyopita kutokana na kushindwa kujiendesha.

# Malalamiko vifaa hati za umiliki ardhi yatua wizarani

**Na Godfrey Mushi,** HAI

TATIZO la kukosekana kwa vifaa vya kutayarishia hati za umiliki wa ardhi katika baadhi ya wilaya za mkoa wa Kilimanjaro, limetua Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, baada ya Ofisa Ardhi wa Wilaya ya Hai, Jacob Mhumba kuwasilisha rasmi suala hilo akitaka serikali iliangalie kwa jicho la kipee.

Muhumba aliwasilisha kilio hicho cha idara nyingi za ardhi, kwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, wakati akihitimisha ziara yake katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini mwishoni mwa wiki.

Katika taarifa yake aliyoikabidhi kwa Naibu Waziri Mabula, ofisa huyo ameeleza kuwa vifaa vinavyokwamisha mpango wa serikali wa kutoa hati hizo ni ukosefu wa karatasi za kutayarisha hati (deed plans).

"Ofisi ya Kamishna wa Ardhi wa Kanda ya Kaskazini imekuwa ikitoa vifaa muhimu kama crested papers (karatasi za hati), cover za hati (jalada) na wakati mwingine karatasi za matumizi ya kawaida na wino. Hata hivyo, ofisi zetu hazipati vifaa vingine kama karatasi za deed plans. Hii inatokana na ukweli kwamba ada zote za hati na zile za ramani za hati zinakwenda wizarani.

"Hali hii wakati mwingine inakwamisha na kuchelewesha utayarishaji hati miliki kwa kasi na kwa wakati."

Malalamiko mengine yaliyowasilishwa wizarani ni kutowasiliana kwa mfumo wa kielektroniki wa kukusanya mapato (GePG) na mfumo wa taarifa za ulipaji kodi za ardhi (LRMS).

Alisema mara kadhaa wamekutana na changamoto ya kutoa bili za viwanja kwa mfumo LRMS na namba husika za malipo kukataliwa benki, kuwa hazitambuliwi au kutajwa siyo sahihi.


Au wakati mwingine, malipo kufanyika kupitia mfumo wa GePG na deni husika lisifutike katika mfumo wa LRMS.

"Ni vyema wataalamu wetu wakaliangalia hili ili kuepuka kuwa madeni hewa mengi katika mfumo wa LRMS," imeeleza zaidi taarifa hiyo.

Kwa mwaka wa fedha 2018/19, Idara ya Ardhi ya Wilaya ya Hai ilipangiwa kukusanya kiasi cha Sh. milioni 250 na kufikia Juni 30 mwaka huu, ilikuwa imevuka lengo kwa kukusanya Sh. milioni 407 sawa na asilimia 162.

Kwa mwaka mpya wa fedha 2019/20, imepangiwa kukusanya Sh. milioni 900 na hadi kufikia Oktoba 18 mwaka huu, idara hiyo ilikuwa imefanikiwa tayari kukusanya Sh. milioni 132.166.

# Nipashe Spotika



WAMEANZA NA REKODI UEFA MSIMU 2019-20 UK. 20





## ISIKUPITE

MSHAMBULIAJI wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe amekuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kufunga mabao 15 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, akiwa na umri wa miaka 20 na siku 306 akiivunja rekodi ya Lionel Messi, ambayo aliiweka akiwa na umri wa miaka 21 na siku 288.

## CHAKARIKA...

Mshambuliaji wa Manchester City, Raheem Sterling 'akichakarika' kumiliki mpira dhidi ya beki wa kulia wa Aston Villa, Frederic Guilbert wakati wa mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Eithad juzi na City kushinda 3-0. **HABARI UK. 28**




# WATANO WANAOPASWA KUTUA UNITED

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imeanza kwa kusuasua msimu wao wakiwa wamejikusanyia pointi 10 tu katika mechi tisa.

'Mashetani Wekundu' hao walikuwa kwenye nafasi ya kuondoka na pointi tatu kwenye mchezo wao dhidi ya vinara, Liverpool kabla ya Adam Lallana kusawazisha bao la Marcus Rashford alilofunga kipindi cha kwanza. Bila kujali matokeo hayo na wapinzani wao wakuu wa Ligi Kuu ya England, Man United haijawa kwenye kiwango chake msimu huu hadi sasa.

**Kocha, Ole Gunnar Solskjaer amekuwa akishutumiwa mno kutokana na kiwango kibovu cha kikosi hicho hadi sasa. Lawama kubwa imemwangukia kocha huyo kutokana na ukweli kwamba, kikosi hicho hakipo kabisa kwenye ubora wake.**

Wakati dirisha la usajili la Januari kipindi cha majira ya baridi likikaribia, hapa tunawaangalia wachezaji watano ambao wanaweza kumsaidia Solskjaer kumaliza tatizo lake kama akiwasajili...

### 5. ALEJANDRO GRIMALDO (SL BENFICA)

Alejandro Grimaldo ni mmoja wa walinzi bora zaidi kwenye Ligi Kuu ya Ureno. Nyota huyo wa kimataifa wa Hispania alikuwa chaguo la Pep Guardiola ambaye anamkosa Benjamin Mendy aliyepo chumba cha majeruhi, lakini usajili wake ulishindikana.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, alilelewa pale kwenye kituo cha kuibua vipaji cha La Masia na aliichezea Barcelona B kati ya mwaka 2011 na 2015. Kipindi cha miaka yake minne alicheza mechi 92 na kufunga mabao sita.

Beki huyo wa kushoto alimaliza mkataba wake pale Nou Camp na Benfica wakamsajili Januari 2015 kwa euro milioni 1.5 na kumpa mkataba wa miaka mitano na nusu.

Wakati huu Luke Shaw akiwa majeruhi, huku mkataba wa Ashley Young ukikaribia kumalizika mwisho mwa kipindi cha majira ya joto kijacho, Grimaldo anaweza kuwa msaada mkubwa kwa kikosi cha Mashetani Wekundu hao.

### 4. JULIAN WEIGL (BORUSSIA DORTMUND)

Julian Weigl alisaini mkataba wa miaka mitano pale Borussia Dortmund mwaka 2016 na bado hajaongeza. Kama ilivyo kwa Grimaldo, mkataba wa Mjerumani huyo unamalizika ndani ya miaka miwili na ana nafasi ya kujiunga na timu nyingine.

Mazungumzo ya mkataba mpya bado hayajafanyika, hivyo ana nafasi ya kuangalia upande mwingine. Weigl akiwa ndo kwanza ana umri wa miaka 24, ana nafasi kubwa ya kuondoka Borussia Dortmund na kutafuta sehemu nyingine.

Manchester United kwa sasa wana Scott McTominay, Nemanja Matic na Fred katika safu ya ulinzi. Hata hivyo, Julian Weigl anaweza kuwa msaada mkubwa kwao.

### 3. MOUSSA DEMBELE (OLYMPIQUE LYON)

Wakati Ole Gunnar Solskjaer alipoteuliwa kuwa kocha wa muda pale Manchester United, Mashetani Wekundu hao walikuwa na wastani wa kufunga mabao zaidi ya mawili katika kila mchezo.

Kocha huyo raia wa Norway kwa sasa amekuwa akishutumiwa kwamba, safu yake ya ushambuliaji imekuwa butu, lakini mshambuliaji wa Lyon, Moussa Dembele anaweza kumaliza tatizo hili.

Msimu wake wa kwanza pale Lyon, mshambuliaji huyo amefunga mabao 20 katika mechi zake 46. Na sasa ana mabao sita katika mechi zake 10 alizocheza msimu huu na kama United watamsajili anaweza kuwa suluhisho nzuri kwao.

### 2. BRUNO FERNANDES (SPORTING LISBON)

Bruno Fernandes alikuwa akihusishwa zaidi na uwezekano wa kuhamia Manchester United kipindi cha majira ya joto, lakini mpango huo ulikwama. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno ana thamani ya euro milioni 70.

Kiungo huyo ana uwezo mkubwa zaidi dimbani kwa kukaba na kusukumiza mashambulizi mbele. Fernandes amechangia mabao 63 katika mechi 69 alizoichezea klabu hiyo ya Ureno na klabu kadhaa Ulaya zimekuwa zikiwania saini yake. Ukiacha Manchester United, klabu za Tottenham Hotspur, Inter Milan, na Real Madrid zimekuwa zikiwania saini yake anaweza kuwa mbadala wa Paul Pogba ambaye haypo katika kiwango chake...

### 1. FLORIAN THAUVIN (MARSEILLE)

Florian Thauvin amekuwa mmoja wa wachezaji wanaofanya vizuri zaidi kweye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, tangu alipojiunga na Klabu ya Marseille Januari mwaka 2016. Mfaransa huyo amekuwa nguzo kubwa ya upachikaji wa mabao kwa klabu hiyo.

Winga huyo wa kushoto alitokea kule Newcastle United akiwa kijana na kama Manchester United wakimpata anaweza kuwa msaada mkubwa zaidi kwao.

**JE, WAJUA?**



FERNANDINHO juzi aliichezea Manchester City mechi ya 200 Ligi Kuu England, hivyo kuwa Mbrazil wa tatu kutimiza idadi hiyo baada ya mshambuliaji wa Chelsea, Willian (206) na mchezaji wa zamani wa Liverpool, Lucas Leiva (247).

## MICHEZO



Kikosi cha Kagera Sugar, wakali wa ugenini. PICHA: MAKTABA

# REKODI ZA KUSHANGAZA LIGI KUU TANZANIA BARA

Na Adam Fungamwango

LIGI Kuu Tanzania Bara inazidi kuchanja mbuga na sasa imeingia raundi ya nane.

Timu 20 zinaendelea kumenyana kutafuta ufalme wa soka Tanzania, ambao kwa sasa unamilikiwa na Simba kwa misimu miwili mfululizo.

**Mpaka sasa timu zimeendelea kuweka rekodi mbalimbali, nzuri, mbaya, za kufurahisha na kushangaza kwa ujumla.**

Mwandishi wa makala haya amekusanya takwimu na rekodi mbalimbali ambazo tayari zimewekwa na timu zinazoshiriki Ligi Kuu mpaka sasa...

**1. SIMBA YAONGOZA KUSHINDA MFULULIZO**

Mabingwa watetezi, Simba ndiyo timu iliyoweka rekodi ya kushinda mechi nyingi mfululizo mpaka sasa. Ukiondoa mechi yake ya jana dhidi ya Singida United, Simba ilishinda mechi tano mfululizo, na hakuna timu yoyote mpaka sasa iliyofanya hivyo.

Ilianza kwa kuifinyanga JKT Tanzania mabao 3-1, ikaichapa Mtibwa Sugar 2-1, kabla ya kuitandika Kagera Sugar 3-0. Baada ya hapo ikaenda Mara na kuichapa Biashara United mabao 2-0, kabla ya kuiadhibu Azam kwa bao 1-0.

Kabla ya mechi dhidi ya Singida United, Simba ndiyo timu pekee ambayo ilikuwa haijapoteza mechi wala kutoka sare.

**2. AZAM, KAGERA ZATIBULIWA NA SIMBA**

Huenda timu za Azam FC na Kagera Sugar zingeweka rekodi ya kushinda mara nne mfululizo kama zisingekutana na Simba. Timu hizo zinafuatia kwa kuweza kushinda mechi zao tatu mfululizo za kwanza kabla ya kupata dhahama kwenye mechi zilizofuata dhidi ya Simba iliyotibua rekodi nzuri za timu hizo kushinda mfululizo.

Kagera Sugar baada ya kuanza vema Ligi Kuu kwa kuichapa Biashara United mabao 2-0, ikaifumua Alliance 2-1 na kushinda bao 1-0 dhidi ya Mbao FC, ilijikuta kwenye mdomo wa Simba na kuchapwa mabao 3-0 kwenye mechi yake ya nne na kufuta rekodi ya kushinda mechi ya nne.

Azam FC, iliifumua KMC bao 1-0, ikaishindilia Ndanda mabao 2-0 na kushinda 2-1 dhidi ya Namungo FC, lakini ilikumbana na kigingi cha Simba na kuchapwa bao 1-0 Jumatano iliyopita na rekodi yao kuishia hapo.

**3. MWADUI, MBEYA CITY WATAALAMU WA SARE**

Mwadui FC na Mbeya City ndizo timu zilizoweka rekodi ya kutoka sare mara nne mfululizo Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.

Baada ya kushinda bao 1-0 dhidi ya Singida United, Mwadui ikaanza mwendo wa sare kwa kutoka sare ya bila kufungana dhidi ya Ndanda, sare nyingine kama hiyo dhidi ya Namungo FC, ikatoka tena sare ya bao 1-1 dhidi ya Alliance, kabla ya nyingine ya 1-1 dhidi ya Mbao FC na rekodi ya sare iliishia hapo kwani mechi iliyofuata ikafungwa mabao 2-1 dhidi ya Coastal Union.

Mbeya City ilianza ligi kwa kutoka sare ya bila kufungana dhidi ya Prisons, ikatoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Ruvu Shooting na mechi iliyofuata ikatoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Lipuli na sare nyingine ya bao 1-1 dhidi ya Mtibwa, rekodi ikaishia hapo kwani mechi yake ya tano ilibamizwa mabao 2-0 dhidi ya Biashara United.

**4. HAKUNA TIMU ILIYOPOTEZA TATU MFULULIZO**

Katika kile kinachoonyesha kuwa Ligi Kuu msimu huu si lelemama, hakuna timu yoyote iliyopoteza mechi tatu mfululizo kabla ya mechi za jana.

Mechi pekee inayoweza kutibua rekodi hii ni kati ya Mwadui ambayo ilikuwa nyumbani jana dhidi ya JKT Tanzania na itakuwa hivyo kama Mwadui ilipoteza.

Ni kwa sababu Mwadui ilifungwa mabao 2-1 dhidi ya Coastal Union na pia bao 1-0 dhidi ya Polisi Tanzania, lakini matokeo ya mechi zote zilizobaki haziwezi kuathiri rekodi hii.

**5. NAMUNGO FC WAKALI KWAO TU**

Timu ya Namungo FC inaongoza kwa kuchukua pointi nyingi ikicheza nyumbani kwao kuliko timu yoyote ile. Imevuna pointi 13 ikicheza Uwanja wa Majaliwa mjini Lindi, ikicheza huko mechi tano, ikishinda nne na kutoa sare moja.

Kabla ya mechi yake ya jana ugenini dhidi ya Biashara United, Namungo ilikuwa haijavuna pointi yoyote ikicheza ugenini, ikiwa imecheza mechi mbili na kuchapwa zote.

Hakuna timu yoyote iliyoshinda jana nyumbani inayoweza kuzifikia pointi za Namungo nyumbani.

**6. KAGERA MTEMI UGENINI, NYUMBANI NYANYA**

Kagera Sugar ndiyo timu yenye rekodi ya kushangaza kidogo kwani ndiyo inayoongoza kwa kuzoa pointi nyingi ugenini kuliko timu zote. Lakini haijaambulia pointi hata moja nyumbani.

Timu hiyo imecheza mechi tano ugenini na kushinda nne, ikitoa sare moja, hivyo kujinyakulia pointi 13. Imecheza mechi mbili nyumbani, lakini zote ikichapwa. Mechi moja ikiambulia kipigo cha mabao 3-0 dhidi ya Simba na nyingine ikichapwa bao 1-0 dhidi ya JKT Tanzania Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

**NJE YA UWANJA**

Robert Lewandowski amekuwa mchezaji wa kwanza Ligi Kuu ya Bundesliga kufunga mechi zote tisa za mwanzo wa msimu baada ya juzi kuifungia Bayern Munich wakati ikishinda 2-1 dhidi ya Union Berlin, hilo likiwa bao lake la 19 katika mechi 14 alizocheza kwenye mashindano yote msimu huu, hivyo kuvunja rekodi ya kufunga mechi nane za mwanzo iliyowekwa msimu wa 2015-16 na mshambuliaji wa zamani wa Dortmund (kwa sasa Arsenal), Pierre-Emerick Aubameyang.



## Extra Time

# VIGOGO EPL 2019/20 MSIMU WA KISULISULI?



**LONDON,** England

KLABU nne kati ya sita kubwa katika Ligi Kuu ya England, Arsenal, Chelsea, Manchester United na Tottenham - zimeonyesha ishara ya kudorora kama si kuelekea kusombwa na upepo wa kisulisuli hadi kufikia sasa msimu huu.

**Huku klabu hizo nne zikivuna jumla ya pointi 49 katika mechi zake nane za kwanza, ikiwa ni pointi chache zaidi tangu kampeni ya kwanza ya ligi hiyo mwaka 1992 na chache zaidi katika misimu ya hivi karibuni.**

Makala haya yanaangalia matatizo wanayokumbana nayo...

### MANCHESTER UNITED

Baada ya kujishindia pointi nane kutoka mechi zake nane za kwanza ikiwa ndio idadi ndogo zaidi katika kipindi kama hiki tangu 1989 - Man United ni mwathiriwa mkuu aliyepoteza alama nyingi.

Ikiwa na mabao tisa pekee kutoka katika mechi zake nane, ni wazi kuna tatizo.

Huku wakiwa na kikosi cha wachezaji wenye umri mdogo zaidi katika msimu wa Ligi ya Kuu England, klabu hiyo ndio iliyofanya mshambulizi machache zaidi.

Kulingana na mabao yaliyotarajiwa, ni klabu ya Newcastle pekee ambayo imekuwa na mashambulizi mabaya kwa wastani ikilinganishwa na kikosi cha Ole Gunnar Solskjaer, kando na penalti.

Cha kufurahisha miongoni mwa mashabiki wa Man United ni kwamba huku washambuliaji wakishindwa kutengeneza fursa za kufunga mabao, safu ya ulinzi imewakabili washambuliaji wa timu pinzani na hivyo basi kuwa mojawapo ya safu bora za ulinzi kufikia kipindi hiki cha msimu.

Baada ya kutumia pauni milioni 130 kuwanunua mabeki Harry Maguire na Aaorn Wan-Bissaka na kumuuza mshambuliaji, Romelu Lukaku msimu uliopita hilo halionekani kuwa suala la kushangaza.

### TOTTENHAM

Kufikia Sikukuu ya Wapendanao maarufu 'Valentine Day', Tottenham ilikuwa katika nafasi ya tatu katika jedwali la Ligi Kuu England pointi tano pekee nyuma ya viongozi Liverpool.

Lakini pointi 22 kutoka mechi 20 tangu wakati huo zimeweka doa katika uhusiano kati ya kocha, wachezaji na klabu hiyo, huku kukiwa na mazungumzo kuhusu hatima ya wachezaji wa timu hiyo nao wengine wakitafuta kujiunga na klabu nyingine.

Tatizo kuu la Tottenham ni kwamba si eneo moja la timu hiyo ambalo lina tatizo.

Mbali na wachezaji kushindwa kuvamia lango la wapinzani wao kama ilivyokuwa hapo awali, safu ya ulinzi na ile ya mashambulizi kufikia sasa ziko katika hali mbaya zaidi katika misimu sita ambayo klabu hiyo imekuwa chini ya uongozi wa Mauricio Pochettino.

Huku ikiwa si rahisi kubaini, hii huenda inatokana na ukweli kwamba kocha na wachezaji wamekuwa pamoja kwa muda mrefu.

Wachezaji nane bado wapo katika klabu hiyo tangu msimu wa kwanza wa Pochettino wa 2014-15 ikilinganishwa na misimu mitatu pekee katika klabu ya Manchester City, na miwili katika klabu ya Liverpool, huku kati ya makocha 32 katika Ligi ya Mabingwa msimu huu, ikiwa ni kocha wa Atletico Madrid pekee, Diego Simeone ambaye ameinoa klabu hiyo kwa kipindi kirefu zaidi ya raia mwenza huyo wa Argentina.

### ARSENAL

Baada ya kuruhusu mashambulizi 10-12 kwa kila mechi katika kila msimu wa misimu 13 ya klabu hiyo chini ya kocha, Arsene Wenger, waliruhusu mashambulizi 13 katika kampeni yao ya kwanza chini ya Unai Emery msimu uliopita.

Cha kufurahisha pekee kwa Arsenal ni kwamba huku timu hiyo ikiwa chini ya shinikizo kali msimu huu, wameweza kuzuia upinzani kutekeleza mashambulizi makali ugenini huku ikiwa ni klabu ya Burnley pekee ambayo imeruhusu fursa chache zisizo na ubora zaidi ya kikosi cha Emery.

Hata hivyo, katika misimu mitano iliopita kabla ya msimu huu, ni klabu tatu pekee ambazo zimeruhusu mashambulizi 17 ama zaidi kwa mechi- klabu ya Sean Dyche mara mbili na ile ya David Moyes iliyoshushwa daraja msimu wa 2016-2017.

### CHELSEA

Licha ya kuwa na kikosi kichanga zaidi katika Ligi Kuu msimu huu, kimepongezwa na wengi, pia kimeruhusu mabao yasiyo ya kawaida 14 katika mechi zake nane kufikia sasa, huku Norwich pekee Watford na Southampton zikiruhusu mabao zaidi ya klabu hiyo.

Ni mara ya pili katika uongozi wa Roman Abrahamovich ambapo klabu hiyo imeruhusu mabao mengi katika kipindi hiki cha msimu, baada ya klabu hiyo chini ya uongozi wa Jose Mourinho ambapo walifungwa mabao 17 katika mechi zake nane mwaka 2015.

Huku akiokoa asilimia 48 ya mashambulizi yote ya upinzani msimu huu, kipa Kepa Arrizabalaga ana takwimu mbaya zaidi za uokoaji katika Ligi Kuu kufikia sasa na analaumiwa kuhusiana na matatizo ya safu ya ulinzi ya timu hiyo.

Kati ya magolikipa 25 walioshiriki katika Ligi ya England ni kipa wa Southampton pekee, Angus Gunn ambaye ameruhusu mabao mengi zaidi ya kipa wa Chelsea.

Licha ya Manchester City kuwa timu pekee inayokabiliwa na mashambulizi machache kufikia sasa msimu huu, ni timu nne pekee ambazo zimeruhusu upinzani kutengeza fursa rahisi zaidi za kufunga mabao zaidi ya Chelsea.

## Nukuu

"Ni mchezaji ambaye anaweza kuamua katika kila mchezo. Kila siku tunamwona ni bora zaidi, rekodi moja zaidi ya kushangaza kwa Leo [Lionel Messi]. Ni rahisi kusema, inaonekana ya asili, lakini ni vigumu sana kuiweka," **Kocha wa Barcelona, Ernesto Valverde akizungumzia rekodi ya Messi ya kufunga katika misimu 15 mfululizo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.**



"Watu wanasema kuhusu Ligi ya Mabingwa, lengo hilo bado hatujawa tayari, tumefunga sana kwa misimu miwili iliyopita na sina hofu kuhusu hilo, lakini tunapaswa kuendelea, kulifanyia kazi hilo," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, ambaye kikosi chake cha City kilipoteza katika kila mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa misimu miwili iliyopita.**



"Naamini kuna mengi zaidi yanakuja kutoka kwake, kwa sababu alikuwa nje ya uwanja kwa muda mrefu na sasa amerejea uwanjani kwa kiwango cha kuvutia. Bado kuna mechi nyingi, hivyo ana nafasi ya kutibitisha ubora wake na sina shaka kwa hilo," **Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp akimzungumzia Alex Oxlade-Chamberlain baada ya kufunga mabao mawili wakati Liverpool ikiibuka na ushindi wa 4-1 dhidi ya Genk kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumatano iliyopita.**





# SIRI KAGERE KUFUNGA BAO LA 30 AZAM IKIFA

**Na Adam Fungamwango**

DAKIKA ya 49, mpira mrefu wa juu uliopigwa kiufundi na Francis Kahata ulitua juu ya kichwa cha straika hatari, Meddie Kagere na kuujaza wavuni, akimwacha kipa Mwadini Ally wa Azam FC akigaagaa kwenye nyasi.

Ilikuwa ni Jumatano iliyopita, Oktoba 23 kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, straika huyo akitimiza bao lake la 30 kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara tangu alipotua msimu uliopita akitokea Gor Mahia ya Kenya.

Bao lake la kwanza kufunga kwenye Ligi Kuu ilikuwa Jumatano Agosti 22, mwaka jana msimu uliopita, ilikuwa dhidi ya Prisons ya Mbeya kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Ilikuwa ni dakika ya pili tu, alipoupata mpira kutoka kwa John Bocco na kupiga shuti dhaifu, lakini la ufundi lilitinga wavuni.

Msimu uliopita Kagere alitwaa Kiatu cha Dhahabu kwa kufunga mabao 23, na kabla ya mechi jana dhidi ya Singida United alikuwa amecheka na nyavu mara saba, hivyo kutimiza idadi ya mabao 30. Bao aliloifunga Azam lilikuwa ni la 30 kwa mchezaji huyo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Hii ni kazi yangu na nimekuwa nikijifanyia tathmini mwenyewe kila baada ya mechi, lakini pia huwa sidharau mechi yoyote ile, malengo yangu ni yale yale, na mechi moja ikiisha nasahau na kujiandaa kwa ajili ya mechi nyingine inayofuata," anasema straika huyo.

**1. UWANJA ULE ULE, GOLI LILE LILE**

Kegere amefunga mabao 30 kwenye viwanja mbalimbali nchini, lakini bao la kwanza la Ligi Kuu na la 30 amefunga kwenye uwanja huo huo na goli la upande huo huo.

Bao la kwanza alifunga kwenye Uwanja wa Taifa na la 30 amelifunga kwenye uwanja huo huo.

Pia bao lake la kwanza dhidi ya Prisons alilifunga goli la kusini na limefanana na la 30 ambalo amelifunga upande ule ule wa kusini mwa Uwanja wa Taifa.

Hata 'engo' ya mabao hayo jinsi yalivyoingia inafanana, yote mpira ulipita kulia mwa magolikipa.

Tofauti ipo kwenye staili ya kufunga, bao la kwanza lilifunga kwa mguu wa kulia, huku lile la 30 dhidi ya Azam akilifunga kwa kichwa.

**2. PASI YA MCHEZAJI MWENZAKE WA GOR MAHIA**

Pasi ya bao la 30 la Kegere imetoka kwa mchezaji mwenzake wa zamani wa Gor Mahia, Francis Kahata.

Kahata na Kagere ndio walikuwa mhimili wa Gor Mahia miaka miwili ya nyuma, lakini kwa sasa wote wako kwenye klabu ya Simba.

Kahata ndiye alikuwa mpishi mkubwa wa mabao ya Kagere wakiwa Gor Mahia na wameanza kukumbushia kwenye mechi dhidi ya Azam, Kahata alipotoa pasi ya mwisho ya kwanza akiwa na Simba, lakini akimpasia swahiba wake mkubwa na akafunga.

**3. AINA YA MABAO ALIYOFUNGA**

Mabao yake 30, nusu yake, yaani 15 ameyafunga kwa kutumia mguu wa kulia, huku tisa akiyafunga kwa kichwa.

Jumla ya mabao sita ameyafunga kwa kutumia mguu wa kushoto na kati ya hayo yote, manne akiyafunga kwa mikwaju ya penalti.

Msimu uliopita alifunga penalti tatu na msimu huu mpaka sasa ameshafunga penalti moja dhidi ya Kagera Sugar.

**4. ALIAHIDIWA SH. MIL 50 KABLA YA MECHI**

Taarifa zinaeleza kuwa kabla ya mechi aliahidiwa kitita cha Sh. milioni 50 na mdau mmoja wa soka ambaye alibishana naye na kuwekeana naye ahadi.

Habari kutoka ndani ya klabu ya Simba zinaeleza kuwa mdau huyo ambaye ni mwanachama mkubwa alimwambia kuwa anazifunga timu ndogo, lakini yeye anataka mabao hayo azifunge timu kubwa. Kagere akamuuliza kama timu zipi akamjibu kuwa kama ataifunga Azam FC mechi inayofuata basi atampa kitita cha Sh. milioni 50.

Straika huyo akatimiza ahadi, akafunga bao pekee kwenye mechi hiyo na Simba kuondoka na ushindi wa bao 1-0.

Taarifa zinaeleza kuwa Kagere akachukua mzigo wake na kuukabidhi kwa kapteni wa timu John Bocco kwa ajili ya kugawana na wachezaji wenzake.

"Hii ni timu, nafunga mabao kwa sababu nacheza na wenzangu, bila wenzangu siwezi kufanya hivi," anasema straika huyo.

**NAJUA WAJUA**



Pep Guardiola amepoteza mara moja tu katika ya mechi 20 za Ligi Kuu England alizocheza dhidi ya timu mpya zilizopanda daraja (ameshinda 15, kutoka sare mara nne na kupoteza moja).

SOKA



# ARSENAL INAPOTEMBEA NA MATARAJIO YA PEPE



**LONDON,** England

LIGI Kuu ya England inazidi kurindima. Mashabiki wanafurahia kila wakati. Kama ilivyo kwa klabu nyingine, Arsenal pia ina matumaini makubwa ya kufanya vizuri msimu huu.

**Vijana hao wa kocha, Unai Emery waliingia msimu huu wakiwa na morali kubwa yakuweza kuwa kwenye kiwango bora zaidi msimu huu.**

Wameshindwa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa msimu wa pili mfululizo. Kufungwa kwao kwenye fainali ya Ligi ya Europa mbele ya Chelsea ulikuwa wakati mgumu zaidi kwao msimu uliopita.

'Washika Bunduki' hao wa London walichapwa mabao 4-1 na The Blues kule mjini Baku. Pamoja na yote Emery bado ana kazi kubwa ya kufanya kwenye kikosi hicho.

Wakati anapewa timu hiyo kitu cha kwanza kilikuwa kuimarisha safu yake ya ushambuliaji na kutafuta mtu ambaye anaweza kuwa patina mzuri wa Pierre-Emerick Aubameyang na Alexandre Lacazzette.

## KUINGIA PEPE

Wakati Arsenal wakitafuta mshambuliaji mpya, walimsajili Nicolas Pepe kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo wakati wa kipindi cha majira ya joto. Wakati wa usajili huo, awali ilionekana ni vigumu kupata mchezaji mpya baada ya harakati zao za kutaka kumsajili Wilfred Zaha wa Crystal Palace kukwama. Hata hivyo, wakafanikiwa kumsajili Nicolas Pepe kutoka kule Lille.

Mshambuliaji huyo ndiye alikuwa mchezaji ghali zaidi wa Arsenal wakati walipomchukua kwa pauni milioni 72. Uhamisho wake wa kwenda pale kwenye dimba la Emirates ulionekana kuwa bora zaidi hasa kutokana na kuwa na kiwango bora zaidi kule Lille katika Ligi Kuu ya Ufaransa msimu uliopita.

Pepe alikuwa mmoja wa washambuliaji wakali zaidi na mara zote alikuwa tishio kwa timu pinzani kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, akiwa na uwezo wa kufunga, kupiga chenga na jicho zuri la goli.

Alimaliza msimu uliopita akiwa na mabao 23 na pasi za mwisho 12 katika mechi 41 alizocheza kwenye mashindano yote.

Kutokana na ada iliyolipwa na kiwango alichokionyesha kule Lille, mashabiki wengi wa Arsenal walikuwa na matarajio naye makubwa zaidi.

Pepe katika mchezo wake wa kwanza na klabu hiyo Agosti 11, mwaka huu dhidi ya Newcastle kwenye Ligi Kuu, alionyesha burudani ya kutosha kwa mashabiki wa Washika Bunduki hao.

## GIZA MBELE

Hata hivyo, katika mechi 11 alikuwa na bao moja tu kwa jina lake kwenye Ligi Kuu England kabla ya kuibuka Alhamisi iliyopita na kutupia mawili kwa mpira uliokufa (faulo) kwenye Europa League dhidi ya Victoria, na wimbo ukabadilika kwa mashabiki wa pale Emirates. Kile ambacho walikuwa wakikitegemea Ligi Kuu kutoka kwa winga huyo kikawa tofauti kabisa.

Pepe amejikuta kwenye wakati mgumu wa kuwafurahisha mashabiki wake kwenye Ligi Kuu. Na sasa wengi wameibua maswali juu ya uwezo wake na kama Arsenal ililamba dume kwa usajili wake.

Pepe hajawa katika kiwango cha kuvutia, kwani matarajio ya wengi yamekuwa tofauti kabisa katika wiki za hivi karibuni.

Ule uwezo wa kucheka na nyavu mara kwa mara kama ilivyokuwa kule Ufaransa umetoweka ghafla na hasa kwenye mechi za Ligi Kuu. Na maswali mengi yameibuka juu yake.

## UVUMILIVU MDOGO


Mara zote katika soka la dunia hii, mashabiki wanakuwa na shauku kubwa juu ya uwezo wa mchezaji wao mpya.

Ukichukua mfano wa Philippe Coutinho wakati akitua pale Barca wengi walikuwa na matarajio naye makubwa na ndivyo ilivyotokea kwa Pepe pale Arsenal.

Pepe mchezaji wa kimataifa wa Ivory Coast kiwango chake kimeonekana si cha kuvutia kabisa. Na mashabiki sasa wanaona kwamba mchezaji huyo si suluhisho la matatizo yao tena.

Hata hivyo, kuna uwezekano Pepe akarudi kwenye ubora wake aliokuwa nao kule Ufaransa, ni jambo la kusubiri na kuona.

KWA mwaka huu, hakuna mchezaji yeyote aliyeifungia klabu yake mabao mengi zaidi ya Robert Lewandowski wa Bayern Munich, ambapo kwa mwaka 2019 katika mechi 37 ameshatupia mabao 37. Idadi hiyo ni zaidi ya Lionel Messi, Cristiano Ronaldo na Kylian Mbappe.



NDANI YA 18



KLABU nne kati ya sita kubwa katika Ligi Kuu ya England, Arsenal, Chelsea, Manchester United na Tottenham - zimeonyesha ishara ya kudorora kama si kuelekea kusombwa na upepo wa kisulisuli hadi kufikia sasa msimu huu.

Uk. 16&17

# WAMEANZA NA REKODI UEFA MSIMU 2019-20




MBAPPE

**PARIS,** Ufaransa

MSIMU wa 2019/20 wa Ligi ya Mabingwa Ulaya unaendelea na tayari mechi tatu za kila kundi zimeshachezwa hadi sasa.

**Hadi sasa jumla ya mabao 53 yameshafungwa katika mechi 16 zilizopigwa.**

Michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ni mikubwa zaidi kwa klabu barani humo na kila mchezaji anakuwa na shauku kubwa ya kufanya vizuri katika mashindano hayo.

Mara zote kumekuwa na rekodi zinazowekwa na wachezaji katika michuano hiyo.

Katika makala haya tunawaangalia wachezaji watatu waliouanza msimu kwa kuweka rekodi katika michuano hiyo baada ya mechi tatu kwa kila kundi...

**1. MESSI – MCHEZAJI WA KWANZA KUFUNGA MARA 15 MFULULIZO**

Lionel Messi mara zote amekuwa baba wa rekodi katika michuano hiyo akiwa na klabu yake ya Barcelona tangu alipohitimu kutoka chuo cha kulelea vipaji cha La Masia.

Kipaji chake kimekuwa muhimu zaidi kwa kikosi chake tangu alipoanza kucheza kwenye michuano hiyo Desemba 2004 wakati Barcelona ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Shakhtar Donestk na baadaye akaanza kufunga kwenye ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Panathinaikos Novemba 2005.

Katika mchezo wa wiki iliyopita dhidi ya Slavia Prague, alifunga bao lililomwezesha kufikisha mabao 133 aliyofunga kwenye michuano hiyo. Hii ina maana kwamba, mzaliwa huyo wa kule Rosario nchini Argentina amekuwa akifunga kila msimu tangu mwaka 2005, ambayo ni sawa na misimu 15 mfululizo na kuweka rekodi hiyo.

Bao hilo pia lilimfanya kuwa sawa na mpinzani wake, Cristiano Ronaldo kwa kufunga dhidi ya timu 33 tofauti katika michuano hiyo.

**2. MBAPPE –MCHEZAJI MDOGO KAFUNGA MABAO 15 UEFA**

Kylian Mbappe ni mchezaji mwingine ambaye ameonyesha kwamba ana safari ndefu ya kwenda kwenye michuano hiyo na kuwa katika daraja la juu kabisa.

Alivuta hisia za mashabiki wengi wakati akiwa na umri wa miaka 17 alipoichezea Monaco msimu wa 2017 na kufuzu kucheza nusu fanali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya pamoja na kushinda taji la Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1.

Usajili wake wa kutua pale PSG umemfanya Mbappe kuwa kwenye daraja la juu huku akiwa ameshinda Kombe la Dunia na pia ametajwa kwenye orodha ya wachezaji wanaowania tuzo ya Ballon d'Or.

**1. HAALAND – MCHEZAJI WA KWANZA KUFUNGA MABAO SITA MECHI TATU**

Erling Braut Haaland ni mtoto wa beki gwiji wa Leeds United, Alf-Inge Haaland, lakini tofauti na baba yake, yeye amejijengea jina lake mwenyewe kwenye soka.

Mshambuliaji huyu wa zamani wa Molde si mgeni kwenye kucheka na nyavu, kwani alijulikana wakati wa michuano ya Kombe la Dunia ya Fifa ya vijana chini ya umri wa miaka 20 alipofunga mabao tisa wakati nchini ya Norway ikiibuka na ushindi wa mabao 12-0 dhidi ya Honduras Juni 2019.

Hiyo ikamfanya amalize michuano hiyo akiwa mfungaji bora licha ya Norway kutolewa mapema kwenye michuano hiyo na baadaye akahamia katika klabu ya nchini Austria ya Red Bull Salzburg.

Nchini Austria mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, ameendelea kufunga mabao kwa timu yake.


Haaland alianza kucheza michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ya msimu huu kwa kufunga mabao matatu 'hat-trick' wakati Salzburg ikiibuka na ushindi wa 6-2 dhidi ya Genk.

Halafu akafunga bao wakati timu yake ikifungwa mabao 4-3 na Liverpool pale Anfield na akafunga mawili wakati Salzurg ikichapwa 3-2 na Napoli.

Na hiyo imemfanya kuwa na mabao sita katika mechi tatu na yupo mbele ya Lionel Messi, Cristiano Ronaldo na Robert Lewandowski.

Zaidi ni kwamba, mabao yake mawili dhidi ya Napoli, yamemfanya kuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao sita katika mechi tatu za mwanzo, pia akifikia rekodi ya Karim Benzema ya kuwa mchezaji mwenye umri mdogo kufunga katika mechi tatu mfululizo za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**USILOLIJUA**




KATIKA mechi 43 ambazo Raheem Sterling amefunga kwenye Ligi Kuu England akiichezea Manchester City, timu hiyo haijawahi kumaliza kwa kipigo (imeshinda 41 na kutoka sare mara mbili).





# Hospitali ya kanda kununua helikopta

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda ya Mbeya ina mpango wa kununua helikopta maalum kwa ajili ya kutoa huduma za dharura eneo lolote la mikoa ya nyanda za juu kusini.

Lengo la kununua chopa hiyo ni kuokoa maisha ya majeruhi wa ajali na wagonjwa wengine wa dharura. Hayo yalisemwa hivi karibuni na Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji, wakati wa mahojiano maalum na Nipashe kuhusu namna huduma za magonjwa ya dharura zinavyozidi kuboreshwa pamoja na changamoto zake.

Alisema malengo ya hospitali hiyo ni kununua helikopta ambayo itakuwa na huduma zote za matibabu na wataalamu wa afya na itafika kila eneo lolote taarifa zitakapotolewa kutoa huduma.

"Sababu ya kuwa na mpango huu wa kununua helikopta ya kutoa huduma kwa wagonjwa wa dharura katika hospitali yetu ya kanda ni kuokoa maisha ya watu kwa haraka zaidi ukilinganisha na ilivyo sasa, ambapo hospitali inatumia gari ya wagonjwa ambulance kuhudumia wagonjwa, tumegundua bado kuna uhitaji mkubwa kwa wateja wetu," alisema Dk. Mbwanji.

Alisema huduma za helikopta itakuwa rafiki zaidi kwa sababu itafika maeneo yote kwa wakati bila kujali changamoto za miundombinu ya barabara au majengo.

Kuhusu gharama za kununua helikopta alisema hospitali imejipanga kwa kushirikiana na Wizara ya Afya pamoja na wadau wengine watakaoisaidia kutimiza azma hiyo ambayo alisema itakuwa na manufaa kwa taifa katika kuboresha huduma za afya.

Daktari bingwa wa magonjwa ya dharura katika hospitali hiyo, Dk. Prosper Bashaka alisema kuna changamoto ya kushindwa kufika kwenye maeneo yenye changamoto ya barabara kwa wakati pindi wanapopata taarifa za ajali na magonjwa mengine ya dharura kwa kutumia gari, hivyo uwepo wa helikopta utarahisisha huduma za matibabu.

Baadhi ya wananchi mkoani Mbeya wamepongeza mpango wa Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya kununua helikopta kwa ajili ya huduma ya magonjwa ya dharura wakidai itasaidia kuokoa maisha ya watu wa uharaka zaidi pindi yanaporipotiwa.

Miongoni mwa wananchi ni Neema Patrick, mama lishe katika Stendi ya Kabwe, alisema maeneo mengi hayafikiwi na gari linalotoa huduma za dharura kwa sababu ya jiografia hivyo mpango wa kununua helikopta utatoa msaada mkubwa zaidi hasa kwa ajali za moto



Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Mary Mwanjelwa (aliyeshika kipaza sauti) akipokea mfuko wa saruji kutoka kwa maofisa wa Benki ya NBC Mkoa wa Mbeya ambapo benki hiyo ilitoa msaada wa mifuko 600 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya jijini Mbeya. **PICHA NA NEBART MSOKWA.**

# Waambiwa lazima kushiriki uchaguzi

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WANAWAKE na wenye ulemavu mkoani Mbeya, wamehamasishwa kugombea nafasi mbalimbali za uongozi bila woga kwani wana uwezo na sifa za kushika nyadhifa mbalimbali za kiuongozi.

Wito huo ulitolewa juzi na mwanachama wa TGNP-Mtandao, Gema Akilimali, wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wanawake, vijana na watu wenye ulemavu mkoani Mbeya kushiriki kwenye uchaguzi ujao wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji ambao ni sehemu ya kutekeleza demokrasia.

Alisema mafunzo hayo ambayo yanaratibiwa na TGNP-Mtandao, yanalenga kufanya kampeni ya kuhamasisha uchaguzi unaozingatia demokrasia na ujuzi ili kutoa nafasi kwa kila mwanamke, kijana na mwenye mlemavu mwenye utashi na uwezo kugombea na kutimiza haki ya kuchaguliwa na kuongoza.

Akilimali ambaye ni mwanaharakati wa masuala ya jinsia na haki za binadamu alisema mafunzo hayo yatasaidia kuimarisha makundi hayo kujengewa uwezo wa kugombea nafasi za uongozi mbalimbali bila woga ili kuiletea nchi maendeleo.

"Alisema kwa tathmini aliyoifanya akiwa mkoani Mbeya amegundua mwitikio wa kundi la wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kushiriki kwenye michakato mbalimbali ya uchaguzi wa serikali za mitaa," alisema Akilimali.

Aidha, katika mafunzo hayo alipongeza hatua ya madiwani wanawake kuwatia moyo na kuwaeleza mbinu walizotumia wao kushika nyadhifa hizo jambo ambalo lilileta hamasa kwa wengine kujifunza kusimama kwa miguu yao bila kutegemea nguvu ya chama au mwanaume.

Wanawake walioshiriki mafunzo hayo walisema mafunzo hayo yamewaongezea ujasiri na uthubutu wa kugombea nafasi za uenyeviti wa mitaa, vitongoji na vijiji kwenye maeneo yao huku wakihamasishana kushikamana na kuwa kitu kimoja.

Diwani wa viti maalam Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Monica Deguha, alieleza changamoto alizokumbana nazo wakati anagombea nafasi hiyo mwaka 2015 alisema kulikuwa na vitendo vya rushwa ya fedha na ngono kutoka kwa baadhi ya viongozi wanaoshiriki mchakato wa uchaguzi.

Alisema viongozi hao walikuwa wanatoa nafasi ya kuchagua aidha utoe rushwa ya ngono au fedha ndipo uingie kwenye kiny'ang'anyiro jambo ambalo alilipinga na kutoa msimamo hadi wakaogopa na kumpa nafasi ya kugombea na kushinda hadi sasa anawatumikia wananchi.

Mhamasishaji kutoka TGNP-Mtandao, Jackson Masawe, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wanawake kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kuanzia serikali za mitaa hadi kwenye uchaguzi mkuu ujao.

Aliwasisitiza wanawake kuchangamkia fursa mbalimbali za uongozi zinapojitokeza kwani kwa kufanya hivyo watajifunza mambo mengi ambayo yatawasaidia hata watakapofikia hatua kubwa ya kushika madaraka ya juu.

# Wahimizwa kufuatilia taarifa za hali ya hewa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKULIMA wa Mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wametakiwa kutumia vizuri kikamilifu taarifa za utabiri wa hali ya hewa zinazotolewa na wataalamu ili ziwasaidie kwenye uzalishaji.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Meneja wa Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) Kanda, Issa Hamad, alipokuwa akizungumza na Nipashe namna walivyojipanga kutoa elimu kwa wakulima katika kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Alisema taarifa za hali ya hewa zimekuwa zikitolewa na TMA, kila wakati kwa lengo la kuwaandaa wananchi na wakulima ili waanze kuchukua tahadhari.

Alisema mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini imekuwa ikipata mvua nyingi na kusababisha baadhi ya maeneo kutishiwa na maafa na wakati mwingine mazao kuharibiwa hivyo taarifa sahihi za hali ya hewa zinasaidia wakulima kuchukua tahadhari mapema.

"Kutokana na taarifa za utabiri wa hali ya hewa msimu wa kilimo utakapowadia mkulima anapaswa kupanda mbegu ambazo zitastahimili hali ya mvua zinazotarajiwa kunyesha ili kuepuka kuingia hasara vile vile wananchi wanatakiwa kujihadhari katika makazi yao kwani mvua hizo zinazaweza kuambatana na upepo pamoja na mafuriko na kusababisha majanga," alisema Hamad.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, baadhi ya wakulima walisema taarifa hiyo ya mamlaka ya hali ya hewa inawataka wajiandae kupanda mbegu zitakazohimili mvua nyingi.

Miongoni mwa wakulima hao, Josephat Mwambeso, kutoka kata ya Iduda jijini Mbeya, alisema kwa uzoefu wake kwenye shughuli za kilimo hasa msimu wa mvua nyingi inatakiwa kupanda mbegu za zamani ambazo zinaweza kuhimili mvua.

Alisema wakipanda mbegu za kisasa kwa kipindi hiki cha mvua zinaweza kukomaa shambani na kuanza kuharibika wakati mvua zikiwa bado zinaendelea kunyesha.

Mkulima Agnes Wiliam, alisema kutokana na hali hiyo ya kuwapo kwa mvua nyingi maofisa kilimo wa ngazi zote wanatakiwa kuwasaidia wakulima kupanda mbegu bora zitakazo kuwa na uvumilivu wa mvua.





# Watoto wapimwe VVU bila masharti

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WABUNGE wameshauri watoto waruhusiwe kupima Virusi ya Ukimwi (VVU) bila kuweka kigezo cha umri.

Lengo ni kuwatambua mapema na kupunguza kasi ya maambukizi. Kwa mujibu wa Sheria ya Ukimwi ya Mwaka 2008 kifungu cha 15(2), mtoto au mtu ambaye hana uwezo wa kupokea matokeo anaweza kupima VVU kwa ruhusa ya maandishi kutoka kwa mzazi au mlezi anayetambulika.

Aidha, sheria hiyo imeweka umri wa miaka 18 wa kupima VVU bila ridhaa ya wazazi.

Ushauri huo waliutoa jana katika kikao cha Kamati ya Bunge inayoshughulikia Ukimwi na dawa za kulevya ilipokutana na Mtandao wa Vijana na Watoto kutoka Mwanza (MYCN) ambao uliwasilisha pendekezo la miaka 12 mtoto kupima VVU bila ruhusa ya mzazi au mlezi.

Wabunge hao walikubali kuwapo na mabadiliko katika kipengele hicho ili watoto waruhusiwe kupima kwa ridhaa yao, lakini kusiwe na kigezo cha umri ili kujua hali za maambukizi.

Mbunge wa Masasi(CCM), Rashid Chuachua, alisema hakuna sababu ya kuweka kigezo cha umri kutokana na kwamba watoto kwa sasa wanaanza ngono wakiwa na umri mdogo.

Aidha, Mbunge wa Nkasi Kaskazini (CCM), Ally Keissy, alisema watoto waruhusiwe kupima wakati wowote hata wakiwa chini ya umri wa miaka 12 inayopendekezwa na mtandao huo.

"Watoto wasilazimishwe kusubiri ridhaa ya wazazi na walezi, tusiwabane watoto kwa kuwawekea umri wakati sisi wenyewe wazazi pamoja na kutowekewa kigezo cha umri hatupendi kupimwa," alisema.

Alieleza kuwa baadhi ya wazazi na walezi wamekuwa wazito kupima na kutowaruhusu watoto kupimwa.

Kwa upande wake, Mbunge wa Bunda (CCM), Boniface Getere, alihoji sababu ya kuweka ukomo wa umri wakati watoto wamekuwa wakipimwa tangu kuzaliwa katika maeneo mbalimbali hasa wakati wa kliniki, hivyo wasizuiwe kusubiri ridhaa ya wazazi.

Kadhalika, Mbunge wa Chambani (CUF), Yusufu Salim Hussein, alisema anakubaliana na suala la ukomo wa umri kwenye pendekezo la viongozi wa dini ambao walishauri mtoto aruhusiwe kupima hata katika umri wa miaka 10 kutokana na misingi ya dini kuanza kuwafundisha mafunzo mapema.

Awali, akitoa mapendekezo kwa kamati hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa MYCN, Shaban Maganga, alisema kwa sasa vijana au watoto wanaogopa kuomba ruhusa ya kupima VVU kwa kuhofia kuhisiwa kuwa wameanza kujihusisha na mahusiano ya kingono.

"Ni vigumu sana kwa mzazi au mlezi kutoa ruhusa ya kupima VVU kwa watoto wao, kwa sababu wao wenyewe wanaogopa kupima, na baadhi ya wazazi au walezi wanawabaka na kuwalawiti watoto wao hawawezi kuwapa ruhusa watoto kupima," alisema.

Aliwaambia kuwa watoto wenye umri wa miaka 12 wapimwe bila ridhaa ya wazazi kwa kuwa idadi ya vijana au watoto kupima VVU nchini ipo chini huku takwimu zikionyesha waliopima ni wenye umri wa miaka 15-17, 15-24, 15-49 na ni vigumu kupata takwimu za umri wa miaka 6-14 au 10-14. Maganga alisema kasi ya maambukizi inatisha nchini, katika watu 200 wanaokutwa na VVU asilimia 40 ni vijana wa umri wa miaka 15 na wengi kati yao hawapimi na kama wangepima hali ingetisha zaidi.

"Utafiti wetu asilimia 60 ya watu tuliowahoji walipendekeza kwamba watoto waruhusiwe kupima virusi vya Ukimwi katika umri wa miaka 12, kutokana na kwamba mitaala ya elimu mtoto wa umri huo anajifunza mambo kuhusu maambukizi hayo," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema Rwanda, Uganda, Lesotho, Malawi, na Afrika Kusini zimeweka umri ni miaka 12, huku Kenya ni miaka 15 na Tanzania ni miaka 18.

Wakizungumzia umuhimu wa kupimwa watoto, mabinti Pudensia Mbiliza na Doreen Odemba, walisema kuna umuhimu wa kupimwa na kuanza kutumia dawa mapema.



Baadhi ya wananchi ambao majina yao hayakupatikana wakionyesha zao la zabibu kwenye tamasha la Urithi Festival lililofanyika jana, viwanja vya Mashujaa jijini Dodoma **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ushirika yapania kuanzisha benki

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKISHO la Vyama vya Ushirika nchini (TFC) limetangaza nia ya kuanzisha benki ya ushirika.

Ili kutimiza azma hiyo, TFC imeiomba serikali kuwasaidia mchakato wa kuanzisha benki ya ushirika ili kuwasaidia wakulima na wafanyabiashara na wateja wao kuepuka riba kubwa kwenye mikopo inayotozwa na taasisi za fedha.

Ombi hilo lilitolewa na Mwenyekiti wa Shirikisho, Theresia Chitumbi, katika mkutano wa kujadili maazimio ya pamoja ya mikakati ya kufungua benki hiyo.

Washiriki wa mkutano huo walikuwa vyama vya ushirika vya msingi, vikuu na mashirikisho uliofanyika jijini hapa.

Alisema wanaamini kuanzishwa kwa benki hiyo itakuwa suluhisho la matatizo ya wanaushirika.

"Tunaomba serikali itusimamie katika hili kwa sababu kuanzisha benki yetu ya ushirika ni sawa tumeingia vitani kupambana na jamii kwa sababu tuna kwenda kuwanyang'anya wateja benki binafsi," alisema Chitumbi.

Alieleza kuwa wanaushirika wanaamini suala hilo la kuanzishwa benki hiyo litakuwa msaada mkubwa kwa wakulima, wafanyakazi pamoja na wafanyabiashara.

Alisema moja ya faida ambazo watazipata baada ya kufungua benki hiyo ni pamoja na kupata gawio, kwa sababu itakuwa ikijitegemea kwa kujiendesha.

Mwenyekiti wa kamati ya uanzishwaji benki hiyo, Ibrahim Mbaga, alisema mwamko wa vyama kuanzisha benki hiyo ni wazo zuri kwa kuwa itawasaidia kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili.

Alisema kuwapo kwa ushirika kutasaidia wakulima na wafanyakazi ambao wapo katika vyama hivyo kupata fursa ya kuchukua mikopo kwa riba nafuu.

Kwa upande wake, Sudi Mangara, kutoka Ngome Saccos, alisema benki hiyo itaimarisha vyama vya ushirika na kwamba hakuna sababu ya vyama hivyo kuhofia bali kinachotakiwa ni kila chama kuweka hisa kwenye benki hiyo itakayoanzishwa.

# Hudumieni wakulima kwa wakati

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHAMA cha Wasambazaji wa Pembejeo za Kilimo na Mifugo nchini (Tadcos) kimevitaka vyama vya ushirika vya mazao kufikisha mbegu, mbolea na viuatilifu kwa wakulima vijijini mapema na kwa wakati.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mwenyekiti wa Tadcos, Gerald Mlenge, alipozungumzia changamoto ya ufikishwaji wa viuatilifu kwa wakulima waliopo pembezoni.

Mlenge alisema ili kuhakikisha wakulima wote vijijini wanapata mbolea na mbegu bora kwa wakati ni lazima ushirikiano uwepo baina ya vyama vya ushirika vya mazao ambavyo kila chama kinajua maeneo ambayo wakulima wanapatikana kulingana na zao wanalolima na msimu wa mvua katika ukanda waliopo.

Alisema wameamua kufanya hivyo ili kuhakikisha wakulima waliopo vijijini wanafikiwa kwa wakati na mbegu bora ambazo husambazwa na Tadcos kupitia vyama hivyo. "Naamini sisi na vyama vingine vya ushirika tukishirikiana tutafanikiwa kwa kiasi kikubwa kutatua changamoto ya upatikanaji mbegu bora kwa wakulima waliopo pembezoni mwa miji hususani vijiji vya ndani," alisema Mlenge.

Alieleza kuwa lengo lao ni kuona wakulima wanafaidika na kazi inayofanywa na chama hicho hasa ikizingatia hivi sasa wakulima wanahitaji kufanya kilimo chenye tija ambacho kitawanufaisha wadau wote. Alisema wanatarajia kuingia mkataba na kampuni zinazozalisha mbolea nje ya nchi ili kuboresha na kurahisisha upatikanaji wake kwa wingi na kwa wakati.

Alisema anaamini kwa kushirikiana na serikali mkakati huo ukifanikishwa changamoto ya upatikanaji mbolea hapa nchini itakwisha.

Katibu wa Tadcos Elia Kajuni, aliwataka wakulima wasihofu juu ya upatikanaji wa mbolea kwa sababu wanatarajia kuingiza nchini tani 45,000 za mbolea kwa ajili ya msimu ujao wa kilimo.

Alisema mbolea hiyo itasambazwa kwa wakulima kwa wakati kulingana na msimu wa mvua katika eneo husika na kukidhi mahitaji ya wakulima katika maeneo ya mijini na vijijini.





# SMZ yasifu UN kuwagusa watu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), imesema utekelezaji wa mipango inayowekwa na Umoja wa Mataifa (UN) na taasisi zake, umekuwa wa mafanikio makubwa na umewagusa hata wananchi wa kawaida.

Rais wa Zanzibar, Ali Mohamed Shein, alisema hayo, katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Balozi Seif Ali Iddi, katika sherehe za maadhimisho ya miaka 74 ya UN.

Alisema Zanzibar imeendelea kufanyakazi na taasisi hizo za UN katika kuendeleza na kukuza elimu, afya, mazingira, uvuvi, kilimo, kuimarisha demokrasia na utawala bora.

Aidha, katika kulinda na kuimarisha haki za binadamu, mapambano dhidi ya udhalilishaji wa kijinsia na watoto na masuala mengine ya maendeleo.

Alielezea imani yake kwamba raia wengi Unguja na Pemba na Tanzania nzima, wanaifahamu miradi hiyo pamoja na mafanikio yaliyopatikana.

Alisema jamii ilikuwa na uzoefu wa kushuhudia shereha za mashirika na taasisi za umoja huo katika vipindi vilivyopita zilikuwa zikihudhuriwa zaidi na viongozi wa ngazi za juu wa serikali na mashirika ya kimataifa bila wananchi.

Alifahamisha kwamba wananchi hasa wakulima wengi wamefurahia na kuzipongeza juhudi zilizochukuliwa hadi wakaweza kupatiwa msaada wa vihori 100 vya kubebea mwani, kila kimoja kikiwa na uwezo wa kubeba takribani nusu tani.

Akizungumzia juhudi za kuwawezesha wanawake kiuchumi, kisiasa na kijamii, alisema imeandaa mipango mbalimbali iliyoainishwa ndani ya mpango wa kupunguza umaskini Zanzibar (MKUZA 111) pamoja na Dira ya Maendeleo 2020.

Alisema mikopo 1,944 yenye thamani ya Sh. bilioni 3.52 imeshatolewa tokea ulipoanzishwa mfuko huo, katika mwaka 2013 ambayo imewanufaisha jumla ya wananchi 31,325, kati yao 17,542 ni wanawake ikiwa ni zaidi ya asilimia 50.

Akitoa salamu za UN Mwakilishi, Shirika la UN la Kuhudumia Idadi ya Watu (UNFPS), Jacquilen Mahon, alisema ushirikiano wa pamoja wa mataifa wanachama ndiyo njia pekee zitakazofanikisha malengo ya umoja huo. Mohan alisema wataendelea kuwajengea mazingira bora wananchi wa Zanzibar hasa kundi kubwa la wawanake katika masuala ya elimu itakayowasaidia kujenga nguvu katika harakati za maendeleo.



Mgeni rasmi kwenye sherehe ya siku ya wazazi wa Shule ya Razufak ya Kwarara, Zanzibar, Mratibu wa Programu ya Kinywa na Meno wa kampuni ya Colgate Tanzania, Noah Sarakiky akiongea na wazazi na wanafunzi katika sherehe hiyo iliyofanyika kwenye ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Kwarara jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

## Bodi ya Mikopo yaanza kuchagua

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BODI ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) Zanzibar, imechagua awamu ya kwanza ya wanafunzi walioomba mikopo ya kujiunga na elimu ya juu kwa mwaka wa masomo 2019/2020.

Akitoa taarifa hiyo kwa vyombo vya habari kwenye ofisi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Mkurugenzi wa Bodi hiyo, Iddi Khamis Haji, alisema waombaji walioteuliwa kwa awamu hiyo ni 1,261 kati ya 2,475 walioomba.

Alisema miongoni mwa waombaji hao walioteuliwa kwa vyuo vya nje ya nchi ni 136 sawa na asilimia 10 na vyuo vya ndani ni 112,525 sawa na asilimia 90 kwa ngazi za shahada ya kwanza, ya pili na ya uzamivu.

Mkurugenzi wa bodi hiyo, alifahamisha kuwa kazi ya uteuzi wa waombaji wa mikopo kwa awamu ya pili inatarajiwa kuendelea Novemba mwaka huu, ambapo lengo la mwaka huu ni kutoa wanafunzi wapya wapatao 1,860.

Aidha, alisema matarajio ya Bodi ya Mikopo ni kutumia Sh. bilioni 12.13 kwa kulipia wanafunzi wapya na wanaoendelea kwa ada za masomo, malazi na chakula ambapo Sh. bilioni 9 .47 zimetoka mfuko wa Hazina na Sh. bilioni 2.6 marejesho ya mikopo ya wanafunzi.

Akizungumzia kuhusiana na nafasi za ufadhili wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa vijana waliofaulu daraja la kwanza kwa mtihani wa kidato cha sita, alisema walioteuliwa kujaza nafasi hizo ni 60 wakiwamo wanawake 30 na wanaume 30.

# Balozi Iddi ahimiza wananchi kuwa wavumilivu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema wananchi wanapaswa kuendelea kujitolea na kuvumilia changamoto zinazojitokeza kwenye miradi ya maendeleo inayowagusa moja kwa moja.

Alisema kitendo cha baadhi ya wananchi kubeba bango la kulalamikia mazao yao kudai fidia licha ya kwamba ni haki yao, lakini kile wanachotengenezewa na kufikishiwa kwenye maeneo yao huleta faida na ustawi wa maisha zaidi.

Balozi Iddi, alisema hayo akikamilisha ziara yake katika mkoa wa Kusini Unguja alipokuwa akikagua maendeleo ya miradi mbalimbali ya maendeleo inayowagusa katika shehia na majimbo yao ikiwamo pia ile ya Chama Cha Mapinduzi.

Alisema ipo miradi ya huduma za majisafi na salama na ujenzi wa barabara zinazotekelezwa na serikali kuu ikiungwa mkono na washirika wa maendeleo ya miradi ambayo wakati mwingine mali pamoja na baadhi ya nyumba za wananchi huathirika.

Inawezekana kuwa ni kutokana na upanuzi wa miradi ambayo wananchi wanaopata changamoto hiyo wanapaswa kuwa wavumilivu.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar aliwapongeza wananchi wanaoendelea kuwa wastahimilivu kutokana na athari hizo na kuwaahidi kwamba Serikali Kuu kupitia taasisi zinazohusika na miradi hiyo zitaendelea kufanya tathmini ya hasara zinazowakumba baadhi ya wananchi hao kwa kupisha miradi ya ujenzi.

Akitoa taarifa ya maendeleo ya ujenzi wa barabara ya Koani hadi Jumbi yenye urefu wa kilomita 6.3 inayotarajiwa katika kiwango cha lami, mhandisi wa ujenzi wa barabara, hiyo kutoka kampuni ya Mecco Nassor Ramadhan, alisema mwendelezo wa mradi huo umesita kutokana na mvua zinazonyesha.

Mhandisi Nassor alisema mradi huo kwa sasa umefikia asilimia 40 baada ya kukamilika kwa kazi za kusafisha eneo linalopita barabara, kumwaga vifusi pamoja na uwekaji wa makalvati kwenye maeneo yanayopita maji.

Aliwahakikishia wananchi wa vijiji vinavyopita barabara hiyo kwamba ukamilishaji wa mradi huo kwa sasa umebakiza miezi mitatu iwapo hakutakuwa na mvua.

Mapema Mkuu wa Mkoa Kusini Unguja, Ayoub Mohamed Mahmoud, alimwagiza mhandisi wa ujenzi wa bara hiyo kujenga mazingira ya kusafirisha watu na mizigo kwa haraka katika kipindi cha mpito kuwawezesha wananchi wanaotumia barabara hiyo wanaondokana na tatizo la ugumu wa usafiri.

Akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Uroa baada ya kukagua kisima cha majisafi na salama kilichopo Kijiji cha Bambi, ambacho kinatarajiwa kusambaza huduma hiyo katika kijiji chao, Balozi Seif aliwapongeza kwa ustahimilivu wao wa muda mrefu hadi serikali iliposikia kilio chao.

Balozi Seif alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, itaendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi, katika kuwasogezea wananchi huduma muhimu ikiwa ni kukamilisha ahadi ilizozitoa.

# Ma-DC, wakurugenzi watupiwa 'zigo' la miradi iliyotelekezwa

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

MKUU wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabriel, amewaagiza wakuu wa wilaya, na watendaji wa serikali wa halmashauri zote mkoani humo kufuatlili na kuikagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa.

Alitoa agizo hilo jana kwa nyakati tofauti wakati akizindua miradi ya ujenzi wa barabara ya lami na soko la kisasa linalojengwa Mtaa wa Katundu inayotekelezwa kwa fedha ya uwajibikaji katika jamii (CSR) kutoka Mgodi wa Geita ( GGML ) kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji Geita mkoani hapa.

Mkuu huyo amsema kuwa viongozi hao hawanabudi kufuatilia na kuikagua miradi inayotekelezwa kwenye halmashauri zao ili kubaini miradi inayojengwa chini ya kiwango na makandarasi wazembe na wababaishaji.

Mhandisi Gabriel akizindua miradi hiyo ya ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilometa 1.5 inayojengwa kwa kiwango cha lami na soko la kisasa linalojengwa katika Mtaa wa Katundu, alisema ni aibu kwa wakuu wa wilaya na watendaji wa serikali kiongozi wa kitaifa kufika kwenye eneo la mradi na kubaini upungufu ikiwamo majengo kujengwa chini ya kiwango wakati wakuu na watendaji hao wapo kwenye maeneo yao.

Pia aliwaagiza wakuu wa wilaya na watendaji wa serikali kuwachukulia hatua za kisheria makandarisi watakaoshindwa kukamilisha miradi walioyopewa kwa wakati sambamba na wanaojenga miradi waliyopewa na halmashauri chini ya kiwango, huku akiwaonya kuwa Mkoa wa Geita si sehemu ya makandarasi kuchuma fedha za umma na kutoweka.

Kuna shida kubwa hapa katika ujenzi wa miradi ya serikali, haiwezekani jengo moja la aina hiyo hiyo katika halmashauri moja lijengwe kwa kiasi cha Sh. milioni hamsini halafu katika halmashauri nyingine litumie zaidi ya Sh. milioni 100. wakuu wa wilaya na watendaji fuatilieni mkague miradi kuondoa aibu hiyo,"alisema Mhandisi Gabriel.

Akizungumzia ujenzi wa mradi wa barabara ya kiwango cha lami kutoka eneo la nyumba za makazi ya askari polisi maarufu 'Siro Barracks' kwenda barabara kuu la Geita-Mwanza lenye urefu wa kilometa 1.5 unaotekelezwa na Mgodi wa GGM kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji wa Geita, alisema miradi hiyo miwili barabara ya kiwango cha lami ,soko la kisasa la Mtaa wa Katundu imezinduliwa rasmi na ni sehemu ya miradi muhimu inayotekelezwa mkoani humo.

Mkurugenzi Mtendaji wa GGML, Richard Jordison, alisema kuwa mgodi huo umetenga fedha za kitanzania kiasi cha Sh. bilioni 9.2 za CSR kwa bajeti ya mwaka huu 2019 /2020 zitakazotumika kutekeleza miradi mbalimbali mkoani humo ikiwamo soko la kisasa ,barabara ya kiwango cha lami pamoja na miradi mingine.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-Tamisemi, Selemani Jafo, akikabidhi cheti cha shukurani kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara ya DCB, Godfrey Ndalahwa (kushoto), kwa kutambua udhamini wa benki hiyo katika hafla ya kutoa Tuzo za Ubora wa Elimu Tanzania kwa wanafunzi, walimu, shule, halmashauri na mikoa waliofanya vizuri katika mitihani ya taifa mwaka 2019, jijini Dar es Salaam mwisho mwa wiki. Kulia ni Naibu Katibu Mkuu Tamisemi, Godfrey Mweli. **MPIGAPICHA WETU**

# Halmashauri yamwaga vitabu 88,652 shule 72

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

ZAIDI ya vitabu 88,652 vya darasa la awali hadi darasa la tano vimegawiwa katika shule za msingi 72 Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga ili kukuza kiwango cha taalumu na kupunguza changamoto ya ukosefu wa vitabu kwa wanafunzi.

Vitabu hivyo ni vya masomo ya Hisabati, Kiswahili, Kingereza, Sayansi, Uraia na Maadili, Maarifa ya Jamii na vya Kifaransa vya hatua ya kwanza na ya pili.

Hayo yalibainishwa na Ofisa Elimu (Vifaa na Takwimu), Mwalimu Sadick Juma, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake na kusema awali kitabu kimoja kilikuwa kinatumika kwa wanafunzi wanne, lakini kwa sasa kila mwanafunzi atakuwa na kitabu chake.

Alisema mbali na vitabu vilivyotolewa kwa wanafunzi wa darasa la awali hadi la tano, wanatarajia kupokea vitabu vingine kwa ajili ya wanafunzi wa darasa la sita na la saba, huku asilimia kubwa ya vitabu hivyo vikiwa vya masomo ya Sayansi na Hisabati.

Hata hivyo, Juma alisema mbali na kutoa vitabu hivyo, bado wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa walimu katika shule za msingi ambapo mwaka jana Halmashauri ya Mji wa Kahama ilipokea walimu 20.

"Tumekuwa na changamoto ya walimu kwenye shule zetu za msingi na kwa kuliona hilo, halmashauri ilichukua walimu wa masomo ya Sanaa 21 kutoka shule za sekondari ambako kulikuwa na zaidi ya walimu na kwenda kufundisha shule za msingi zenye changamoto ya uhaba wa walimu," alisema Juma.

Juma aliongeza kuwa Shule ya Msingi Majengo ina jumla ya wanafunzi 2,800 na ina uhitaji wa walimu 64 na walipo ni 36, huku Shule ya Msingi Muhungula ina jumla ya wanafunzi 4,000, uhitaji wa walimu 88 na walipo 39 tu, lakini shule hizi zimekuwa zikifanya vizuri kwenye mitihani ya mwisho.

# 142 wakatishwa masomo miezi tisa kwa mimba

**Na Said Hamdani,** LINDI

JUMLA ya wanafunzi wa kike 142 wanaosoma shule mbalimbali za msingi na sekondari mkoani Lindi, wamekatishwa masomo baada ya kupewa mimba kwa kipindi cha miezi tisa iliyopita.

Wilaya ya Kilwa imetajwa kuwa inaongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi walioacha masomo kutokana na ujauzito.

Kwa mujibu wa taarifa iliyowasilishwa kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) na Ofisa Elimu (Taaluma), Htibu Tuki, walipata ujauzito kuanzia Januari hadi Septemba 30, mwaka huu.

Akiwasilisha taarifa ya hali ya mimba, Tuki aliitaja Halmashauri ya Kilwa inaoongoza kwa kuwa na mimba (52) zikiwamo shule za msingi 22 na sekondari 30, ikifuatiwa na Lindi/Mtama mimba 30, kati ya hizo sekondari ni mimba 24 na msingi sita.

Tuki alisema Halmashauri ya Liwale mimba 21, ambapo kwa shule za sekondari mimba 16 na msingi tano. Lindi Manispaa mimba 19, ambapo mimba mbili ni kwa shule za msingi na 17 kwa shule za sekondari.

Kwa Wilaya ya Nachingwea ni mimba 13, kati ya hizo mimba tisa ni kwa shule za sekondari na msingi nne wakati Ruangwa zipo mimba saba, ambapo kwa shule za msingi mimba mbili na sekondari tano.

Hata hivyo, Ofisa Elimu huyo wa Taaluma hakuelezea hatua za kisheria zilizochukuliwa dhidi ya wanaume waliohusika kuwapa mimba wanafunzi hao.

Wakichangia tatizo la mimba shuleni, baadhi ya wajumbe walishauri itungwe sheria itakayotoa adhabu ya kifungo kwa wanafunzi wa kike watakaowaficha wanaume wanaowakatisha masomo kwa kupewa ujauzito.

Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Christopher Ngubiagai, aliwalaumu baadhi ya walimu, ambao alisema wamekuwa na tabia ya kushiriki mapenzi na wanafunzi wao, hali inayochangia kukatisha ndoto zao na kushusha kiwango cha elimu katika Mkoa huo.

Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, aliwaagiza wakuu wa wilaya kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kuwasaka wanaume waliohusika kuwapa mimba wanafunzi na kuwafikisha mahakamani.

## Rais anayemaliza muda ashinda uchaguzi

**GABORONE,** Botswana

MOKGWEETSI Masisi amerejea madarakani kwa miaka mitano kama Rais wa Botswana baada ya uchaguzi mkuu uliofanyika Jumatano nchini humo.

Chama chake, ambacho kimekuwa madarakani tangu uhuru mwaka 1966, kimeshinda viti vingi bungeni, kwa mujibu wa ofisa wa ngazi ya juu katika Mahakama Kuu nchini Botswana.

"Mimi, Terrence Ranowane ninatangazia Taifa la Botswana na ulimwengu kwamba Dk. Mokgweetsi Eric Keabetswe Masisi amechaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Botswana," alisema katika kwenye televiseni.

Kiongozi mkuu wa upinzani na kiongozi wa muungano wa upinzani wa chama cha Umbrella for Democratic Change (UDC), Duma Boko, alitarajiwa kuleta ushindani mkali kwa Rais Mokgweetsi Masisi.

Mwanzoni mwa wiki, Jeshi la Botswana lilikanusha taarifa kutoka upinzani kwamba, linaegemea upande wa chama tawala, kwa kuwa jeshi linamsafirisha Rais anayemaliza muda wake katika ndege zake katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Jeshi la Botswana lilikataa kutumiwa kama hoja ya uchaguzi, wakati wa kampeni ya uchaguzi uliokuwa na ushindani mkubwa nchini Botswana.

Mwanzoni mwa wiki, Rais Mokgweetsi Masisi mwenye umri wa miaka 58, mtoto wa waziri, mwigizaji wa zamani na mwalimu wa shule ya awali alisema ana imani kuwa Chama chake cha Botswana Democratic Party (BDP), ambacho kipo madarakani tangu Botswana ilipopata uhuru mwaka 1966 kitashinda uchaguzi huo.

Kwenye uchaguzi huo Chama cha BDP kilipata ushindi katika uchaguzi mkuu kwa kupata viti 29, ikiwa sawa na asilimia 51 ya viti vyote vya bunge.

Awali Mwanasheria Mkuu wa Botswana, Terrence Rannowane, alitangaza matokeo hayo kwa kueleza kuwa chama cha BDP, kimeshapata zaidi ya nusu ya viti vya bunge, ingawa kura ziliendelea kuhesabiwa.

Katika uchaguzi huo vyama vya upinzani wa UDC vilipata viti 13 na chama cha BPF kimepata viti vitatu.

Wa-botswana walipiga kura Jumatano kuwachagua wabunge 57 wa Bunge la Taifa na madiwani 490 wa serikali za mitaa na mgombea wa chama kinachoshinda anatajwa kuwa Rais.

Chama cha BDP hivi sasa kinahitajika kufanya mageuzi ya haraka ya uchumi kuokoa uchumi wa taifa hilo, lenye utulivu wa kisiasa barani Afrika kutokana na kudorora kwa uchumi wake katika miaka ya hivi karibuni. **RFI**

# Marekani yafanya msako kiongozi wa IS

**WASHINGTON,** Marekani

MAJESHI ya Marekani yamefanya operesheni ya kumtafuta kiongozi mkimbizi wa wapiganaji wa kikundi cha Islamic State (IS), Abu Bakr al-Baghdadi.

Ikulu ya Marekani imesema kuwa Rais Donald Trump atatoa taarifa kuu lakini haikutoa maelezo zaidi.

Rais Trump awali aliandika ujumbe katika mtandao wa Twitter akisema: "Kitu kikubwa sana kimefanyika!"

Kiongozi huyo wa IS aliwahi kuripotiwa kimakosa kuwa amefariki siku zilizopita. Maofisa wa juu kutoka Jeshi la Marekani walieleza kuwa wanamsaka kiongozi wa kundi la Islamic State katika Mkoa wa Idlib, Kaskazini Mashariki mwa Syria.

Kamanda wa vikosi vya Syria vinavyoongozwa na wapiganaji wa Kikurdi, Mazloum Abdi, jana alisema kuwa operesheni hiyo ya kihistoria ilifaulu kutokana na kazi ya pamoja ya kiintelijensia na Marekani.

**Alijifunza mengi kuhusu jinsi anavyoweza kufanya opereshemi zake kutoka kwa maofisa wa ujasusi wa aliyekuwa Rais wa Iraq Sadam Hussein.**

Ofisa wa Marekani aliliambia Shirika la Habari la Reuters kwamba operesheni ilifanyika lakini hakuweza kuthibitisha madai kuwa Baghdadi aliuawa.

Ikulu ya Marekani haijathibitisha kuwa operesheni hiyo ilifanyika, wala kukanusha matokeo yake.

Operesheni hiyo ilifanywa na vikosi maalumu baada ya kupokea taarifa za uhakika.

Shirika la kutetea haki za binadamu la Syrian Observatory, lenye makao yake nchini Uingereza na ambalo limekuwa likichunguza kundi hilo, linasema mashambulio ya angani yaliwaua watu tisa katika kijiji kimoja mkoani Idlib, ambako makundi yaliyo na ufungamano na Islamic State yanaishi.

Abu Bakr al-Baghdadi, kiongozi mkimbizi wa wapiganaji wa kundi la Islamic State (IS) na uongozi wake wa kidini amewekewa dola za Marekani milioni 25 na serikali ya Marekani kwa mtu yeyote atakayempata.

Ni mzaliwa wa Samarra, nchini Iraq, mwaka 1971, Jina lake kamili ni Ibrahim Awad al-Badri.

Akiwa mfuasi mkuu wa dini ya Kiislamu tangu akiwa mdogo, baadaye alikuwa amefungwa katika kambi moja ya Marekani kwa jina Bucca 2004 kufuatia uvamizi wa Ufaransa na Marekani.

Akiwa katika kambi hiyo aliweka ushirikiano mzuri na wafungwa wengine wakiwamo maofisa wa zamani wa ujasusi nchini Iraq.

Alijifunza mengi kuhusu jinsi anavyoweza kufanya operesheni zake kutoka kwa maofisa wa ujasusi wa aliyekuwa Rais wa Iraq Sadam Hussein.

Usalama wake ni wa hali ya juu kutokana na kiwango cha juu cha wasiwasi alionao. **BBC**



Wananchi wa Iraq wakiwa mitaani wakiandamana. **PICHA: REUTERS**

# Waandamanaji 30 wauawa Iraq

**BAGHDAD,** Iraq

WAANDAMANAJI 30 wameuawa wakati wa wimbi jipya la maandamano ya umma yaliyofanyika dhidi ya serikali nchini Iraq.

Taarifa iliyotolewa na Mjumbe wa Kamisheni ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa, Faisal Abdullah, ilieleza kuwa vifo hivyo vilitokea wakati polisi ilipofyatua risasi za moto na gesi ya machozi kutawanya waandamanaji.

Alisema watu wanane waliuawa kwenye Mji Mkuu Baghdad, wengine 18 katika miji ya Maysan na Dhi Qar, watatu mjini Basra na mtu mmoja aliuawa kwenye Jimbo la Kusini la Muthanna.

Kulingana na Abdullah watu wengine zaidi ya 2,300 walijeruhiwa huku takriban majengo 50 ya serikali na ofisi za vyama vya siasa yaliyochomwa moto katika baadhi ya majimbo nchini Iraq. Marufuku ya kutotoka nje imetangazwa kwenye majimbo ya Dhi Qar, Basra, Muthanna na Wasit.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa waandamanaji walianza kukusanyika kwenye medani ya Tahrir mjini Baghdad baada ya hotuba ya Waziri Mkuu, Adel Abdel-Mahdi, aliyoitoa kwa njia ya televisheni, ambayo alitumia kutoa ahadi ya kufanya mageuzi na mipango ya kufanyia mabadiliko baraza lake la mawaziri wiki ijayo.

"Kutaka serikali iangushwe bila kuwa na njia mbadala ya kikatiba kutaitumbukiza nchi kwenye machafuko," alisema Abdel-Mahdi.

Waandamanaji walipeperusha bendera za Iraq na kuimba kaulimbiu za kutaka kujiuzulu kwa serikali na Bunge.

Pia walitaka kufanyika kwa mageuzi katika sheria za uchaguzi na tume mpya ya uchaguzi iundwe ikiwa na wajumbe walio huru.

Maandamano hayo dhidi ya serikali yanafuatia maandamano kama hayo yaliyofanyika mwanzoni mwa mwezi huu ambayo yalisababisha vifo vya takriban watu 149 na maofisa wanane wa polisi. **DW**

# Kamati kushughulikia changamoto bandarini

**Na Enock Charles**

SERIKALI inatarajia kuunda kamati inayohusisha taasisi 22 zinazotakiwa kufanya kazi na Mamlaka ya Bandari nchini ili kutatua changamoto za wafanyabiashara na wawekezaji katika bandari hiyo na kuboresha huduma za bandari.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Isaac Kamwelwe, amesema serikali inapenda kuona wafanyabiashara na wawekezaji zaidi wakivutiwa na Bandari ya Dar es Salaam na hivyo serikali imejipanga kuondoa vikwazo kwa watumiaji wa bandari.

"Tuna taasisi 22 kwenye bandari ambazo tunatakiwa kushirikiana nazo kwenye ku clear mizigo bandarini, lakini unakuta hazina malengo ya pamoja kwa hiyo itaundwa kamati ya pamoja ili kuwa na malengo ya pamoja," alisema Waziri Kamwelwe.

Taasisi zitakazohusishwa katika kamati hiyo ni pamoja na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Majini (TASAC).

Waziri Kamwelwe alisema pamekuwapo na malalamiko kwa baadhi ya watumiaji wa bandari kuhusu huduma zinazotolewa na bandari hiyo, ikiwamo baadhi ya mizigo kufika ikiwa na upungufu na kutumika kwa muda mrefu mpaka kutolewa kwa mzigo na hivyo kukwamisha juhudi za serikali za kuwaletea maendeleo wananchi.

Alisema ili kuondoa changamoto ni muhimu pakawapo na usimamizi wa pamoja ili kuondoa kero mbalimbali wanazokutana nazo watumiaji wa Bandari ya Dar es Salaam wanaotoka ndani na nje ya mipaka ya Tanzania.

Akizungumza kuhusu uboreshaji wa bandari hiyo amesema serikali imejitahidi kuboresha Bandari ya Dar es Salaam ambayo sasa ina uwezo wa kupokea meli zenye urefu wa zaidi ya mita 260 na zenye uwezo wa kupakia hadi kontena 3,500 kutoka 2,000 za awali.



Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo, akipokea madawati kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha IT wa Benki ya Stanbic Tanzania, Mussa Ally, wilayani Kisarawe juzi. Msaada huo umelenga kuchangia kampeni ya elimu ya Tokomeza Zero. Benki hiyo inaamini ukiwekeza katika elimu ni sawa na kuwekeza katika maendeleo ya taifa. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Madaktari bingwa 15 watua Kigoma

**Na Magreth Magosso,** KIGOMA

ZAIDI ya madaktari bingwa 15 kutoka Jiji la Dar es Salaam wamepokelewa mkoani hapa kwa ajili ya kutoa huduma ya vipimo na tiba ya magonjwa mbalimbali kwa wagonjwa 1,000.

Hayo yalijiri jana kwenye uwanja wa Lake Tanganyika Manispaa ya Kigoma Ujiji wakati wa shughuli ya utoaji huduma mtambukwa kwa walengwa hao, ikiwa ni sehemu ya kushirikiana na serikali katika kutoa huduma ya vipimo na tiba bure kwa wahitaji.

Kaimu Mganga Mkuu wa Kigoma, Hosea William, alisema amepokea madaktari bingwa zaidi ya 15, ambao wana huduma ya upimaji wa magonjwa ya macho, watoto, meno, upasuaji utakaosaidia wahitaji kutambua maradhi yao.

Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Jamii Bora ya Kiislamu, Dk. Abbas Mussa, alifafanua kuwa, wanashirikiana katika suala la utoaji wa huduma ya afya katika kambi mbalimbali walizoshiriki kuwafikia wananchi wa maeneo husika.

"Kigoma tumeanza Oktoba 26 hadi 27, mwaka huu, kwa ajili ya kujua afya za jamii na namna ya kuwaelimisha wagonjwa watakaobainika kuathirika na ugonjwa husika, wanawake wengi wana vidokezo vya saratani ya maziwa na kizazi, magonjwa yasiyoambukizwa ni tishio kwa jamii," alisema Dk. Mussa.

Akizungumzia lengo la taasisi hiyo, Amiri Mkuu wa Taasisi ya JAI, Yahaya Masao, alithibitisha kufungua tawi Kigoma na kuwa mkoa wa 21 nchini kuweka kambi ya upimaji wa afya za magonjwa mbalimbali kama sehemu ya mchango wao kwa umma.

"JAI imeleta madaktari bingwa na kawaida zaidi ya 15, hii ni kambi ya tatu, Zanzibar tulifanya kambi mbili, msingi wetu kusaidia wananchi wenye changamoto ya fedha za matibabu kwa wagonjwa waliotelekezwa hospitali, kuanzia vipimo, dawa, damu, chakula, mavazi na Waislamu wanaofariki hawana familia tunawazika kama ndugu wa kiimani," alisema.

Aliwataka wananchi wa Kigoma kuisaidia taasisi hiyo tawi la Kigoma kifedha, kwa ajili ya kuwasaidia wakazi wenye uhitaji wa kiafya kwa nia ya kurudisha utu wa binadamu katika changamoto za maisha kutokana na mfumo wa kale wa ujamaa kutetereka katika jamii zao.

Naye Katibu wa JAI Kigoma, Ndimugwako Kamana, alibainisha taasisi hiyo inajihusisha na sekta ya afya, mazishi kwa mwislamu asiye na uwezo, wagonjwa wasiomudu gharama za zilizo ndani ya uwezo wao, tangu wazindue tawi Septemba 9 hadi 26 Oktoba, mwaka huu wagonjwa 10 wamenufaika na taasisi hiyo na kiasi cha Sh. 500,000 zimetumika.

Baadhi ya wahitaji wa huduma hiyo Sara Rafael na Raya Katanga kwa nyakati tofauti, wameipongeza taasisi hiyo kwa kubaini changamoto ya kipato duni kwa wananchi wengi ni kikwazo cha kushindwa kuonana na madaktari bingwa wa magonjwa husika na kuomba siku ziongezwe kwa wahitaji.

## Mafuriko yaua 13

INATOKA UK. 2

Phillis Nyimbi, alitembelea maeneo yaliyoathirika kwa mvua hiyo na kufika kwenye msiba wa mtoto Yohana na kuipa pole familia hiyo.

"Nyumba nyingi zilizoathirika ni zile zilizoezekwa na kuwekewa mawe juu ya bati jambo ambalo ni hatari sana, niwaombe wananchi kuachana na tabia hiyo na mjikite katika kujenga nyumba zilizo imara na bora zaidi," alisema Dk. Nyimbi na kuongeza:

"Nikiangalia nyumba zilizoathirika ni zile zilizo maeneo ya wazi ambako hakuna miti na ndio chanzo kikubwa cha nyumba nyingi kuanguka na kuezuliwa mvua zinapoanza kunyesha na kuambatana na upepo mkali," alisema Nyimbi.

Aidha, aliwaangiza wataalamu wa mazingira na misitu wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, kwenda katika kata zote 18 za wilaya hiyo ili kutoa elimu ya ujenzi wa nyumba bora na kupanda miti ya matunda na kivuli, ili kuepukana na athari za mvua na upepo.

Diwani wa Lwanima, Reuben Nzari, aliomba serikali kuzisaidia kaya zilizoathirika kwa mvua hiyo, ili wasiathirike na majanga mengine, kwani mvua zinaendelea kunyesha.

**TANGA**

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Edward Bukombe, akizungumza na waandishi wa habari, alieleza kuwa hadi jana watu 11 walikuwa wamefariki kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha mkoani humo.

Alisema barabara ya Segera-Arusha iliyokuwa imefungwa kutokana na maji kujaa, imeshafunguliwa na magari yameanza kupita.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Handeni Vijijini, Mustafa Beleko, akizungumza na Nipashe, alisema watu 51 waliokolewa jana wakiwa juu ya miti baada ya kuzingirwa na maji.

"Tumefanikiwa kuwaokoa wananchi waliokuwa wamekwama juu ya miti, watoto walikuwa 29, wanaume 13 na wanawake tisa, wote ni wafugaji katika kijiji hicho," alisema Beleko.

Alisema miundombinu hasa barabara imekuwa haipitiki kwa baadhi ya vijiji ikiwamo kijiji cha Nkale na Kwamkono, huku barabara ya Korogwe-Handeni ikiwa imefungwa mpaka itakapofanyiwa ukarabati mkubwa.

Wakizungumza na Nipashe kijijini hapo, wananchi hao walisema maji yalianza kuwazunguka saa 2:30 usiku wa kuamkia jana na walipotaka kujiokoa walishindwa kutokana na kuwa na watoto wadogo.

Idd Athumani, mmoja wa waliokolewa, alisema baada ya kuona maji yamezunguka eneo lote wanaloishi alianza kuwabeba watoto na kuwapandisha juu ya mti uliokuwa karibu, huku akishuhudia mifugo na vyombo vikienda na maji.

Alisema baada ya kuanza kuwapandisha watoto juu ya mti, alianza kuishiwa nguvu kutokana na ongezeko la maji.

Athumani, ambaye anawatoto wanne, alisema wakati akiwa juu ya mti na familia yake ghafla ilianza kusikia yowe za nyumba za majirani wakihitaji msaada wa kuokolewa.

"Nililazimika kupiga mbizi kwenda kuwaokoa hali ilizidi kuwa mbaya zaidi kutokana na wingi wa maji. Ni tukio ambalo sitoweza kulisahau na pia siamini kama nimeweza kuokoa watu wengi," alisema Athumani.

**Imeandikwa na Boniface Gideon, Handeni na Rose Jacob, Mwanza**

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MCHANGANYIKO

**2 ACRE YARD FOR RENT**

Facing New Julius Nyerere International Airport.
Call: +255 754 375 967.
Email: gold@goldtz.net

## VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA LINAUZWA**

Shamba la Ekari 13 linauzwa liko Mlandizi barabara iendayo Bagamoyo, lina miti ya matunda inayozaa, lina umeme. Lina maji ya DAWASCO na maji ni matamu. Pia kuna kisima kirefu. Kwa mawasiliano piga simu namba 0655 099825 / 0767 237404 / 0715 237404.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA

BEI NAFUU SANA


## KUPOTEA KWA CHETI



115481302

**EVA .P. SHUMA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0248-0030** kilichotolewa na MARIAN GIRLS SEKONDARI mwaka 2011. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **UD/RB/2114/2019.**

## KUPOTEA KWA VYETI



115481402

**JESSE RICHARD** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S1253/0057** kilichotolewa na ULAYA SEKONDARI mwaka 2005. Cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P0631/0014** kilichotolewa na UMOJA SEKONDARI mwaka 2017. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba P0132/0574 kilichotolewa na MILAMBO SEKONDARI mwaka 2019. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/412364/2019.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA MADAI NO. 382 MWAKA 2019**

**JAPHET CIDRECK GAMA.......................MAREHEMU**

**DHIDI YA**

**JUDITH ANN GAMA .....................MUOMBAJI**

**KUITWA SHAURINI**

**Kwa: 1. JUDITH ANN GAMA**

Kwa kuwa mdai aliyetajwa hapo juu, amefungua shauri la madai dhidi yako, shauri ambalo maelezo yake yameelezwa katika nakala za hati za madai zinapatikana katika Mahakama hii kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Mahakama hii wewe mwenyewe au wakili au mwakilishi wako anayeruhusiwa kisheria, siku ya tarehe 14/11/2019 saa tatu kamili (3:00) asubuhi mbele ya Mheshimiwa Jaji J. A. De-Mello, kujibu madai hayo dhidi yako. Unaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo unatarajia kuvitumia katika utetezi wako siku hiyo.

**ANGALIA:** Kama usipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kuwa umepokea taarifa hii ya kuitwa shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wako.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Chapa ya Mahakama leo tarehe 01 mwezi 10, 2019.

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU**
**KANDA YA DAR ES SALAAM.**

115479902

## KUPOTEA KWA KADI

CREN TRANSPORT AGENT CO. LIMITED anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TRAILER yenye usajili wa namba T 309 DDM iliyotolewa na Mamlaka ya mapato Tanzania.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
DAR/CEN/RB/407353/2019

xxxxxxx

## KUPOTEA KWA KADI

CREN TRANSPORT AGENT CO. LIMITED anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TRAILER yenye usajili wa namba T 306 DDM iliyotolewa na Mamlaka ya mapato Tanzania.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
DAR/CEN/RB/407353/2019

xxxxxxx

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA JUDICIARY

In the RM/S COURT OF TANGA
AT TANGA
CIVIL CASE NO. 8 OF 2019
HAMOUD SALIM HAMOUD...........................PLAINTIFF (s)
VERSUS

**1. Sima mototo Trans ltd defendant (s)**
**2.Juma ally Mbwana**

**SUMMONS TO FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFFENCE**

To: Juma ally mbwana of
Duga mwembeni area, Tanga
WHEREAS the above named plaintiff(s) has /have instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in annexed copy of the plaint

**YOU ARE HEREBY NOTIFIED** that you must file your **WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE** in duplicate within twenty one (21) days of services of this notice upon you if there is more than one plaintiffs additional copies of you written statement of defence must be filed sufficient for service on each of the plaintiffs if there are more defendants than one and the defence is not joint defence, you must fill sufficient copies for services on each of the other defendants

**AND TAKE NOTICE** that if you default in filling the written statement of defence within the time specified, the court may pronounce judgment against you.

**TAKE FURTHER NOTICE** that the case also has been fixed for order before Honorable **E.F MCHAURU PRM.**

Resident Magistrate on the 7th day of Nov 2019 at 08:30.
**GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE** Court this 25th October 2019.

XXXXXX


**Uza,**
**Chenye Thamani**
**Kubwa Kwa Kutangaza**
**Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0767 223311**

**NJOO UTANGAZE**

**SANA**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku


Tupigie
0767 223 311

Nipashe


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# MESSI ALITAKA KOMBE LA DUNIA AKILIA NA MUDA




**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi amesisitiza angeweza kubadili chochote kwenye maisha yake ya soka ili kushinda Kombe la Dunia.

Kukosekana kwa mataji makubwa ya kimataifa kunabakia kuwa pigo kwa nyota huyo wa Barcelona.

Alitajwa kuwa mchezaji bora wa michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2014, ambapo Argentina walifungwa bao 1-0 na Ujerumani kwenye muda wa zaida katika fainali hiyo.

Kombe la Dunia lililopita nchini Urusi walitolewa na Ufaransa kwa kufungwa mabao 4-3 katika hatua ya mtoano wa timu 16-bora.

Messi atakuwa na umri wa miaka 35, wakati wa michuano ya Kombe la Dunia nchini Qatar 2022 na katika mahojiano yake na TyC Sports, akakubali kwamba, muda wa yeye kulibeba taji hilo ni kama umepita.

"Ningependa kuwa bingwa wa dunia," alisema. "Lakini nafikiri nisingeweza kubadilisha chochote nilichopata kwenye maisha yangu ya soka.

"Hiki ndicho kinachonigusa mimi, kile ambacho Mungu amenipa."

Messi alikuwa nahodha wa Argentina iliyotinga nusu fainali ya Copa America mapema mwaka huu, na wakafungwa na wenyeji Brazil. Katika michuano hiyo mara mbili mfululizo, Argentina ilifungwa kwenye fainali kwa mikwaju ya penalti na Chile.

# Bayern yakataa kumuuza Muller

**MUNICH,** Ujerumani

MKURUGENZI wa Soka wa Bayern Munich, Hasan Salihamidzic, amekanusha taarifa kwamba, Thomas Muller ataondoka klabuni hapo wakati wa dirisha dogo la usajili Januari.

Muller amekuwa akihusishwa na mpango wa kutua kwa miamba wa Ligi Kuu ya England, Manchester United na kule kwa wakali wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Inter tangu alipobainisha kwamba ataangalia majaliwa yake hapo Bayern.

Akiwa kwa sasa hapati nafasi ya kucheza mara kwa mara chini ya kocha, Niko Kovac, nyota huyo wa timu ya Taifa ya Ujerumani, ameanza katika mechi mbili zilizopita ikiwamo ya juzi, Jumamosi ya ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Union Berlin.

Huku uvumi huo ukizidi kuenea kuhusu majaliwa ya Muller, Salihamidzic ameiambia Sky Sport: "Tuna majeruhi wa muda mrefu, na unajaribu kutushawishi kutaka kumuuza mtu.

"Hiyo ni kama hadithi inayoandikwa kila wakati. Hatufikirii kuhusu kuuza wachezaji kwa sasa, tunamhitaji kila mchezaji aliyepo kwenye kikosi chetu."

Na baada ya mchezo huo ambao mabao yake yalifungwa na Benjamin Pavard na Robert Lewandowski, Muller alitania kuhusu uvumi huo.

"Nimesikia kwamba, naondoka, nafikiri mimi bado ni mchezaji wa Bayern, mengine silazimika kuyajibu," alisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30.





# Bruyne aionya Liver mbio za ubingwa EPL

**MANCHESTER,** England

KEVIN De Bruyne amewakumbusha vinara wa Ligi Kuu ya England, Liverpool kwamba, bado kuna safari ndefu msimu huu baada ya kufunga bao kwenye ushindi wa 3-0 dhidi ya Aston Villa na kuisaidia Manchester City kupunguza pengo la pointi hadi tatu kwenye msimamo.

Raheem Sterling alifunga bao la uongozi kwa City kwenye mchezo huo uliopigwa pale kwenye dimba la Etihad kabla ya De Bruyne kufunga la pili kwa kumzidi akili golikipa, Tom Heaton.

Ilkay Gundogan aliongeza la tatu kwenye mchezo huo na De Bruyne atabanaisha kwamba, City walikuwa na matatizo kwenye kipindi cha kwanza, lakini waliyamaliza haraka.

"Nafikiri kipindi cha kwanza tulikuwa na matatizo, hatukuwa kwenye ubora wetu, na timu haikuwa na muunganiko mzuri," alisema De Bruyne akiiambia BT Sport.

"Gabi (Gabriel Jesus) alikuwa na nafasi kadhaa za kuiwezesha timu kuwa mbele na kipindi cha pili alianza vizuri zaidi.

"Katika kipindi cha kwanza tulikuwa na nafasi nyingi za kufunga, lakini hatukuzitumia vizuri ingawa tulicheza kwa kujiamini.

"Lakini jambo la muhimu ni kwamba, tulipata ushindi na sasa tumewakaribia Liverpool na msimu bado mrefu na tuna safari ndefu ya kwenda."

Ushindi wa Man City umekuja wiki tatu baada ya kupata kipigo cha kushtukiza cha mabao 2-0 kutoka kwa Wolves, na hivyo kuipa nafasi Liverpool ya kujiweka sawa zaidi kwenye mbio za ubingwa.

Na sasa De Bruyne anaona kwamba, safari bado ni ndefu kwenye mbio za ubingwa huo.

# Lampard akunwa na kiwango cha Pulisic

**LONDON,** England

CHRISTIAN Pulisic "ameonyesha kiwango bora" kwa kufunga mabao matatu 'hat-trick' wakati Chelsea ikiibuka na ushindi wa 4-2 dhidi ya Burnley, kwa mujibu wa kocha, Frank Lampard.

Pulisic ambaye ni mchezaji wa kimataifa wa Marekani, alifunga kwa mguu wa kushoto, mguu wa kulia na kwa kichwa kuipa Chelsea uongozi wa mabao matatu katika mchezo huo wa Jumamosi uliopigwa kwenye dimba la Turf Moor.

Willian aliongeza bao la nne kabla ya Jay Rodriguez na Dwight McNeil kuifungia Burnley mabao mawili katika dakika tano za mwisho, lakini Blues hao wakapata ushindi wao wa saba kwenye mashindano yote.

Lampard alimsifia Pulisic baada ya mchezo huo kwa kuibuka shujaa wa kupiga 'hat-trick' na anajiamini kwamba mchezaji huyo ameshapata uzoefu wa kufunga kwenye soka la Uingereza.

"Kwa namna alivyokuwa anajifua kwa wiki kadhaa zilizopita matokeo yake yameonekana," alisema Lampard akiwaambia waandishi wa habari.

"Kwa uhakika kabisa nimeridhishwa na kiwango chake, na hicho ndio tunachokitaka kutoka kwa mchezaji. Alionyesha kiwango chake bora kabisa."

Pulisic huo ulikuwa ni mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu kuanza tangu Agosti na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, sasa anaweza kuwa kwenye kikosi cha kwanza cha Chelsea.





# SIMEONE ATAKA UMOJA ATLETICO

**MADRID,** Hispania

DIEGO Simeone amewataka wachezaji wake kuonyesha umoja na kuwa na mweleko mmoja baada ya Atletico Madrid kupata ushindi wake dhidi ya Athletic Bilbao kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga.

Atletico ilikumbwa na sare tatu mfululizo kwenye ligi kabla ya juzi Jumamosi kupata ushindi wa mabao 2-0, shukrani kwa mabao ya Saul Niguez na Alvaro Morata.

Baada ya mchezo huo wa tatu nyumbani, Simeone aliwashukuru wachezaji wake na kuwataka kuwa na umoja pamoja na utulivu.

"Tunatakiwa kuwa wamoja daima," alisema baada ya mchezo huo akiwaambia waandishi wa habari.

"Sisi ni timu mpya iliyojaa wachezaji wapya. Leo kwa mfano, nyuma tulikuwa na wachezaji wapya tuliowasajili.

"Tunajua malengo yetu na kile ambacho mashabiki, wakurugenzi, makocha na wachezaji wanachokitaka, hivyo lazima tupambane."

Aliongeza: "Mashabiki bado wana hamasa kubwa na kikosi chetu, ni watu bora zaidi wanaotuzunguka."

# Majeruhi Inter Milan wamtia hofu Conte

**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte amesema anahofia kuhusu majeruhi kukiathiriki kikosi chake cha Inter kwa wiki zinazokuja baada ya timu yake kuambulia sare ya kufungana mabao 2-2 dhidi ya Parma juzi, Jumamosi.

Kwadwo Asamoah na Stefan de Vrij waliachwa kwenye kikosi cha Conte pale kwenye dimba la San Siro, ambapo mabao yake yalipatikana katika kila kipindi kupitia kwa Antonio Candreva na Romelu Lukaku kuwasaidia Nerazzurri hao kupata pointi moja.


Matokeo hayo yameiacha Inter pointi moja nyuma ya vinara wa Serie A, Juventus, ambao walitoka sare ya kufungana 1-1 na Lecce mapema Jumamosi, na Conte ameelezea wasiwasi wake kuhusu majeruhi kwenye kikosi chake.

Inter itacheza mechi zake tatu zijazo ugenini dhidi ya Brescia, Bologna na Borussia Dortmund ndani ya siku nane, na Conte ameiambia Sky Sports: "Huu ulikuwa ni mchezo wetu wa tatu ndani ya siku sita. Tunacheza zaidi au kidogo na tutakuwa na wakati mgumu.

"Hatujawa watulivu kuhusu hili. Tuna mechi nyingine nne kwa muda mfupi ujao. "De Vrij alikuwa na matatizo na Asamoah anasumbuliwa na goti. Inakuwa ni vigumu kucheza kwenye mashindano mawili na kikosi ambacho kimepungua."



# DONDOO Z
## MAGAZETI YA




# 'OZIL BENCHI ARSENAL NI UAMUZI WA KLABU'

### ●●● Hapa tuna makubaliano ya kimkakati na klabu na timu, najua mashabiki...

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery amesisitiza kwamba, uamuzi wa kutomtumia Mesut Ozil unaungwa mkono na uongozi wote wa klabu hiyo.

**Ozil hajaichezea Arsenal mechi tano zilizopita kabla ya jana dhidi ya Crystal Palace, huku kocha Emery akitoa maelezo machache juu ya uamuzi wake wa kutomtumia mchezaji huyo anayelipwa mshahara mkubwa zaidi katika historia ya klabu hiyo.**

Kiungo huyo raia wa Ujerumani alituma mara kadhaa ujumbe kwenye mitandao ya kijamii hivi karibuni akisisitiza kwamba, anataka kubakia klabuni hapo na atajifua kwa bidii ili kupata namba.

Pia kumekuwa na kundi la mashabiki wanaomuunga mkono mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, wanaova fulana inayoonyesha kikosi cha 'Washika Bunduki' hao kimekosa ubunifu dimbani.

Lakini Emery amebainisha kwamba, kumekuwa na mazungumzo na viongozi wa juu wa klabu hiyo ambao wamekubali mpango wa kumtema Ozil kikosini.

"Hapa, tuna makubaliano ya kimkakati na klabu na timu," alisema wakati alipoulizwa kama kuna presha yoyote kutoka juu inayomtaka kumweka benchi Ozil. "Kwa sababu jambo muhimu zaidi ni klabu, timu inatafuta kiwango chake. Awali wote tulikuwa tunazungumza kati yetu kuchukua maamuzi haya.

"Najua mashabiki wote wanataka kujua kitu, lakini sasa sio wakati sahihi kwao. Nafikiri sio wakati wa kumzungumzia yeye."

Mmoja wa wachezaji watano ambao walikuwa wanamburuza nyota huyo kwenye namba 10 alikuwa Lucas Torreira, kiungo mkabaji ambaye amekuwa na wakati mgumu wa kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara chini ya Emery msimu huu.

Akiwa amemshuhudia mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay akicheza vizuri wakati wa ushindi dhidi ya Vitoria, Emery ameelezea kwamba Torreira anaweza kuwa chaguo lake la kuongoza mashambulizi.

"Nilikuwa nazungumza naye kuhusu nafasi bora kwake ili kuisaidia timu," amesema kocha huyo.

"Inategemea na mfumo wa timu. Msimu uliopita nafasi yake bora zaidi ilikuwa ni kucheza kama kiungo mchezeshaji pamoja na (Granit) Xhaka au Matteo (Guendouzi). "Mwaka huu tumekuwa tukicheza kwa mtindo wa kumtumia kiungo mmoja, na anaweza kucheza kwa ubora zaidi kwenye eneo la hatari na kufunga mabao ni mchezaji mwenye akili na ana kasi.

"Halafu wakati tukiandaa timu kucheza kwa kasi ya kushambulia, kwa upande wetu yeye ni muhimu kwani ni mchezaji mwenye akili akiwa sambamba na viungo wawili."

## ZISIKUPITE

### BALE TATIZO MAJERUHI UTD

MANCHESTER United imekuwa ikiweka kando nafasi ya kumsajili mshambuliaji wa Real Madrid, Gareth Bale, 31, kwa sababu ya rekodi ya majeraha ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Wales. ***(Mirror)***

### JESUS KUIGHARIMU BAYERN

MANCHESTER City itaweka dau la pauni milioni 100 kwa mshambuliaji wa kimataifa wa Brazil, Gabriel Jesus, 22, kutokana na jaribio la Bayern Munich kuvutiwa naye. ***(Sun)***

### REAL KUMREJESHA CEBALLOS

REAL Madrid inajiandaa kutolea nje matumaini ya Arsenal kumsajili jumla kiungo wa kimataifa wa Hispania, Dani Ceballos, 23, kwa kumrudisha msimu ujao kutoka katika klabu hiyo anayoichezea kwa mkopo. ***(AS, via Mail)***

### SON AZIVUTIA NAPOLI, JUVE

KIPENZI cha Tottenham, Mkorea Kusini Son Heung-min, 27, amekuwa akifukuziwa na Juventus na Napoli. ***(Express)***

### LIVERPOOL YAMKERA GOMEZ

BEKI wa Liverpool, Joe Gomez amezidi kuchanganyikiwa kuhusu nafasi chache ya kucheza msimu huu wakati huu Tottenham na Arsenal zikivutiwa na beki huyo wa England. ***(90min)***

### PHILLIPS NDANI RADA ZA UTD

MANCHESTER United inamfuatilia kiungo wa Leeds, Kalvin Phillips, na kocha msaidizi Mike Phelan alimtazama mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 akicheza dhidi ya Birmingham wiki moja iliyopita. ***(Sun)***

### INTER KUUZIWA RAKITIC

BARCELONA imefanya mazungumzo na Inter Milan kuhusu uwezekano wa kuwauzia nyota wa kimataifa wa Croatia, kiungo Ivan Rakitic, 31. ***(Sport)***

### MATHESON AZIVUTIA UTD, CITY

MANCHESTER United na Manchester City zipo katika vita ya kuwania saini ya beki kinda wa Rochdale na England U-18, Luke Matheson, 17. ***(Star)***

### NAPOLI KUMGOMEA RUIZ

NAPOLI haivutiwi kumuuza kiungo anayewindwa na Manchester City, Fabian Ruiz, 23, katika nyakati za hivi karibuni. ***(Gazzetta dello Sport, via Inside Futbol)***

### DALBERT AWEKWA SOKONI

INTER Milan imetangaza nia ya kumuuza kwa dau la euro milioni 20 beki wao, Mbrazil Dalbert, 26, ambaye anaichezea Fiorentina kwa mkataba wa mkopo wa muda mrefu wakati huu klabu hiyo ikiwa haina kipengele kinachoiruhusu kumnunua jumla. ***(Calciomercato)***

### HAVERTZ, MULLER WANUKIA UTD

MAKAMU Mwenyekiti wa Manchester United, Ed Woodward amekubali dau la pauni milioni 125 kwa wachezaji wawili kutoka Bundesliga, kiungo wa Bayer Leverkusen, Mjerumani Kai Havertz, 20, na mshambuliaji wa Bayern Munich, Thomas Muller, 30. ***(Mirror)***

HABARI MICHEZO

## Gari SportPesa bado siku mbili

**Na Mwandishi Wetu**

ZIKIWA zimesalia siku mbili tu kabla ya Kampuni ya Michezo na Burudani ya SportPesa kuwazawadia watumiaji wa mtandao wa Tigo kupitia huduma ya TigoPesa, zawadi ya gari jipya aina ya Renault Kwid yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 23 za Kitanzania, simu kibao zimeendelea kutolewa kwa washindi.

SportPesa kwa kushirikiana na Kampuni ya mitandao ya simu ya Tigo wanaoendesha promosheni ijulikanayo kama Faidika na Jero ikiwa na lengo la kuwazawadia wateja wao zawadi mbalimbali ikiwamo smartphone (simu janja) na mwisho wa siku mshindi kuondoka na gari.

Droo ya mwisho ya gari itachezeshwa keshokutwa Jumatano Oktoba 30, mwaka huu, ambapo watatafutwa washindi saba wa simu aina ya Samsung A10s pamoja na gari likiwa linasoma kilometa sifuri.

Akizungumzia promosheni hiyo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa, Tarimba Abbas alisema: "Zimebaki siku mbili mpaka kumalizika kwa promosheni hii na ningependa kuwahamasisha Watanzania washiriki vilivyo ili kuhakikisha wanatumia nafasi vizuri kujishindia zawadi zilizopo.

## Mndeme atoa neno Kunyumba Marathon

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

WAKAZI wa Mkoa wa Ruvuma wamehimizwa kuona umuhimu wa kujikita zaidi katika michezo ikiwamo mchezo wa riadha ambao ulikuwa ni zaidi ya burudani wakati wa mashindano ya Kunyumba Marathon yaliyofanyika mwishoni mwa wiki.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme ambaye alikuwa mgeni rasmi wa Kunyumba Marathon yaliyofanyika mjini Songea na washiriki zaidi ya 200 kujitokeza.

Katika mashindano hayo yaliyoandaliwa na taasisi isiyo ya Kisekali ya VAYOEVENTS ya mjini Songea inayojishughulisha na uandaaji wa matamasha mbalimbali yakiwamo ya michezo, utamaduni, utalii na jamii kwa ujumla ambayo yalifanyika Uwanja wa Majimaji, wanariadha walikimbia umbali kilometa 21, kilometa 10 na kilometa tano. Mndeme alisema ni vema wananchi wakatambua kuwa riadha ni sawa na michezo mingine hivyo kuona umuhimu kuchangamkia marathon kwani kwa namna moja au nyingine inawajengea uwezo washiriki kuwa na afya huku pia ikiwaepushwa na mambo mengi ikiwamo ulevi na anasa.

Aidha, Mndeme alikabidhi zawadi kwa washindi mbalimbali ambapo mshindi wa kwanza wa mbio za kilometa 21, Mohamed Dule alikabidhiwa Sh. 300,000 huku mshindi wa pili France Komba akilamba Sh. 200,000 na Ostin Kinyunyu na John Haule waliibuka na Sh. 100,000 kila mmoja.

# MBAO, MBEYA CITY HAPATOSHI KIRUMBA

**Na Somoe Ng'itu,** MWANZA

MBIO za kuwania taji la Ligi Kuu Tanzania Bara zinatarajiwa kuendelea tena leo kwa Mbao FC kuwakaribisha Mbeya City kutoka Mbeya katika mchezo utakaochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini hapa.

**Timu zote zitashuka uwanjani leo zikiwa na kumbukumbu ya kufungwa mechi zao zilizopita, Mbao FC wakipoteza kwa bao 1-0 dhidi ya Yanga katika Uwanja wa CCM Kirumba wakati Mbeya City ikiwa nyumbani ilipokea kichapo cha mabao 4-1 kutoka kwa Kagera Sugar.**

Akizungumza na gazeti hili jijini hapa, Kocha Mkuu wa Mbao FC, Hemed Morocco, alisema wamejiandaa vizuri kwa mchezo huo na wamejipanga kutorudia makosa waliyoyafanya katika mchezo uliopita.

Morocco alisema wanajua mchezo huo utakuwa mgumu kwa sababu wapinzani wao Mbeya City, nao wametoka kupoteza mchezo uliopita, hivyo wataingia uwanjani wakiwa makini zaidi.

"Tuko tayari kwa mechi ya kesho (leo), tunajua itakuwa ngumu, kwa kifupi ligi yote ni ngumu na ina ushindani, hakuna mechi rahisi, mabao si mengi sana, isipokuwa mchezo wa Mbeya City uliopita ndio wamefungwa mabao mengi, ila si kwamba ni wepesi, hapana, hatutawadharau," alisema Morocco.

Alimtaja Shiro Mkwama, ndiye mchezaji pekee ambaye ni majeruhi katika kikosi chake ambacho kimedhamiria kufanya vizuri katika msimu huu wa Ligi Kuu ambayo hutoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Naye Kocha Mkuu wa Mbeya City, Juma Mwambusi, alisema wako tayari kwa mchezo wa leo, na wataingia uwanjani wakiwa wamesahau matokeo ya mchezo uliopita.

"Akili na mawazo yetu yako kwa ajili ya mechi ya Mbao, tumejipanga kufanya vizuri, hatukufurahishwa na mchezo uliopita, sasa tutaingia kupambana ili kupata pointi tatu, ligi hii haina nyumbani wala ugenini, kokote mtu unaweza kushinda, naamini tutatimiza malengo ya timu yetu," Mwambusi alisema.

Katika msimamo wa ligi hiyo inayoongozwa na mabingwa watetezi Simba, Mbao FC wenye pointi saba wakiwa wameshuka dimbani mara saba wako katika nafasi ya 15 wakati Mbeya City ina alama nne na imecheza michezo sita, huku kwenye msimamo ikiwa katika nafasi ya 19.




Mshindi wa wiki iliyopita wa Promosheni ya Faidika na Jero, Ramadhani Tindwa (katikati) mkazi wa Mbagala Dar es Salaam akikabidhiwa zawadi ya simu janja aina ya Samsung A10s na Msemaji Mkuu wa Simba/ Balozi wa SportPesa, Haji Manara, wakati wa kuwatangaza washindi wa wiki hii. Kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Kidigitali Tigo, Ikunda Ngowi. Makabidhiano hayo yalifanyika katika Ofisi za SportPesa jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

# ZFF, TFF kukutana kuyamaliza

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Visiwani Zanzibar (ZFF), limesema litaendeleza ushirikiano uliopo na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) ili kufikia malengo ya pamoja ya kukuza soka kwa pande zote mbili.

Awali ZFF ilitoka taarifa ya kusitisha uhusiano wake na TFF kwa sababu mbalimbali ikiwamo kutofikia muafaka wa TFF kutolipa malipo ya wachezaji waliohamishwa kutoka klabu za Zanzibar kwenda kucheza klabu za Tanzania Bara pamoja na kutopata ruzuku inayotoka Fifa.

Hayo yameelezwa na Msemaji wa Rais wa ZFF, Adam Natepe wakati akizungumza na waandishi wa habari za michezo ambapo alisema wameamua kuendeleza ushirikiano huo baada ya pande zote mbili kutarajia kukutana kuzungumzia matatizo hayo.

Alisema ZFF na TFF wanatarajia kukutana hivi karibuni ili kujadili tatizo lililopo kabla ya kufikia muafaka wa pamoja katika mustakabali wa kukuza soka kwa pande zote mbili.

Alisema ZFF haina tatizo na TFF ila kilichopo hivi sasa kinatokana na changamoto ya kifedha inayolikumba shirikisho hilo hali inayosababisha hata kushindwa kuisimamia ligi yake vizuri pamoja na kuziandaa timu zake za taifa ambazo zinashiriki michuano ya Cecafa.

"Hatuna mgogoro na wenzetu sote ni wamoja hakuna Tanzania kama hakuna Zanzibar na sawa TFF na ZFF, timu ambazo wachezaji wao wamehamishwa Bara mara nyingi wanafika ofisini kuja kudai fedha asilimia zao, lakini pia bado kuna tatizo la fedha zinazotoka Fifa hili ni tatizo la muda mrefu sana licha ya kutumia njia zinazopaswa kutumika ikiwamo kuandika barua na hata vikao, lakini bado tatizo lipo," alisema.

Hata hivyo, alisema madai ya ZFF hayahusiani na masuala ya kisiasa juu ya Muungano ulipo wa Tanzania Bara na Zanzibar bali wao wapo katika masuala ya michezo na namna gani pande zote mbili zitanufaika.

Michezo

Jumatatu Oktoba 28, 2019

Nipashe



'Ozil benchi Arsenal ni uamuzi wa klabu'

UKURASA 30

PAMBANA...



Kiungo wa Aston Villa, Mbazil Douglas Luiz akipambana na Kipa wa Manchester City, Ederson, baada ya kuwatoka mabeki wa timu hiyo kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa kwenye dimba la Etihad juzi na wenyeji kushinda 3-0. **PICHA: MTANDAO**

## Simba inajichapia, Azam chali tena

**Na Adam Fungamwango**

BAO pekee lililofungwa na Miraji Athumani kwenye dakika ya 42, limeifanya timu ya Simba kuichapa Singida United 1-0 kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha wakati Azam ikipotea dhidi ya Ruvu Shooting.

Mzamiru Yassin, kiungo aliye kwenye kiwango cha juu hivi sasa, alichukua mpira katikati ya uwanja kabla ya kutoa pasi ndefu kwa mfungaji ambaye akiwa amezongwa na mabeki wawili wa Singida United aliachia kombora kali la mguu wa kushoto na mpira ukajaa wavuni.Miraji anatimiza bao la nne msimu huu akiwa na timu hiyo iliyomsajili kutoka Lipuli ya Iringa.

Kwa ushindi huo Simba imeendeleza rekodi yake ya kushinda kwa asilimia 100, ikishinda mechi zote sita ilizocheza, ikianza kwa kuichapa JKT Tanzania mabao 3-1, Mtibwa Sugar 2-1, Kagera Sugar 3-0, ikaitandika Biashara United ya Mara 2-0, ikashinda bao 1-0 dhidi ya Azam FC, kabla ya mechi ya jana kupata ushindi kama huo, hivyo inaongoza ligi ikiwa na pointi 18.

Mechi nyingine Azam FC imechapwa kwa mara nyingine na Ruvu Shooting bao 1-0 kwenye Uwanja wa Mabatini baada ya kupoteza kwa bao 1-0 dhidi ya Simba mechi iliyopita.

Mwadui ikiwa Mwadui Complex imeichapa JKT Tanzania mabao 2-0, Lipuli ikipoteza nyumbani kwa bao 1-0 dhidi ya Coastal Union na Biashara United ikiichapa Namungo FC bao 1-0 kwenye Uwanja wa Karume mjini Mara.

# Upepo wa kisulisuli wageukia Yanga

**Na Somoe Ng'itu,** MWANZA

### ●●● Mashabiki waimba Zahera atimuliwe wakati kasi ya Pyramids ikiwashinda, Tshishimbi amuinua Lipumba...

MAMBO magumu! Hivyo ndivyo unavyoweza kusema baada ya upepo wa kisulisuli uliokuwa ukitarajiwa kupeperusha Pyramids FC ya Misri katika Uwanja wa CCM Kirumba jijini mwanza, jana kugeuka ghafla na kuvuma langoni mwa Yanga kabla ya kuidondosha mara mbili kwenye mechi ya awali ya mchujo ya kuwania kushiriki hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika.

**Katika mechi hiyo iliyoanza kwa kasi huku Pyramids wakionekana kutafuta bao la mapema, Yanga ilishindwa kuhimili vishindo na kujikuta ikikubali kipigo cha mabao 2-1, hivyo kujiweka katika mazingira magumu ya kutinga hatua ya makundi watakaporudiana wiki mbili zijazo.**

Ili sasa iweze kutinga hatua ya makundi, Yanga inatakiwa kupata ushindi wa kuanzia mabao 2-0, katika mchezo wa marudiano utakaochezwa Novemba 3, mwaka huu nchini Misri.

Bao la kwanza la wageni hao lilifungwa dakika ya 42 na Eric Traore baada ya kumalizia gongeana nzuri zilizofanyika ndani ya eneo la 18 la wawakilishi hao pekee wa Tanzania waliobakia kwenye mashindano ya kimataifa.

Upepo uliendelea kuvuma langoni mwa Yanga na dakika ya 63, Omar Gaber aliifungia Pyramids bao la pili baada ya kumalizia kazi nzuri iliyofanywa na Mohammed Farouq na kuwafanya baadhi ya mashabiki wa Yanga kuanza kuondoka uwanjani hapa mapema kwa kukata tamaa ya kuendelea kuishangilia timu yao.

Papy Tshishimbi alimnyanyua Mwenyekiti wa CUF, Ibrahim Lipumba kushangilia baada kuifungia Yanga bao kufuatia mabeki wa Pyramids kupoteana huku wakionekana kutegea wakijua mfungaji atatoa pasi na badala yake alipiga moja kwa moja wavuni.

Hata hivyo, Yanga ilimaliza mchezo huo ikiwa pungufu kutokana na beki wake wa kati, Kelvin Yondani, kuonyeshwa kadi nyekundu, ikiwa ni ya pili ya njano baada ya kumchezea faulo Gaber wa Pyramids ambaye alikuwa anaelekea kufunga dakika za nyongeza.

Pyramids inayofundishwa na kocha wa zamani wa timu ya Taifa ya Uganda (The Cranes), Mfaransa Sebastien Desabre, ambayo ilitua jijini hapa kwa ndege binafsi, ilianza kwa kasi mchezo huo kwa dakika ya kwanza kufanya shambulizi lakini kipa wa Yanga, Farouk Shikalo, alifanikiwa kudaka shuti hilo lililopigwa na Mohammed Elgabbas "Dodo" na hivyo kuwanyima Waarabu hao bao la mapema.

Yanga iliyoonekana nayo kucheza mipira ya juu, ilijibu shambulizi hilo dakika ya 10 kupitia kwa beki wake, Ally Mtoni, lakini shuti lake la kushtukiza lilipanguliwa na kipa wa Pyramids, Ahmed El Shenawy.

Dakika moja baadaye Kelvin Yondani alifanikiwa kuokoa hatari katika lango la Yanga kwa kutoa mpira uliopigwa na Traore huku kipa Shikalo akiwa ameshapoteza "hesabu" katika eneo lake, lakini dakika iliyofuata alisawazisha makosa yake na kudaka mpira wa mwisho uliopigwa na Traore aliyepokea kutoka kwa Mohammed Fathy.

Ali Ali alikaribia kufunga lakini shuti lake lilipaa juu na hivyo kupoteza nafasi nyingine ya kuifungia Yanga bao dakika ya 22 baada ya mabeki wa Pyramids wakiwa wanadhani atatoa pasi kwa mchezaji mwenzake.

Feisal Salum "Feitoto" alikaribia kuifungia timu yake mabao dakika ya 57 na 68, lakini shuti lake la kwanza lilipaa juu ya lango na lingine likiishia mikononi mwa kipa wa Pyramids.

**NJE YA UWANJA**

Mashabiki wa Yanga kutoka jijini hapa, Dar es Salaam na mikoa ya jirani ambao walianza kuingia tangu saa 5:00 asubuhi, walishindwa kuujaza Uwanja wa CCM Kirumba ambao unaingiza mashabiki 22,000.

Mbali na kushindwa kuujaza uwanja huo, pia mashabiki wake walionekana kushindwa kuishangilia timu yao na kusikika mara chache pale wachezaji wao wanapofanya mashambulizi ama kupiga chenga.

Hata hivyo, mashabiki wachache wanaodhaniwa ni wa Simba, walionekana kuwa na shangwe zaidi na kuuteka uwanja kila wachezaji wa Pyramids walipokuwa wanafunga au wakionyesha soka safi katika mchezo huo uliochezeshwa na waamuzi kutoka Ivory Coast.

Pia wachuuzi wa jezi, chakula na vinywaji, walisema kuwa jana walipata wateja wengi tofauti na kiasi cha fedha wanachoingiza zinapochezwa mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Zikiwa zimebakia dakika chache, mashabiki wa Yanga walikuwa wakiimba kwamba hawamtaki Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera kuendelea kuifundisha timu yao.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002